بسم الله الرحمن الرحيم

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU
MWINGI WA REHMA MWENYE
KUREHEMU

ß‰ƒ Ì • ãƒ $ y J ¯R Î) ﴿
| = Ï dõ‹ã‹ Ï 9 ª ! $ #
ãNà6Z tã
}@÷d r & §ô_ Í h • 9 $ # Ÿ
Mø • t 7ø9 $ #
ö / ä . t • Î d gsÜãƒ u r
﴾ # ZŽ • Î g ôÜs?

(al-Ahzaab: 33).

Zimepokelewa hadithi nyingi sana katika vyanzo na maswadir za kisunni na kishia juu ya (Kuhusiana na) kuteremka kwa aya hii tukufu ikihusiana na watu watano As'habul-kisaa (a.s), na kuhusika kwa istilahi ya (Ahlul-baiti) na wao pekee, nao ni: Muhammad (s.a.w.w) na Ali, Fatima, Hasan na Husein (a.s), kwa mfano rejea vitabu vifuatavyo:

Musnad Ahmad (241 h): juzu 1 / 331, na juzu 4 / 107, juzu 6 / 292 na 304. Sahihi Muslim (261 h): juzu 7/ 130. Sunanut-tirmidhi (279 h): juzu 5/ 361 na vinginevyo.As-sunanul-kubraa cha Nasai (303 h): juzu 5 / 108 na 113.Adhuriyyatut-twahirah Annabawiyyah cha Duulabi (310 h): juzu 8 /.Al-mustadrak alaa swahihaini cha Bwana Al-haakim An-naisaburi (405 h): juzu 2 / 416, na juzu 3 / 133 na 146 na 147. Al-burhan cha Zarkashi (794 h): 197. Fat'hul-bari Sharhu swahihul-bukhari cha Ibnu Hajar Al-askalani (852 h): juzu 7 / 104. Usulul-kafi cha Kulaini (328 h): juzu 1 / 287. Al-imaamatu wat-tabswirah cha Ibnu Baabawaihi (329 h): 47, H 29. Daaimul-islaam cha Maghribi (363 h): 35 na 37. Al-khiswal cha Swaduuq (381 h): 403 na 550. Al-amali cha Tuusi (460 h): H 438 na 482 na 783 vile vile angalia tafsiri ya aya hii katika kitabu Jaamiul-bayan cha Twabari (310 h). Ahkaamul-qur'an cha Jaswaas (370 h). Asbabun-nuzuul cha Al-waahidi (468. Zaadul-masiir cha Ibnul-jawzi (597 h). Al-jaamiu liahkaamil-qur'an cha Qurtubi (671 h). Tafsiru ibnu kathiir (774 h). Tafsiruth-thaalabi (825 h). Ad-durrul-manthuur cha Suyuutwi (911 h). Fat'hul-qadiir cha Shaukani (1250 h). Tafsirul-ayyashi (320 h). Tafsiirul-qumi (329 H). Tafsiru Furati cha Al-kufi (352 h) chini ya aya ya Ulul-amri. Majmaul-bayan cha Twabrasi (560 h) na vyanzo vingine vingi.

IMANI YA KWELI YA WATU WA AFRIKA

قَالَ رَسُولُ اللهِ 3:

إِنِّي تَارِكٌ فِيكُمُ الثَّقَلَيْنِ: كِتَابَ اللهِ وَعِتْرَتِي أَهْلَ بَيْتِي، مَا إِنْ تَمَسَّكْتُمْ بِهِمَا لَنْ تَضِلُّوا بَعْدِي أَبَداً، وَإِنَّهُمَا لَنْ يَفْتَرِقَا حَتَّى يَرِدَا عَلَيَّ الْحَوْضَ.

Hakika mimi nimeacha miongoni mwenu vitu viwili vizito, Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kizazi changu Watu wa Nyumbani kwangu (Ahlul-Bait wangu), vitu ambavyo ikiwa mtashikamana navyo hamtapotea kamwe baada yangu na kwa hakika vitu viwili hivyo havitatengana :kamwe hadi vitakapo ingia kwangu kwenye Hodhi.

Imepokelewa kwa mfumo ulio karibiana katika Sahihi Muslim, juzu 7, ukurasa 122, Sunanud-daarimi, juzu 2 ukurasa 432, Musnad Ahmad, juzu 3, ukurasa 14,17, 26,59,na katika juzu 4, ukuras 366, 371, na juzu 5, ukurasa 182, Mustadrakul-haakim, juzu 3, ukurasa 109, 148, 533, na vyanzo vinginevyo.

(Inapatikana katika vitabu Sahihi na Masaaniid)

IMANI YA KWELI YA WATU WA AFRIKA

Mwandishi:

SAYYID MUHAMMAD HUSSEIN MURTADHA

Mtarjumi:

ABDULMAJID NASSIR

JUMUIYA YA KIMATAIFA YA AHLUL-BAIT (AS)

نام كتاب: الولاء الحقيقي
نويسنده: السيد محمد حسين مرتضى
مترجم: عبد الماجد ناصر
زبان ترجمه: سواحيلي

Jina la kitabu: IMANI YA KWELI YA WATU WA AFRIKA
Maudhui: Historia
Mtunzi: SAYYID MUHAMMAD HUSSEIN MURTADHA
Muandaaji: Ustadh Abdulmajid Nassir
Mtarjumi: Ustadh Abdulmajid Nassir
Mhakiki: Baraza
Upitiaji wa mwisho:
Mchapishaji:Kituo cha Uchapishaji na Usambazaji cha Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS)
Chapa ya: Kwanza
Chapa ya: Israa
Idadi ya chapa:3000
Tarehe ya Usambaji: 2008
Haki ya Usambaji imehifadhiwa na Msambazaji
ISBN : 978-964-529-364-0
www.ahl-ul-bayt.org
info@ahl-ul-bayt.org

YALIYOMO

TAMKO LA JUMUIYA YA AHLUL-BAIT.....13

TAMKO LA MUBALLIGH WA UJUMBE WA MWENYEZI MUNGU.....17

UTANGULIZI.....17

AFRIKA NI SHUKIO LA WAHYI (UFUNUO) 25

AFRIKA NI KITUO CHA HEKIMA NA MAHUKAMA (WANA HEKIMA).....27

LULU ILO PANGIKA KATIKA MAWAIDHA YA LUQMANIL- HAKIIM (AS) 44

WAFALME WA AFRIKA SI MADHALIMU NA ARDHI YA AFRIKA NI ARDHI YA UKWELI 73

UKWE WA MTUME MTUKUFU (SAW) KWA WATU WA AFRIKA.....87

MUUMINI WA KIAFRIKA NI TOSHELEZO LA MUUMINI YEYOTE.....93

MJA MWEMA, BILAL WA UHABESHI.....97

USAWA KATIKA UTOAJI WA AMIRIL-MUUMINIIN (AS) KATI YA MWEUPE, MWEUSI NA MWEKUNDU 111

KUOKOLEWA KWA MWANAMKE WA KIAFRIKA NA AMIRIL-MUMINIIN (AS) KUTOKANA NA ADHABU YA KUPOPOLEWA KWA MAWE 114

KUVUTIWA KWA FATUMA ZAHRAA (AS) NA BAADHI YA MILA NA ADA ZA KIARFIKA.....117

ADABU NA TABIA ZA MAIMAMU WA AHLUL-BAITI (AS) KWA WAAFRIKA.....120

KITENDO CHA MAIMAMU (AS) CHA KUWATAKA USHAURI WAAFRIKA 121

UJITOLEAJI MUHANGA WA WAAFRIKA ROHO ZAO KWA AJILI YA KUTETEA HESHIMA YA AHLUL-BAIT (AS) 125

FEDHAH MNUBI WA AFRIKA.....126

MWENYEZI MUNGU ANALO JESHI MIONGONI MWA WAAFRIKA LENYE KUWANUSURU AHLUL-BAITI (AS)133

KUSALLIM AMRI KIJANA WA KIAFRIKA MBELE YA AMRI YA MOLA WA VIUMBE NA KUZAMA NA KUJITOLEA UHAI WAKE KWA AJILI YA AMIRIL-MUUMINIIN (AS).....135

JOHN BIN HAWIYYU MTWANA WA ABI DHARRIL-GHIFARIY.....138

UKWE WA MAIMAMU MAASUMU WA AHLUL-BAIT (AS) KWA MATU WA AFRIKA.....141

HAMIDAH MBARBARI MAMA WA IMAM MUSAL-KAADHIM (AS) 141

NAJMAH WA MOROKO MAMA WA IMAM RIDHAA (AS) 146

SABIIKAH MNUBI MAMA WA IMAM JAWAAD (AS) ...149

SUMAANAH MMOROKO MAMA WA IMAM ALI AL-HADIY (AS).....153

HUDAITHU MAMA WA IMAM HASSAN ASKARI (AS)156

NAARJIS MAMA WA MTAWALA WA ZAMA HIZI IMAM WA KUMI NA MBILI 157

KUTOKEA KWA KUNDI LA WATU WEMA MIONGONI MWA WAAFRIKA PAMOJA NA IMAM AL-QAAIM (AS) ..159

ADAARISAH NA UENEZAJI WA UISLAMU ASILIA WA MUHAMMADIY KATIKA NCHI ZA AFRIKA 164

KUULIWA KWA MASHIA HUKO AFRIKA.....181

DOLA LA FAATIMIYYUN.....182

SHEKH MTUKUFU ADBUL-AZIZ AL-JAALUDIY MMOJA WA VIONGOZI WA MASHIA IMAMIYYAH KATIKA NCHI YA MOROKO 189

RAIHAAN WA UHABESHI NI KIGEZO KATIKA ZUHDI NA ADABU.....196

MSIMAMO WA KIPEKEE WA IMAM KHOMEIN KUHUSIANA NA WATU WA AFRIKA.....199

YANZO VILIVYOTEGEMEWA KATIKA UANDISHI WA KITABU HIKI 206

TAMKO LA JUMUIYA YA AHLUL-BAIT

Hakika urithi wa Ahlul-Bait (AS) ambao umehifadhiwa na madrasa yao, na wafuasi wake kuuhifadhi usipotee, unaelezea na kuibainisha ile madrasa iliyokusanya maarifa mbali mbali na ya aina tofauti ya Kiislamu.

Kwa hakika madrasa hii imeweza kulea nafsi na nyoyo zenye uwezo na maandalizi ya kunufaika na elimu hii kutoka kwenye mto huu wenye maji safi yenye kutiririka, na kuupatia Umma wa Kiislamu maulama wakubwa wenye kufuata nyendo na njia ya watu wa Nyumba ya Utume (Ahlul-Bait ar-Risaalah). Wameweza kujibu kwa njia bora na ya kukinaisha kabisa maswali na shubha za madhehebu na mielekeo mbali mbali ya kifikra iliyomo ndani na nje ya Uislamu katika kipindi chote cha historia na karne zilizopita.

Kwa hakika Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS) kutokana na majukumu yake iliyojitwisha mabegani, inatekeleza wajibu wa kutetea heshima na utukufu wa Uislamu na ukweli wake ambao umefunikwa na ukungu wa viongozi wa makundi, madhehebu na watu wenye mielekeo ya kuupinga Uislamu. Ili kufikia lengo hilo, imekuwa ikifuata njia ya Ahlul-Bait (AS) na wafuasi wa madrasa yao yenye uongofu ambayo wakati wote imekuwa ikijibu, bila kusita wala kuchoka, maswali na changamoto zinazotolewa mara kwa mara kutoka pande mbalimbali. Imejaribu wakati wote kuendelea kubaki katika njia ya mapambano na kwa kiwango kihitajikacho katika kila zama.

Hakika uzoefu na tajriba iliyohifadhiwa kwenye vitabu vya wanazuoni wa Madrasa ya Ahlul-Bait (AS) kuhusiana na maudhui hii ni wa kipekee, kwani ni uzoefu wenye njia na

nembo ya kielimu inayohukumiwa na akili na dalili za wazi, na unaojitenga na kujiepusha na matamanio binafsi na taasubi iliyo kemewa. Unawazungumzia na kuwahutubia maulama na wanafikra wenye ujuzi maalumu mazungumzo yenye kuipendeza na kuivutia akili na kukubaliwa na maumbile safi ya kila mtu.

Kwa hakika Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS) imejaribu kuwapatia watafuta-ukweli marhala na hatua mpya ya uzoefu huu ulio tajiri kupitia mijadala ya kielimu na vitabu kadhaa ambavyo hutungwa na kuandikwa na waandishi wa zama hizi kati ya watunzi wafuatao Madrasa ya Ahlul-Bait (AS), au watunzi ambao Mwenyezi Mungu amewaongoza na kuwapa taufiki kujiunga na madrasa hii tukufu. Mbali na hayo, Jumuiya pia imechukua jukumu la kusambaza na kuyafanyia utafiti mambo yenye faida kwenye tungo na vitabu vya maulama watukufu wa Kishia, wakiweo wa zamani, ili viwe chemchemi ya maji matamu kwa ajili ya kukata kiu ya nafsi zenye kutafuta haki na ukweli. Jambo hilo litawawezesha kufungukiwa na ukweli wa Madrasa ya Ahlul-Bait wa Mtume ulimwengu kote, katika zama hizi ambapo akili ni zenye kukamilika na kupevuka na nafsi na roho kuungana kwa kasi kubwa na kwa kiwango cha kushangaza.

Tunatoa shukurani zetu za dhati kwa mheshimiwa Sayyid Muhammad Hussein Murtadha kwa kuandika kitabu hiki na pia kwa ndugu wote waliochangia, kwa njia moja au nyingine, uchapishaji wake.

Ni matarajio yetu sote kuwa tumefanikiwa, kadiri ya uwezo wetu, kuchangia sehemu ya majukumu yaliyo mabegani kwetu kuhusiana na ujumbe wa Mola wetu Mtukufu ambaye alimtuma Mtume wake kwa uongofu na

dini iliyo ya kweli, ili aidhihirishe juu ya dini zote. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Shahidi wa yote.

Jumuiya ya Kimataifa ya Ahlul-Bait (AS)
Kitengo cha Utamaduni

TAMKO LA MUBALLIGH WA UJUMBE WA MWENYEZI MUNGU KATIKA NCHI YA NIJERIA MHESHIMIWA SHEKH MUHAMMAD NUURDAS WA NIJERIA

Sifa zote njema ni zake Mwenyezi Mungu Mola wa na muumba wa viumbe vyote na swala ziwe juu ya mbora wa viumbe wake Muhammad na Ahli Baiti wake ambao aliwaondolea uchafu na kuwatwaharisha kikamilifu.

Amesema Mwenyezi Mungu aliyetakasika na Mtukufu katika Kitabu chake Kitukufu:

ں ڻ ڻ ٹ ٹ ٹ

(Watu ni sawa na meno ya shanuo)[1]

Kufuatia kuja kwa Uislamu mwanadamu au mtu mweusi akapata nafasi ya kupumua kutokana na mafunzo ya dini hii tukufu na yenye baraka. Kwa ajili hiyo, watu weusi wakatoa mchango mkubwa na wa kupigiwa mfano katika kuitangaza na kuipeleka dini hii mbele.

Kitabu hiki kilichoko mikononi mwako ewe msomaji mpendwa, chenye jina la (IMANI YA KWELI YA WATU WA AFRIKA), kinazungumzia maudhui ya imani ya kweli ya dini ya Kiislamu na Uislamu wa kweli na wa asili uthibitikao na kudhihiri kwenye madhehebu ya Ahlil-Bait (AS) ambao alifaulu kuupata mtu mweusi tangu mwanzoni mwake.

Kitabu hiki ni natija ya juhudi na kazi kubwa aliyoifanywa ustadh mwenye ikhlasi Hujjatul-Islaam wal-Muslimiin Sayyid Muhammad Hussein Murtadha wa Lebanon ambaye wakati wote amekuwa akitufaidisha na elimu yake yenye nuru, pana na inayotokana na ikhlasi yake ya dhati.

Kwa hakika nimebahatika kuishi naye kwa muda wa miaka kumi takriban na sikuona kwake isipokuwa ikhlasi, unyenyekevu, kifua kipana, na mapenzi mengi ambayo huyaonyesha kwa ndugu zake weusi, ambao huhusiana naye. Hii ni pamoja na mambo mengine mengi ya kimaanawi ambayo hutufikia kutoka kwake na kutokana na vitabu vyake ambavyo vinazidi kumi.

Na mwisho ni juu yako ewe msomaji mtukufu kufaidika na fursa ya kusoma kitabu hiki ambacho kiko mbele yako ili uweze kupata faida katika nyumba mbili (ya dunia na

[1]-Nahjul-Faswaha, ukurasa 635.

akhera). Tunamuomba Mwenyezi Mungu aliyetakasika amuwafikishe ustadh wetu zaidi na zaidi.

Wasswalaam Alaikum Warahmatullahi Wabarakatuhu.

MUHAMMAD NUURDAS MNIJERIA – MJI MTAKATIFU WA QUM

UTANGULIZI

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye aliwafanya viumbe kuwa mataifa mbali mbali na makabila tofauti ili waweze kuelewana na akafanya kigezo cha utukufu wao kuwa ni ucha-Mungu (taqwa), kisha swala bora zaidi na maamkizi kamilifu yawe juu ya mtamkaji wa maneno haya:

أَلاَ لاَ فَضْلَ لِعَرَبِيٍّ عَلَى عِجْمِيٍّ وَلاَ عِجْمِيٍّ عَلَى عَرَبِيٍّ وَلاَ أَسْوَدَ عَلَى أَحْمَرَ وَلاَ أَحْمَرَ عَلَى أَسْوَدَ إِلاَّ بِالتَّقْوَى.

(Fahamuni ya kuwa, hakuna ubora wowote alionao Muarabu juu ya Muajemi (asiyekuwa Muarabu), wala hakuna ubora wowote wa Muajemi juu ya Muarabu, wala mweusi juu ya mwekundu, wala mwekundu juu ya mweusi isipokuwa kwa ucha-Mungu),[1]

yaani hitimisho la manabii na mitume na ambaye ni rehma ya Mwenyezi Mungu kwa walimwengu wote Muhammad bin Abdillahi rehma na amani iwe juu yake na juu ya Ahlil-Bait wake Maimamu waongofu na jahazi la uokovu, na laana ya milele iwe juu ya maadui zao, viumbe walio wabaya kabisa hapa ulimwenguni.

Amma baad: Hakika kuchanganyika na watu wa aina yoyote na kuishi nao kwa muda na zama fulani, humpelekea mtu kufahamu na kuelewa mambo mengi sana na maalumu yanayohusiana na itikadi na mmwenendo wa kimatendo wa watu hao.

Kutokana na haya, hakika kuishi kwangu kwa karibu na ndugu zangu wa Kiafrika na kuchanganyika nao kwa zaidi

[1]-Al-jaamiu liahkaamil-qur'anil-kariim juzu 16\ 223.

ya miaka kumi kwa urafiki na kwa kuwafundisha, na kutokana na kusoma kwangu kwingi vitabu vinavyohusiana na watu hawa watukufu na wenye fadhila, kulinifanya niweze kutambua na kuona kwenye dhati zao imani yao halisi kwa Mwenyezi Mungu aliyetakasika na Ahlil-Bait wake walio watwaharifu na maasumiina (AS), zamani na hivi sasa.

Kwa hakika kulikuwa na manabii na mitume katika ardhi yao na baadhi yao walikuwa ni mitume ulul-azmi kama vile Nabii Mussa (AS). Kulikuwepo pia na mahukamaa (watu wenye hekima na busara) watokanao na Waafrika waliofunzwa na Mwenyezi Mungu na wakapewa hekima kwa kufika kwao kwenye kilele cha ukamilifu kama vile Luqmanil-Hakiim (aliyepewa hekima). Walikuwa ni wenye kumuamini Mtume wetu Mtukufu (SAW) na mafunzo yake ya kweli kwani walifahamika kutokana na ikhlasi yao na kusalimu amri kwao mbele ya amri zake zote, mfano akiwa ni Bilal al-Habashi (Muhabeshi) (radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu ziwe juu yake) na wenye ada nzuri zilizompendeza na kumvutia binti wa Mtume Fatwimah (AS) na kumpelekea kuzitekeleza na kuzifuata. Maswahaba kutoka barani humo pia walikuwa ni wafuasi wazuri wa Ahlil-Bait (AS). Walifahamika kwa mapenzi yao ya kiwango cha juu kwa Maimamu Watoharifu kama vile John bin Hawiyyi, mtwana wa Abu Dharri al-Ghafariy (amani ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake) na ambaye alikufa shahidi katika uwanja wa mapambano dhidi ya dhulma akiwa na Abi Abdillahill-Hussein (AS) katika uwanja wa Karbala. Wao pia ni katika askari wa jeshi la Imamu wetu wa Zama (Mwenyezi Mungu aharakishe kudhihiri kwake) linaloongozwa na Imam Khomeini (rehma ya Allah iwe juu

yake na utawala wake wenye baraka). Yote haya yalitupelekea kuamua kubainisha na kufafanua zaidi nafasi ya watu wa bara hili ili kuwarejeshea watu hawa wazuri na wema haki yao ambayo walinyang'anywa na kuporwa tokea huko nyuma hadi hivi leo pamoja na kukandamizwa kwa kipindi chote cha historia.

Na hayakufanyika hayo isipokuwa ni kutokana na rangi ya ngozi ya mtu mweusi ambayo ni mojawapo ya alama na ishara za kuwepo Mwenyezi Mungu ili awatie viumbe majaribuni na kumfahamu ni yupi mwenye matendo mazuri zaidi. Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

ں ڻ ڻ ڈ ڈ ۋ ۋ ۅ ۅ ۉ ۉ ې ې ۍ ۍ

(Na miongoni mwa alama (ishara) zake ni kuumba mbingu na ardhi na kutofautiana kwa lugha na rangi zenu. Hakika katika hayo kuna ishara kwa wenye elimu (wenye kufahamu).[1]

Na amesema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu:

ۏ ۏ ې ې ۑ ۑ ے ے ۓ ۓ ۔ ۔

(Na miongoni mwa watu na wanyama wanaotambaa na wanyama (wengine), pia rangi zao ni tofauti. Kwa hakika wanaomwogopa Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni: Bila shaka Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na msamehevu.[2]

Ni jambo lililo wazi (lisilofichika) kuwa vigezo na mizani ya ukemeaji, usifiaji, uchukiaji na kuvutiwa au kupendezwa na kitu hutokana na matendo ambayo hutokakana na hiari pamoja na utashi wa mwanadamu. Ama mambo ambayo huwa nje ya uwezo wake na yanayofungamana na kuumbwa kwake hayapaswi kukemewa, kudhauriwa wala kufanyiwa

[1]-Suuratur-Ruum aya 22.
[2]-Suurat Faatwir aya 28.

kejeli, na hasa tunapotambua kwamba mambo kama hayo huwa yanatokana moja kwa moja na mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Naam, mtu mwenye akili timammu ni yule anayefanya juhudi za kuzuia uso wake usiwe mweusi Siku ya Kiama hata kama atakuwa ni mweupe hapa duniani.

Mwenyezi Mungu anasema katika Kitabu chake Kitakatifu:

ۇ ۇ ۆ ۆ ۈ ۈ ۇٴ ۋ ۋ ۅ ۅ ۉ ۉ ې ې ۋ ۋ

Siku ambayo nyuso zitakuwa nyeupe na zingine kuwa nyeusi. Ama wale ambao nyuso zao zitakuwa nyeusi wataambiwa; "Je, mlikufuru baada ya kuamini kwenu? Basi onjeni adhabu kwa yale mliyokuwa mkiyakufuru." Na ama wale ambao nyuso zao zitakuwa nyeupe, watakuwa katika rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao watakaa humo milele.)[1]

Ni kwa sababu hiyo ndio maana kila mara Mtume Mtukufu na Maimamu (AS) walipokuwa wakitaka kutawadha au kuosha nyuso zao walikuwa wakisema:

اَللَّهُمَّ بَيِّضْ وَجْهِي يَوْمَ تَسْوَدُّ فِيهِ الْوُجُوهُ وَلاَ تُسَوِّدْ وَجْهِي يَوْمَ تَبْيَضُّ فِيهِ الْوُجُوهُ.

(Ewe Mwenyezi Mungu! Ufanye uso wangu uwe mweupe siku ambayo nyuso zitakuwa nyeusi na wala usiufanye uso wangu kuwa mweusi siku ambayo nyuso zitakuwa nyeupe).[2]

Ni jambo lililo wazi kwamba, wale ambao huwafanyia maskhara wenzao kutokana na rangi yao na mfano wa hayo

[1]-Suurat Aaali Imraan aya 106-108.
[2]-Wasaailush-Shia juzu 1 \ mlango wa 16 kati ya milango ya udhu.

itawajia siku ambayo wao pia watafanyiwa maskhara, tena yaliyo makubwa na mabaya zaidi kuliko hayo wanayowafanyia wenzao. Mwenyezi Mungu akisimulia kisa cha Nabii Nuhu (AS) anasema:



(Ikiwa mnatufanyia maskhara (mnatucheka) na sisi tutaku-fanyieni maskhara (tutakuchekeni) kama mnavyotufanyia maskhara).[1]

Pia amesema:

(Kwa hakika wale ambao walifanya madhambi walikuwa wakiwacheka walioamini. Na pindi wanapopita karibu yao hukonyezana. Na wanapo rudi kwa jamaa zao, hurudi wakifanya mizaha na kufurahi (kwa kuwaudhi). Basi leo wale walioamini wanawacheka makafiri).[2]

Kwa hivyo basi sheria yetu takasifu na mafundisho ya Ahlil-Bait walio maasumu na watoharifu (AS), yote hayo yalikuja ili kusisitiza yafuatayo: Hakika muumini ni mweupe hata kama atakuwa na ngozi nyesi, na kafiri fasiki na muovu mwenye kuwafanyia wenzake stihizai ni mweusi hata kama atakuwa na rangi nyeupe, na muumini wa kike ni Hurul-aini hata kama atakuwa ni kijakazi wa uhabeshi.

Inasimuliwa kuwa kulikuwa na mtu mmoja miongoni mwa masayyid na watu wajinasibishao kwenye kizazi cha Mtume Mtukufu (SAW) ambaye alikuwa muovu na fasiki akifanya ufuska wake dhahiri na bayana. Katika upande wa pili kulikuwepo na mtu mwingine Muafrika mweusi ambaye alikuwa na daraja la juu katika elimu na matendo mema na akitekeleza vyema sheria ya Mtume (SAW), na watu kumuadhimisha na kumtukuza na kumuheshimu

[1]-Suurat Huud aya 38.
[2]-Suuratul-Mutwaffifiin aya 29-34.

sana. Siku moja Mwafrika huyo alitoka nyumbani kwake kwenda msikitini kwa ajili ya ibada huku akifuatwa na kundi kubwa la watu wakitabarruku naye. Mara akakutana na muovu yule ambaye alikuwa ni katika kizazi cha Mtume huku akiwa amelewa na watu wakimfukuza atoke kwenye njia aliyokuwa akipitia yule aalimu Mwafrika. Yule bwana akawazidi nguvu na kushika nguo za yule muumini wa Kiafrika na akasema: 'Ewe mweusi wa kwato (miguu) na midomo! [1] Ewe kafiri mtoto wa kafiri! Mimi ni mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW). Ninadhalilishwa na kudharauliwa na wewe ukitukuzwa na kuheshimiwa (kusaidiwa)'? Hapo watu wakamgeukia kwa kipigo. Yule muumini Mwafrika akawawasihi wasifanye hivyo kutokana na heshima ya babu yake (SAW). Alisema, ilipasa kumsamehe japokuwa alikuwa amevuka mipaka. kisha akamuelekea yule sayyid na kumwambia: 'Hakika nimekufanya kweupe ndani ya dhamiri yangu na ndani yangu na wewe umekufanya kweusi ndani ya dhamiri yako na moyoni mwako. Kwa hivyo, weupe wa moyo wangu unaonekana juu ya weusi wa uso wangu na nikawa mzuri mwenye kupendeza, na weusi wa moyo wako uko juu ya weupe wa uso wako na kukufanya wewe kuwa mbaya. Nimechukua mwenendo wa baba yako na wewe ukachukua mwenendo wa baba yangu, kwa hivyo watu wakaniona nikiwa katika mwenendo wa baba yako na wakakuona wewe ukiwa katika mwenendo wa baba yangu. Wakanidhania mimi kuwa ni mtoto wa baba yako na wakakudhania wewe kuwa ni mtoto wa baba yangu. Wakakufanyia mambo waliyokuwa wakimfanyia baba yangu na wakanifanyia mimi mambo ambayo walikuwa

[1]-Akiashiria kuwa miguu yake na midomo yake ni myeusi.

wakimfanyia baba yako.'

Kwa vyovyote vile, tunamuomba Mwenyezi Mungu atuwafikishe sisi sote kutekeleza matendo kwa mujibu wa mafunzo ya Mtume wetu Mtukufu (SAW) na atufufue pamoja naye, hakika yeye ni msikivu sana na mwenye kuitikia na kujibu maombi.

MUHAMMAD HUSSEIN MURTADHA -
MJI MTAKATIFU WA QUM

AFRIKA NI SHUKIO LA WAHYI (UFUNUO)

Nchi za Kiafrika huzingatiwa kuwa ni miongoni mwa nchi tajiri kwa manabii na mitume na hasa nchi ya Misri ambayo imetajwa katika Qur’an tukufu na katika aya nyingi za Qur'ani Tukufu. Amesema Mwenyezi Mungu aliyetakasika:

ۓ ۋ ۅ ۉ ۇ ۆ ۈ ۇٴ ۋٴ ۅٴ ۉٴ ېٴ ېٴ

Na tuliteremshia wahyi Musa na ndugu yake ya kwamba waandalieni na watengenezeni watu na kaumu zenu katika mji nyumba (ya kuishi au ya ibada) na zifanyeni nyumba zenu kuwa ni misikiti na simamisheni swala. Na uwape waumini bishara njema ya ushindi na pepo. [1]

Na amesema Mwenyezi Mungu kuhusiana na Nabii Yusuf (AS):

ۓ ۀ ۀ ۂ ۂ ۅ ۅ ۉ ۉ ۇ ۇ ۆ

Na akasema yule ambaye alimnunua kutoka Misri kumwambia mkewe mkirimu: "Mtengenezee mahala pazuri pa kufikia huenda akatufaa au tukamfanya kuwa mtoto wetu."[2]

Na katika sehemu nyingine akimuashiria na kumuelezea Nabii Yaaqub (AS) na watoto wake anasema Mwenyezi Mungu:

ۆ ۈ ۈ ۇٴ ۋٴ ۅٴ ۉٴ ېٴ ېٴ ۆ

Na pindi walipoingia kwa Yusuf akawakumbatia wazazi wake (akawakaribisha kuwaweka kwake) na akasema: "Ingieni katika mji wa Misri Inshaallah mumo katika

[1]-Suurat Yunus aya 87.
[2]-Suurat-Yusuf aya 21.

amani."[1]

Kwa hivyo kama tutaipekua Qur’an Tukufu kwa makini tutakuta kuwa imekusanya na kutaja idadi nzuri tu ya mitume waliokuwa Afrika na wakiongozwa na Nabii Musa (AS) ambaye huzingatiwa kuwa ni katika mitume Ulul-Azmi-yaani alikuja na kuleta sheria mpya iliyofuta sheria za wale waliomtangulia. Hii ina maana kuwa nchi hizo zimebeba watu walio wema na wazuri na nafsi njema ziwezazo kuzifikisha nchi hizo kwenye daraja na vyeo vitukufu na mambo mema.

Na mashukio ya wahyi hayakuhusika tu na wanaume wao bali yaliwahusu pia wanawake japokuwa kwa aina na namna tofauti. Amesema Mwenyezi Mungu:

ۆ ۈ ۈ ۇٴ ۋٴ ۅٴ ۉٴ ېٴ ېٴ ۆ

Na tulimfunulia mama yake Musa (tuliutia fahamu moyo wake) ya kwamba mnyonyeshe na ikiwa utamuogopea hatari, basi mtie (mtumbukize) mtoni na wala usiogope wala kuhuzunika, kwa hakika sisi tutamrudisha kwako na tutamfanya kuwa miongoni mwa mitume.[2]

[1]-Suurat Yusuf aya 99.
[2]-Suuratul-Qaswas aya 7.

AFRIKA NI KITUO CHA HEKIMA NA MAHUKAMA (WANA HEKIMA)

Hekima kwa wanahekima ilifahamika na kuarifishwa kuwa ni ukamilifu wa nafsi ya mwanadamu kwa kujipamba na elimu za kinadharia na kupata uwezo kamili juu ya matendo mema na bora kwa kadri ya uwezo wake, au kufahamu na kuwa na elimu ya ukweli kama ulivyo. Elimu yenyewe ni nuru na huvitia nuru vitu vingine[1]. Kutokana na kuwa hekima huchukua jukumu la kujenga na kuimarisha nyumba mbili na hufanya hivyo kwa kuzijenga na kuziimarisha nguvu mbili ilihitajia nadharia ya tajarrudi (Kutoambatana na mwili) ihusianayo na nafsi ya mwanadam iliyo mujarradah, (isiyokuwa na mahusiano na mwili), na kuhitajia kazi ya maambatano ya kimaumbile yahusianayo na mwili wa mtu au mwanadamu.[2]

Na hekima hii na pande zake mbili alipewa Luqman Hakiim na Mwenye Mungu Mjuzi na Mwenye Hekima. Anesema:

ٱ ب ب ٻ ٻ پ پ پ پ پ ڀ ڀ ٺ ٺ ٺ ٺ ٽ ٽ

Na kwa hakika tulimpa Luqman hekima (tukamwambia) ya kwamba mshukuru Mwenyezi Mungu; na mwenye kushukuru kwa hakika hushukuru kwa ajili ya nafsi yake, na mwenye kukufuru hakika Mwenyezi Mungu ni mkwasi na mwenye kuhimidiwa (juu ya neema azitoazo).[3]

---

[1]-Angalia maelezo ya kitabu Fususul-Hikam cha Qaiswariy, Fassi ya kwanza ya Yusufi juzuu 1 \ 459.

[2]-Ili kuelewa kwa upana zaidi rejea Kitabul-Asfaar, Safari ya kwanza, Maslakul-Awwal ukurasa 20.

[3]-Suurat Luqman aya 12.

Mfasiri na mwanazuoni mashuhuri wa fiqhi Ali bin Ibrahiim al-Qumiy (Mwenyezi Mungu amrehemu - mmoja wa wanazuoni wakubwa wa karne ya tatu na nne Hijiria) amepokea hadithi kutoka kwa Hussein bin Muhammad kutoka kwa Mualla bin Muhammad kutoka kwa Ali bin Muhammad kutoka kwa Bakri bin Swaleh kutoka kwa Jaafar bin Yahya kutoka kwa Ali bin An-Nadhri kutoka kwa Abi Abdillahi (AS) akisema: " Nilimuuliza: Nifanywe kuwa fidia yako, nini maana ya kauli ya Mwenyezi Mungu isemayo:

ٱ ب ب ٻ

(Kwa hakika tulimpa Luqmani hekima).[1]

Akasema: Alipewa maarifa ya kumfahamu Imamu wa zama zake.[2]

Tunasema: Kumfahamu Imamu wa Zama ni miongoni mwa vielelezo vya wazi kabisa na muhimu vya hekima. Ni kutokana na ukweli huo ndio maana madhehebu na makundi mbali mbali ya Kiislamu yakanukuu riwaya kutoka kwa Mtume Mtukufu (SAW) ya kwamba:

مَنْ مَاتَ وَلَمْ يَعْرِفْ إِمَامَ زَمَانِهِ مَاتَ مِيتَةً جَاهِلِيَّةً.

Mtu anayekufa bila ya kumfahamu imamu wa zama zake atakuwa amekufa kifo cha kijahili (kifo cha kikafiri).[3]

Na ni jambo lililo wazi ya kwamba, Luqman Hakiim alikuwa ni mja wa Uhabeshi nchi iliyoko Afrika ya Mashariki ifahamikayo hivi leo kama Ethiopia na sehemu moja wapo kati ya milima ya Unubini (An-Nuubah).

---

[1]- Tafsiirul-Qumiy juzuu 2 \ 161

[2]- Tafsiirul-Qumiy juzuu 2 \ 161

[3]- Angalia Musnad Ahmad juzuu 4 \ 94- Usuulul-Kafiy juzuu 1\ 376, na juzuu 2 \ 208- al-Miiyar wal-Muwazanah: 24- Sharhul-Maqaasid juzuu 2 \ 275- Asraarul-Imaamah: 318 na vinginevyo.

Kwa hakika mwanahistoria mkubwa na mtukufu Abu Hassan Ali bin Hussein bin Ali al-Masoudiy: (aliyefariki dunia mwaka 346 h) amesema ya kuwa Luqman Hakiim ni Luqman bin Unqaa'u bin Marbad bin Swaaruun, na alikuwa ni Mnubi mtumwa na mtwana wa Laqqiin bin Jisr. Alizawa miaka kumi tangu kusimama utawala wa Nabii Daud (AS), na alikuwa ni mja mwema, Mwenyezi Mungu akamneemesha kwa kumpa hekima. Aliendelea kuishi duniani akionyesha na kudhihirisha hekima na ucha-Mungu (Zuhdi) ulimwenguni hadi katika zama za NabiiYunus bin Mataa (AS) ambapo alipotumwa huko Nainawa katika ardhi ya Muuswil (iliyo huko Iraq).[1]

Na Allamah mwanahekima na mwanafalsafa mcha-Mungu Swadrudin ash-Shiraziy (Mwenyezi Mungu autukuze utajo wake aliyezaliwa mwaka 1050 h) amesema ya kwamba: Luqman ni mtoto wa Baura kati ya watoto wa Zariin dada wa Ayub (AS) au shangazi yake. Na Abu Laith akasema ya kuwa hakika Kun'ya ya Luqman ni Abul-An'am, na katika kitabu Ainul-Maaniy inasemekana kwamba alizaliwa miaka kumi tangu kusimama utawala wa Nabii Daudi (AS) na akaishi hadi kukutana na kumdiriki NabiiYuunus (AS). Inasemekana ya kuwa aliishi miaka elfu moja na wataalamu wametofautia kuhusu utume wake. Maulama walio wengi wanasema kuwa hakuwa mtume, na kwamba alikuwa mtumwa. Wanasema alikuwa ni Mhabeshi mwenye rangi nyeusi mwenye midomo migumu. Miongoni mwa hekima zake ni kuwa alifuatana na Nabii Daudi (AS) kwa muda wa miezi kadhaa huku akitengeneza vazi maalumu litumiwalo kwenye vita[2], na hakumuuliza kuhusu vazi hilo. Pindi

[1]-Murujudh-Dhahab juzuu 1 \ 70.
[2]-yaani akizitia nakshi.

alipomaliza kulitengeneza akalivaa na akasema: "Uzuri wako ulioje ewe vazi la kivita! Akasema: Kunyamaza ni hekima na ni wachache sana wafanyao hivyo."[1]

Na katika kitabu Durrul-Manthur Suyutwiy (aliyefariki dunia mwaka 911 h) anamnukuu Ibnu Abbas (Radhi za Allah ziwe juu yao) kwamba: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW):

إِتَّخِذُوا السُّودَانَ فَإِنَّ ثَلاَثَةً مِنْهُمْ سَادَاتُ أَهْلِ الْجَنَّةِ؛ لُقْمَانَ الْحَكِيمَ وَالنَّجَاشِيَّ وَبِلاَلَ الْمُؤَذِّنَ.

(Shikamaneni na Sudan (watu weusi) hakika watu watatu miongoni mwao ni masayyid wa watu wa peponi Luqman al-Hakiim, Najaashiy na Bilal muadhini).[2]

Na amepokea hadithi bwana Muhammad bin Muhammad bin al-Ash'ath al-Kufiy kwamba: Alitwambia Abdallah, kutoka kwa Muhammad, kutoka kwa Musa, akisema: Tulisimuliwa na baba yangu, kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake Jaafar bin Muhammad, kutoka kwa Baba yake, kutoka kwa babu yake Ali bin Hussein, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Ali bin Abi Twaalib (AS) ya kwamba amesema:... wa mwanzo kati ya waandishi ni (Luqmaanul-Hakiim) na alikuwa ni mtumwa mhabeshi[3]

Na riwaya zinazosema kwamba Luqman alikuwa ni Mwafrika ni nyingi sana kutoka pande mbili na kwa kuzitegemea riwaya hizo maulamaa wa Kiislamu wakashikamana na kauli hiyo, isipokuwa ni kwamba

[1]-Sharhu Usuulul-Kafiy: ukurasa 55 chapa ya Hajariyyah.
[2]-ad-Durrul-Manthuur cha Suyuutwiy juzuu 5 \ 160 chini ya aya 12 ya Suurat Luqman.
[3]-Qurbul-Isnaad wal-Jaafariyyaati ukurasa 392-kutoka kwake al-Mustadrak lil-Wasaail juzuu 16-mlango 16 kati ya ya a--Mukaatabah, juzuu 2.

ilijitokeza tofauti kuhusiana na iwapo alikuwa ni mtume au walii kati ya mawalii wa Mwenyezi Mungu.

Kwa hakika amesema mwanairfani Sayyid Jalaaluddin al-Ishtiyaaniy (Mwenyezi Mungu arefushe umri wake) ya mwamba maulamaa wakubwa waliowengi wanaitakidi ya kuwa Luqman alikuwa ni walii kwa sababu yeye alipewa hekima na Mwenyezi Mungu.

Na imesemekana ya kuwa yeye (AS) alikuwa ni nabii, na inayathibitisha hayo kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(Na mwenye kupewa hekima kwa hakika amepewa kheri nyingi).[1] Yaani kheri isiyokuwa na kikomo.

Yeye (AS), alikuwa mtumwa wa Kihabeshi wa Nabii Daudi (AS), na Mwenyezi Mungu akampatia hekima, na kumuweka kwenye daraja hilo na cheo hiki cha kupewa, kisicho cha kutafuta kwa juhudi binafsi.

Mwenyezi Mungu akampa kheri nyingi kutokana na aliyokuwa akiyastahiki kwa dhati yake. Na asiyekubali utume wake, hana budi kukiri na kukubali uwalii wake.[2]

Tunasema: Inadhihiri kutokakana na mwanairifani huyu mkubwa Muhyiddini al-Arabiy kwamba aliamini kuwa Luqman Hakiim alikuwa ni mtume na hayo ni kutokana na kumtaja kwake pamoja na mitume au manabii katika kitabu chake Fusuus kwani alitoa anwani ifuatayo:

حِكْمَةٌ إِحْسَانِيَّةٌ فِي كَلِمَةٍ لُقْمَانِيَّةٍ.

Vyovyote itakavyokuwa, imepokelewa kutoka kwa Ahlil-

[1]-Suuratul-Baqarah aya 269.

[2]-Sharhu Fusuusul-Hikam pamoja na maelezo ya Sayyid Jalaalddini al-Ishtiyaaniy ukurasa 1085.

Bait (AS) kuhusu utukufu wa Luqman, mambo yanayotufanya tulazimike kumfuata kama kigezo huenda jambo hiulo likatufanya tufarajike na matone machache ya hekima yake kubwa, tukufu na yenye baraka.

Kwa hakika mfasiri na mwanafiqhi mkweli na wa kuaminika Abul-Hassan Ali bin Ibrahiim al-Qumiy-ambaye alikuwa miongoni mwa maulamaa wakubwa wa karne ya tatu na nne Hijiria, amepokea na kusimulia hadithi kutoka kwa baba yake Ibrahiim bin Haashim, kutoka kwa Qaasim bin Muhammad, kutoka kwa Suleiman bin Daud al-Manqariy, kutoka kwa Hammad kwamba: Nilimuuliza Aba Abdillahi (AS) kuhusiana na Luqman na hekima yake ambayo Mwenyezi Mungu aliitaja, akasema:

Ama ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Luqman hakupewa hekima kutokana na hadhi yake, wala mali, wala kutokana na jamaa, wala kutokana na nguvu nyingi za kimwili, wala kutokana na uzuri bali alikuwa ni mtu mwenye nguvu katika kutekeleza amri za Mwenyezi Mungu, mwenye kujizuia na mambo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mwenye kunyamaza na mtulivu, mwenye mtazamo wa kina, mwenye kufikiri sana, mwenye mtizamo mkali na wenye mazingatio na mwenye kujitosheleza kutokana na mazingatio. Hakuwahi kulala mchana kamwe, na hakuna mtu yeyote aliyemuona akijisaida haja ndogo wala kubwa wala akioga kutokana na kujisitiri kwake sana, kwa mtazamo wake wa kina na kutokana na kujihifadhi na kujisitiri katika mambo yake. Wala hakushika kitu chochote kwa kuogopa madhambi, hakuchukia kamwe wala kumfanyia mzaha mtu yeyote. Hakufurahia kitu chochote kilichohusiana na dunia wala kukihuzunikia kitu chochote. Alioa wanawake na kuzaliwa watoto wengi na

kuwatoa wengi wao muhanga kwa kuvuka mipaka [1], na wala hakulia kwa kifo cha yeyote kati yao. Hakupita kando ya watu wawili wakigombana au wakipigana isipokuwa alikuwa akiwasuluhisha na kuwaacha wakiwa wamependana.[2] Hakusikia kauli kutoka kwa mtu yeyote akapendezwa nayo bila ya kuuliza tafsiri yake na ilikotoka. Alikuwa akikaa sana kwenye vikao vya mafuqahau na watu wenye hekima. Alikuwa akiwaogopa mahakimu na wafalme na watawala, na akiwalilia na kuwahuzunikia mahakimu kutokana na mambo waliyotihaniwa nayo. Akiwarehemu watawala na wafalme kwa kujitukuza kwao kwa jina la Mwenyezi Mungu na kuwa kwao na matumaini katika hilo. Akipata mazingatio na kujifunza yale yaizidiayo nafsi yake na kuyapinga matamanio ya nafsi yake kwa mazingatio hayo na akiyatumia kujikinga na kujihadhari na shetani. Alikuwa akiutibu moyo wake kwa kufikiri na nafsi yake kwa mazingatio. Hakuyakubali mambo ila yale yaliyomnufaisha, na kutokana na hilo akapewa hekima na ismah. Mwenyezi Mungu aliyaamuru makundi ya malaika wakati ilipofika nusu ya mchana na macho kutulia kwa usingizi wakamuita Luqman huku akiwasikia isipokuwa tu hakuwaona wakasema: Ewe Luqman! Je, unaridhia Mwenyezi Mungu akufanye wewe uwe khalifa katika ardhi na uhukumu kati ya watu? Luqman akasema: Ikiwa Mwenyezi Mungu ataniamuru kufanya hivyo basi nitasikiliza na kutii kwa sababu yeye ikiwa atanifanya hivyo atanisaidia katika hilo na atanifunza na kunilinda na ikiwa atanihiyarisha basi nitachagua lililo na afya na uswalama ndani yake.

Malaika wakasema: Ewe Luqman kwa nini umesema

[1]-Huenda: wengi wao walikufa kwa kuvuka mipaka.
[2]-Huenda: wakiheshimiana wao kwa wao.

hivyo? Akasema: Kwa sababu kuwaongoza na kuhukumu kati ya watu ni kati ya vyeo vikubwa sana katika dini. Ni cheo chenye fitina na mabalaa mengi, hatelekezwi wala kunusurika kutokana na dhulma kutoka kila upande. Mwenye cheo hicho huwa kati ya mambo mawili. Ikiwa atasibu haki kwenye jambo hilo basi atakuwa amesalimika na ikiwa atakosea basi atakuwa ameikosea njia ya kwenda peponi. Mwenye kuwa dhalili na dhaifu duniani hesabu yake itakuwa nyepesi katika akhera. Kuwa katika akhera ni muamuzi ya mwenye daraja na sharafu ya juu kabisa. Mwenye kuchagua dunia na kuiacha akhera atapata hasara ya vitu vyote hivyo viwili hiki kitamuondokea na asikidiriki na kukipata kile kingine. Akasema:

Malaika wakastaajabu kutokana na hekima yake na Mwenyezi Mungu akapendezewa na kufurahishwa na maneno yake. Na ulipofika wakati wa usiku Mwenyezi Mungu akamteremshia hekima na kumfunika kwa hekima hiyo kuanzia kichwani hadi unyayoni mwake huku akiwa amelala. Alimfunika kwa funiko la hekima na akaamka huku akiwa ni mwenye hekima kubwa zaidi miongoni mwa watu wa zama zake, na akatoka kwa watu akitamka hekima na akiieneza na kuitawanya kati yao.[1]

Kuhusiana na suala hilo alimwambia mtu mmoja aliyekuwa akimtazama: Ikiwa unaniona ni mwenye midomo migumu kwa hakika hutoka kwenye midomo hiyo maneno laini na mazuri yenye kuvutia, na ikiwa waniona mweusi basi elewa ya kuwa moyo wangu ni mweupe.[2]

Imepokelewa kwamba umri wa Luqman ulifikia miaka

[1]-Tafsiirul-Qumiy juzuu 2 \ 162.
[2]-Tafsiirul-Kashaf juzuu 3 \ 493-Jaamiul-Ahkaamil-Qur'an juzuu 14 \ 41.

elfu tatu na mia tano (3500), na aliambiwa na kuulizwa: Je, wewe si mtumwa wa familia ya fulani? Akasema: ndio. Akaulizwa: Ni jambo gani lililokufikisha kwenye daraja hili tulionalo? Akasema: Ukweli wa mazungumzo, na kutekeleza amana na kutojishughulisha na yasiyonihusu.[1]

Na imepokelewa ya kwamba mtu mmoja alisimama kwenye kikao chake na kusema: Je, si wewe unachunga mifugo pamoja na mimi mahala fulani? Akasema: Ndio. Akasema: Ni jambo gani lililo kufikisha kwenye daraja hili nilionalo? Akasema: Ukweli katika mazungumzo (kuwa mkweli) na kuyanyamazia yasiyonihusu.[2]

Imesemekana: Alikuwa ni mchungaji na kauli hii inaungwa mkono na hayo yaliyotangulia. Isemekena pia: Alikuwa ni fundi cherehani na kauli nyingine inasema alikuwa ni fundi seremala. Akaambiwa na sayyid au bwana wake: Nichinjie mbuzi mmoja na uniletee mapande mawili ya nyama yaliyo mazuri sana (au mapande mawili ya nyama), akamletea ulimi na moyo. Akamwambia: Je, hakukuwa na nyama iliyo nzuri zaidi kuliko hivi vitu viwili ulivyoniletea? Akanyamaza kidogo, kisha akamuamuru achinje mbuzi mwingine kisha akamwambia: Tupa vipande viwili vya nyama vilivyokuwa vibaya zaidi, akatupa ulimi na moyo. Akamwambia: Nimekuamuru uniletee vipande viwili vya nyama vilivyo kuwa vizuri ukaniletea ulimi na moyo, na nikakuamuru uniletee vipande viwili vya nyama vibaya zaidi na ukatupa ulimi na moyo! Akamwambia: Kwa hakika hakuna kitu kizuri zaidi kuliko vitu hivyo viwili pindi vinapokuwa vizuri, na hakuna vitu vibaya sana kuliko vitu

[1]-Bahrul-Maarif juzuu 2 \ 144.
[2]-chanzo kilicho tangulia.

viwili hivyo pindi vinapokuwa vibaya.[1]

Inasemekana kuwa: Luqmani alirudi kutoka safarini, akakutana na mtumwa wake, akasema: baba yangu amefanya nini? Akasema: Amekufa: Akasema: Ewe bwana wangu unayemiliki jambo (hatima) langu, mama yangu amefanya nini? Akasema: Amekufa. Akasema: Hima yangu yote imepotea na kuondoka, na dada yangu amefanya nini? Akasema: Amekufa. Akasema: Umesitirika uchi wangu (sehemu zangu za siri), akasema: na mke wangu amefanya nini? Akasema: Amekufa. Akasema: Umelijadidi na kulifanya jipya tandiko langu, na kaka yangu amefanya nini? Akasema: Amekufa. Akasema: Ohoo! Mgongo wangu umevunjika (umekatika kwa maana nguvu zangu zimekwisha).[2]

Na Ibnul-Mundhir amemnuku Akramah akisema: Hakika jambo la kwanza lililopokelewa kati ya hekima za Luqman ni kwamba wakati alipokuwa na bwana wake ghafla aliingia chooni na kukaa sana au kwa muda mrefu huko. Luqman akamuita mtu huyo na kusema hakika kukaa sana chooni huathiri maini na husabaisha kutokwa na bawasiri[3] na husababisha kupanda kwa joto kichwani kwa hivyo basi kaa kidogo na utoke. Akatoka na kuandika hekima yake juu ya

[1]-al-Jaamiu Liahkaamil-Qur'an juzuu 14 \ 42.
[2]-al-Kashkuul cha Bahaiy-juzuu 2 \ 97-na kauli ya Luqman: Oh mgongo wangu umekatika, na imepokelewa riwaya kama hiyo kutoka kwa Imam Hussein (AS) na aliitoa pale alipouliwa nduguye Abbas (AS) katika tukio la Karbalaa akasema: Hivi sasa uti wa mgongo wangu umevunjika na kukatika na hila zangu kupungua.-Ina maana ile ile-337.
[3]-Bawasiri:Huu ni ugonjwa utokao sehemu ya nyuma na husababishwa na kupanuka mishipa ya matako na husabaisha kuvuja kwa damu.

mlango wa choo.[1]-[2]

Tunasema: Ameyapokea haya Aminil-Islaam Atwabrasiy (aliyefariki mwaka 548 h) lakini yeye alisema: Na imesemekana: kwamba bwana wake aliingia chooni na kukaa sana humo Luqman akamuita: Kukaa sana chooni kunasababisha maumivu na kukatika kwa maini na kuyataabisha. Husababisha kupatwa na bawasiri, na hupandisha joto kichwani, kwa hivyo basi kaa kidogo, na simama kidogo. Akasema: Basi akaiandika hekima yake juu ya choo.[3]

Na amepokea Shaikh Tuusiy (Mungu autukuze utajo wake) kutoka kwa Muhammad bin Ali bin Mahboub kutoka kwa Al-abbas, kutoka kwa Hussein bin Yazid, kutoka kwa Ismaili bin Abi Ziyaad, kutoka kwa Muhammad bin Muslim, kwamba: Nimemsikia Aba Jaafar (AS) akisema: Luqman alisema kumwambia mwanawe: Kukaa sana chooni husababisha bawasiri. Akasema: Akayaandika maneno haya juu ya mlango wa choo.[4]

Na kutokana na sababu hii ndio maana mafuqaha wetu wakatoa fatwa ya kwamba ni makruhu kukaa sana chooni, Shahidul-Awwal na Shahiduth-Thaniy (mwenyezi Mungu atukuze utajo wao) wamesema: Ni makruhu kisheria kukaa sana chooni kwa kuohofia kupatwa na bawasiri. Imepokelewa na Imam Swaadiq (AS) kutoka kwenye hekima ya Luqman udogoni mwake, kwamba yeye

[1]-al-Hash:Bustani, na limetumika kimajazi juu ya sehemu ya kujisaidia na sehemu ya haja kubwa, kwa sababu wao walikuwa wakijisaidia kwenye mabustani.
[2]-Addurul-Manthuur juzuu 5 \161.
[3]-Majmaul-Bayaan juzuu 8 \318 na amepokea kutoka kwake Wasaaili juzuu 1 \ 20 kati ya milango ya hukumu za chooni h 5.
[4]-Chanzo hicho hicho kilichotangulia h 1.

aliiandika maneno hayo juu ya malango wa choo.[1]

Na Sheikh Warram amesema katika kitabu Tanbiihul-Khawaatir hivi: Na Luqman alikuwa akikaa sana peke yake, na bwana wake alikuwa akimpitia na kusema: Ewe Luqman, hakika wewe unakaa sana peke yako, lau kama ungekaa na watu ingekuwa ni anasa kwako? Luqman akasema: Hakika kukaa sana peke yangu hunisaidia kufahamu fikra na kufikiria sana ni dalili ya kuielekea njia ya pepo.[2]

Baada ya kuyajua haya ni kwamba, mmoja kati ya wanafunzi mashuhuri wa Luqmanul-Hakiim ni bwana Inbaadhqliis ambaye alikuwa miongoni mwa wakubwa wa hekima na waheshimiwa na vinara wake. Alikuwa mmoja wa marais watano mashuhuri wa nchi ya Ugiriki. Aliishi katika zama za Mtume Daudi (AS) na akapata elimu kubwa kutoka kwake. Alikuwa akienda kwa Luqman mara kwa mara na kuchukua hekima kutoka kwake na kisha kurudi nchini kwake.[3]

Kutokana na ukubwa huu ambao Luqman aliufikia, Mwenyezi Mungu akamfanya kuwa ni Qur'an isomwayo usiku na mchana ili awe ni kigezo kwa watu wema, na nuru kwa watu wenye macho na busara.

Na nguzo ya mafuqaha na wanazuoni wa elimu ya itikadi, Khalifa Sayyid Murtadha amesema katika kitabu kiitwacho Ulumi Abu Swalaah Taqiiy bin Najmil-Halabiy (Mwenyezi Mungu autakase utajo wake - aliyezaliwa mwaka 374-na kufariki mwaka 447 h) kwamba: Na kwa hakika kuna habari iliyo mashuhuri na inayokubaliwa na wanahistoria

[1]-al-Fawaaidul-Milliyyah Lisharhi Risaalatin-Nafliyyah ukurasa 49.
[2]-Mustadrakul-Wasaail: juzuu 11 \ 186.
[3]-al-Asfaar: juzuu 5 \210.

wote kuhusiana na umri mrefu wa Luqman Hakiim (AS) na kwamba aliishi umri wa Unsur saba (karne). Ila tu kwamba wanatofautiana kuhusu muda wa Unsur. Kuna wanaosema kuwa Unsur ni sawa na miaka elfu moja, na kuna wanaosema ni miaka mia tano. Riwaya iliyopokelewa ikielezea uchache wake ni kwamba umri wa Unsur saba aliyoishi Luqman ni miaka elfu moja na mia tano.[1]

Na imepokelewa kutoka kwa Imaaduddini al-Hassan bin Ali at-Twabarsiy (Mungu autukuze utajo wake - kati ya wanazuoni wa karne ya saba Hijiria) kwamba Luqman aliishi miaka elfu tatu.[2]

Na inasemekana ya kwamba kaburi la Luqman Hakiim liko katika mahala au kitongoji kilichoko karibu na Twabariyyah huko Palestina.[3]

[1]-Taqriibul-Maarif: ukurasa 449.
[2]-Asraarul-Imamah ukurasa 102.
[3]-Nafsur-Rahmaan: 17 chapa ya Hajariyyah.

LULU ILO PANGIKA KATIKA
MAWAIDHA YA LUQMANIL- HAKIIM (AS)

Na hebu tuwe na mwisho mzuri kuhusiana na maisha ya Luqman Hakiim (AS) kwa kutaja mawaidha na hekima zake zilizotajwa kwenye Qur'ani Takatifu au zilizopokelewa kutoka kwa Amiril-Muuminiin (AS) na baadhi ya Maimamu Maasumu (AS), zilizopokelewa katika baadhi ya vyanzo na vitabu vya maulamaa wetu, (radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao wote) na katika baadhi ya vitabu vingine.

Amesema Mwenyezi Mungu katika Kitabu chake Kitukufu katika Surat Luqman:

ٱ ب ب ٻ ٻ پ پ پ پ ڀ ڀ ٺ ٺ ٺ ٺ ٽ ٽ ٿ ٿ ٿ ٿ ٹ ٹ ٹ

ajili ya udogeshaji wa kumdharau لاَ تُشْرِكْ بِاللَّهِ (Usimshirikishe Mwenyezi Mungu). Inasemekana ya kuwa mwanawe alikuwa mshirikina na hakuacha kumpa mawaidha hadi akasilimu إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ (Hakika ushirikina ni dhulma kubwa) na hilo linatokana na kumfanya sawa na kumlinganisha aliye mbora kabisa na yule aliyekuwa dhalili zaidi kati ya viumbe, na kati ya mwenye kuneemesha aliye tajiri na mwenye kujitosheleza bila mipaka (mutlaq) na anayeneemeshwa na aliye fakiri wa kutupa. Alitanguliza kwenye mawaidha yake kemeo na katazo la kumshirikisha Mwenyezi Mungu, kwa sababu kumpwekesha Mwenyezi Mungu (Tawhiid) ndilo chimbuko la mawaidha na asili yake, na pia kwa sababu shirki ni dhulma isiyosamehewa na Mwenyezi Mungu mtukufu bila ya kutubia tofauti na makosa mengine ambayo huenda yakasamehewa na Mwenyezi Mungu bila ya kuhitajia kuyatubia.

ہ ھ

'Ewe mwanangu hakika,' yaani jambo lolote lile kati ya uovu na wema

ہ ھ ھ

'Ikiwa ni wenye uzito' yaani wenye kiwango na uzito wa

ے ے ئے

'Chembe ya Khardali,' na Khardali ni mmea wenye majani majani huota nchi kavu, mashambani pamoja na mazao au pembezoni mwa njia. Chembe hii ni ndogo sana na yenye rangi nyeusi. Hupigiwa mfano kwa udogo wake na kusemwa: Sina kiasi cha kadhaa cha Khardali, yaani sina chochote, na mbegu zake hutumika kwa ajili ya tiba na kwa ajili ya kukitia ladha chakula (kama vile pili pili).

ۓ ڭ ڭ ڭ ۇ ۇ ۆ ۆ

'ikawa ndani ya jabali au mbinguni au ardhini', yaani lau kama mambo haya yangekuwa sehemu ya siri na iliyo fichika sana na iliyowekewa ngome kama vile ndani ya jiwe kubwa ambalo ni miongoni mwa vitu vigumu sana au sehemu iliyo mbali sana na ya juu zaidi kama vile mbinguni au kwenye kina cha ardhi au chini yake

ۈ ۈ ۋۋۇ

'basi Mwenyezi Mungu atayaleta,' yaani atayahudhurisha na kumhesabu mtu juu ya matendo na mambo hayo.

ۇ ۋ ۋ ۇ ۋ

'Hakika Mwenyezi Mungu ni mpole خَبِيرٌ mwenye habari ya mambo yote,' yaani ni mwenye ujuzi na habari za mambo yote kikamilifu yaliyo dhahiri naya siri

ۍ ې ې

'Ewe mwanangu! Simamisha swala' kwa ajili ya kuikamilisha na kuifikisha nafsi yako kwenye ukamilifu.

ې

'Na uamrishe mema na kukataza maovu" na ufanye hivyo kwa ajili ya kuwafikisha wengine kwenye ukamilifu na pia kuifikisha jamii ya viumbe kwenye ukamilifu.

'Na kuwa mvumilivu na mwenye subira juu ya yale yatakayokupata' kati ya mabalaa au mashaka na matatizo na maudhi katika njia ya kuamrisha mema na kukataza mabaya au maovu 'Hakika hilo' yaani subira au akiashiria mambo yote aliyoyaamrisha 'Ni miongoni mwa mambo yenye kuazimiwa,' yaani ni mambo yanayostahili kuyaazimia na utashi wake au irada yake kuwa ni yenye nguvu na yenye kujizatiti isiyodhoofiki mbele ya mafunzo ya Mwenyezi Mungu na sheria yake. Hii ni kwa

sababu kuwa na rai mbali mbali kunapingana na azma juu ya jambo moja.

'Na wala usijitenge na watu', yaani usijiepushe na watu katika mahusiano na kuashiriana pamoja nao na wala usijiepushe na anayekusemesha kwa kumdharau na inasemekana: Usiidhalilishe na kuidharau (nafsi yako) kwa watu kwa ajili ya kuvitilia tamaa walivyonavyo.[1] Na imepokelewa kutoka kwa Imam Swaadiq (AS) katika aya hii isemayo (وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ) kwamba: Watu wote wawe sawa kwako kielimu.[2]

ی ی ی ی

Yaani usitembee kwa majigambo na kutakabari kwa watu na kwa kufurahia uliyonayo

'Hakika Mwenyezi Mungu hampendi kila mwenye kutakabari mwenye kujifakharisha' yaani hampendi mtu mwenye kiburi mwenye kujifakharisha kwa watu wengine. Na imepokelewa kutoka kwa Mtume Mtukufu (SAW) ya kwamba amesema:

مَنْ مَشَى عَلَى الأَرْضِ إِخْتِيَالاً لَعَنَتْهُ الأَرْضُ وَمَنْ تَحْتَهَا وَمَنْ فَوْقَهَا.

(Mwenye kutembea juu ya ardhi kwa maringo basi ardhi humlaani na vilivyomo chini yake na juu yake).[3]

'Na tembea mwendo wa wastani', yaani fanya wastani katika utembeaji kati ya maringo ya dhahiri kwa kufanya wastani katika kutembea na kati ya kuidharau nafsi na

[1]-Tafsiir Ali bin Ibrahiim juzuu 2 \ 265.
[2]-Tafsiirul-Burhaan juzuu 3 \ 276.
[3]-Thawaabul-Aamal cha Swaduuq (Mungu amrehemu) ukurasa 588- Intishaaraatil-Akhlaq –Qumil-Muqaddasah.

kutoiheshimu kidhahiri kwa kutembea haraka haraka, na kwa sababu hiyo ndio maana ikapokelewa kutoka kwa Mtume wetu Mtukufu (SAW) ya kuwa:

سُرْعَةُ الْمَشْيِ تُذْهِبُ بَهَاءَ الْمُؤْمِنِ.

"Kutembea haraka haraka kunaondoa heshima na hadhi ya muumini"[1]

'Na punguza sauti yako', yaani punguza sauti yako na wala usiiinue kwa kiwango unachoweza kuuinua. Makusudio ni kuifanya ya wastani kiasi cha kumwezesha kuisikia aliyekusudiwa bila ya kuzidi hapo.

'Hakika sauti zichukizazo' yaani zenye kutisha na mbaya na yenye kuudhi zaidi

'ni sauti ya punda.' Na huu ni mfano wa sauti ya juu kwa ukubwa wa mlio wake. Hii ni istiara kwa ajili ya kuonyesha ukubwa wa kemeo na kwamba ni kemeo kali sana. Kama ambavyo amefanya sauti kuwa moja kwa makusudio ya jinsi na si kwa ajili ya kuitaja sauti moja. Imepokelewa kutoka kwa Imam Swaadiq (AS) akisema Kwamba: Hiyo (yaani sauti yenye kukera) ni kupiga chafya kwa sauti ya juu na mbaya, na mtu anapopaza sauti anapozungumza upazaji ulio mbaya isipokuwa anapokuwa anamuita mtu au anaposoma Qur'an.[2]

Na vilevile anapokuwa mbele ya adui kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu

[1]-al-Jaamiu Liahkaamil-Qur'an juzuu 14 \ 48- Na Tafsirul-Baidhawiy juzuu 4 \ 215.
[2]-Nuuruth-thaqalaini juzu 4 \ 208- Na Bayaanus-saadah juzu 3 \ 231.

پ پ پ

'Ni Wakakamavu kwa makafiri.'[1] Kama ambavyo inapaswa bali ni sunna kwa muadhini kuwa mwenye sauti kubwa yaani sauti ya juu, ili liweze kufikiwa lengo la adhana nalo ni kutangaza wakati wa kuwadia swala. Kuna riwaya nyingi zinazothibitisha hilo zilizopokelewa kutoka kwa Ahlul-Baitil (AS).[2]

Na inampasa mwanafunzi na mtoto kupunguza sauti zao mbele ya mwalimu na baba yao kwa sababu si si jambo la kupendeza wala jema kupaza sauti zao yao.[3]

Na kwa hakika Luqman (AS) alikuwa akimwambia mwanawe: "Ewe mwanangu! Kwa nini watu hawaogopi yale wanayoahidiwa? Wao wanayatengua kila siku. Ni vipi hajiandai kwa ajili ya lile aliloahidiwa yule aliye na muda unaomalizika? Ewe mwanangu! Chukua katika dunia fungu lenye kukutosheleza na wala usiingie duniani uingiaji utakaoidhuru akhera yako na wala usiitupe mkono na kuikataa na hivyo kuwa ni mwenye kuwategemea na kuwahitajia watu. Fanya ibada ya funga itakayokata na kuondoa matamanio yako, na usifunge funga itakayokuzuia kuswali, kwani swala ni kubwa na yenye daraja kubwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko funga.

Ewe mwanangu! Usijifunze elimu ili kujifakharisha nayo kwa maulamaa na kuwafanyia mijadala watu wasio kuwa na akili timamu au kujionyesha kwa elimu hiyo katika vikao, na wala usiiache elimu kwa kufanya zuhdi na kwa kupendelea ujinga.

---

[1]-Suuratul-fat'hi aya 29.

[2]-Angalia:Jawaahirul-kalaam juzu 9 \ 108-na Hadaaiqun-naadhirah juzu 7 \ 336.

[3]Angalia:Tafsiirul-Maudhui cha ustadh al-Mamuliy (Mwenyezi Mungu amzidishie umri) juzu 7 \ 399.

Ewe mwanangu! Chagua vikao na majaalisi kwa macho yako na kwa kutumia busara. Kwa hivyo basi ukiona watu wakimtaja Mwenyezi Mungu kaa nao, hakika wewe ukiwa ni aalim (mwenye elimu) basi elimu yako itakufaa na kukunufaisha na kukuzidishia elimu, na ukiwa ni mjinga watakuelimisha, na huenda Mwenyezi Mungu mtukufu akawafunika kwa rehma na ikakujumuisha na wewe pia.

Ewe mwanangu! Ikiwa utakuwa na shaka na mauti, basi ondoa usingizi katika nafsi yako na wala hautoweza kufanya hivyo. Na ikiwa utakuwa na shaka na ufufuo, basi ondoa ung'amuaji usoni mwako na hutoweza kufanya hivyo, kwani wewe ikiwa utafikiria na kufanya mazingatio utafahamu ya kuwa nafsi yako iko mikononi mwa mtu mwingine, na kwa hakika usingizi ni sawa na kifo na kwamba kuamka baada ya kulala usingizi ni sawa na ufufuo baada ya kifo.

Ewe mwanangu! Kila mnyama humpenda mwenziwe (aliye mfano wake) na binadamu hampendi mwenziwe (aliye mfano wake), kwa hivyo basi usiueneze wema wako isipokuwa kwa mwenye kuutaka na kuutafuta, na kama ambavyo hakuna urafiki kati ya mbuzi na bweha, vile vile hakuna urafiki kati ya mwema na muovu. Mwenye kuukaribia uovu hufanya baadhi yake, vile vile mwenye kushirikiana na muovu hujifunza baadhi ya njia zake. Mwenye kupenda kujionyesha hushutumiwa, mwenye kuingia sehemu mbaya hutuhumiwana mwenye kuambatana na kufuatana na rafiki mbaya hasalimiki. Na asiyedhibiti ulimi wake hujuta.

Ewe mwanangu! Kuwa sahibu wa watu mia na wala usimfanyie uadui yeyote.

Ewe mwanangu! Mimi tangu nilipodhihiri duniani niliipa

mgongo dunia na kuielekea Akhera. Kwa hivyo basi, nyumba uiendeayo na kuielekea iko karibu sana kuliko nyumba ujitengayo nayo na kuwa mbali nayo.

Ewe mwanangu! yale uyaonyeshayo na kujidhihirisha nayo kwa adui yako yawe ni kujikinga na kujiepusha na mambo ya haramu, na fadhila katika dini yako, kulinda na kuhifadhi heshima yako na kuikirimu nafsi yako kwa kutoichafua kwa kumuasi Mwenyezi Mungu mwenye rehma. Jiepusha na tabia chafu na matendo mabaya na ifiche siri yako na zifanye siri zako ziwe njema na nzuri. Hakika ikiwa utafanya hivyo basi utasalimika kwa sitara ya Mwenyezi Mungu na adui wako asipate aibu yoyote au kosa lolote kutoka kwako. Usijiaminishe na vitimbi vyake asije akapata faida kutoka kwako katika baadhi ya hali zako, kwani ikiwa ataweza kupata jambo lolote kwako atakurukia na kutoacha mtelezo wowote utokeao kwako. Na yadharau mambo mengi na kuyaona madogo katika kutafuta manufaa na yaliyo madogo yaone kuwa ni makubwa katika kuingia na kujitumbukiza kwenye madhara.

Ewe mwanangu! Usikae na watu kwa njia tofauti na wanavyokaa wao, na wala usiwabebeshe mambo zaidi ya uwezo wao. Kwani kwa kufanya hivyo rafiki yako ataendelea kukuchukia nawe na yule aliyebebeshwa vitu vilivyo juu ya uwezo wake atakuwa ni mwenye kujitenga na wewe na kukuepuka. Likithibiti hilo, utakuwa ni mtu usiye na rafiki anayekuliwaza wala ndugu akutiaye nguvu, na ikiwa utabaki peke yako utakuwa ni mwenye kuachwa na kutelekezwa na hapo utakuwa dhalili. Na wala usiombe udhuru mtu asiyetaka kukukubalia udhuru na wala asiyekuona kuwa una haki. Usishirikiane katika mambo yako isipokuwa na yule apendaye kupata malipo katika kukidhi haja zako.

Akiwa hivyo basi atataka kukidhi haja zako kama vile atafutavyo mahitaji kwa ajili yake (ya nafsi yake), kwa sababu yeye baada ya kukufanya wewe ufaulu, hiyo itakuwa ni faida na mafanikio katika dunia yenye kutoweka na atakuwa amepata hadhi na akiba yake katika nyumba yenye kubakia milele na hapo kufanya juhudi kukukidhia haja zako. Na wawe ndugu zako na marafiki zako ambao unawaamini na kuwa na nia nzuri kuhusiana nao na unaosaidiana nao juu ya mambo yako, wawe ni wenye heshima na hadhi na wenye kujiepusha na madhambi. Wawe ni matajiri, wenye akili na wacha-Mungu ambao ukiwanufaisha na kuwafaidisha watakushukuru, na ukighibu na kutokuwa karibu nao watakukumbuka.

Na Luqman akasema kumwambia mwanawe: Ikiwa utajifunza adabu ukiwa mdogo basi utafaidika nayo ukubwani, na mwenye kuitilia maanani adabu na (maadili) huitilia umuhimu, na mwenye kuitilia umuhimu hujikalifisha kujifunza adabu hiyo[1], na mwenye kujikalifisha kujifunza huhamasika na kufanya juhudi kuitafuta, na mwenye kuhamasika kwa kuitafuta atapata manufaa kwa elimu hiyo na kuifanya kuwa ni kawaida na desturi yake. Na jihadhari na uvivu wa kuitafuta elimu na kujishughulisha na kukitafuta kitu kingine.

Ikiwa utapitwa na utafutaji wa elimu hakika wewe hutapata kitu kikubwa sana ulichokipoteza kuliko kuiacha elimu.

Ewe mwanangu! Warekebishe jaama na ndugu kati ya watu wenye elimu (wanazuoni) ikiwa watakutii, kukusikiliza na kutekeleza amri zako. Na jihadhari nao pindi hali itakapowafanya wajitenge nawe. Hakika uadui wao ni

[1]-Yaani mwenye kufanya juhudi ya kujifunza elimu hiyo.

mkubwa, mbaya na wenye madhara makubwa kuliko uadui wa watu wa mbali ikiwa watu watawasadikisha kutokana na kufahamu kwao vyema habari zako.[1]

Kuwa mwenye akili aliye bubu, na wala usiwe mjinga mwenye ufasaha. Na fahamu ya kuwa kila kitu kina alama, na alama ya akili ni kufikiri sana, na kunyamaza kwingi (kutozungumza sana).[2]

Ewe mwanangu! Pindi ukisafiri pamoja na watu fulani, basi watake sana ushauri katika jambo lako na mambo yao. Na kuwa mwingi wa kutabasamu usoni mwao, na kuwa mkarimu kwa akiba yako ya safari kati yao, na ikiwa watakuita na kukukaribisha waitikie mwaliko na mwito wao. Na ikiwa watakutaka msaada basi wasaidie, na washinde kwa mambo matatu: Ukimya mwingi, kusali sana, na kuwa mpole na mkarimu wa nafsi kwa mnyama uliye naye, mali au akiba ya safari.

Na ikiwa watakutaka ushahidi juu ya haki, basi watolee ushahidi, na jitahidi kuwapatia maoni yako pindi wanapokutaka ushauri. Kisha usiazimie na kufanya maamuzi mpaka uthibitishe na kufanya uchunguzi, na wala usijibu mashauri yoyote uliyotakiwa kuyatolea ushauri mpaka uyafanyie utafiti. Usimame na kukaa, kulala na kuamka na kusali kwa kuyafikiria, na huku ukitumia fikra na hekima yako katika kuwapa ushauri. Hakika asiyefanya utafiti kwa ajili ya mtu aliyemtaka ushauri basi Mwenyezi Mungu atampokonya maoni yake na kumvua amana aliyopewa.

Na ikiwa utawaona rafiki zako (maswahibu wako) wakitembea basi tembea pamoja nao, na ukiwaona

[1]-Qiswasul-Anbiyaa cha Raawandii:ukurasa 190-194.
[2]- Bahrul-Maarif juzu 1 \ 620.

wakifanya kazi basi fanya kazi pamoja nao, na ikiwa watatoa sadaka na kukopesha basi na wewe toa sadaka pamoja nao na msikilize aliyekuzidi kiumri au mkubwa kukuliko. Na wakikuamuru kufanya jambo fulani na kukuomba, basi jitolee kwa ajili yao na sema, ndio, na wala usiseme hapana. Hakika 'hapana' ni ujinga na udhalili.

Na ikiwa mtatatizika na kutahayari katika njia yenu basi teremkeni (wekeni kituo), na ikiwa mtaingiwa na shaka katika makusudio basi simameni na kutofanya chochote, na shaurianeni. Na mkimuona mtu mmoja, basi msimuulize kuhusianan na njia yenu, na wala msimtake ukuelekezeni njia au muendako. Hakika mtu mmoja akiwa jangwani au porini ni mwenye kutatiza, huenda akawa ni mpelelezi wa wezi na majambazi, au akawa ndiye shetani aliyekutatizeni. Jihadharini na watu wawili pia ila kama mtaona nisiyoyaona mimi. Hakika mtu mwenye akili (busara) pindi anapoona kwa macho yake kitu fulani huifahamu haki kutokana na kitu hicho, na mwenye kushuhudia au shahidi huona asiyoyaona asiye kuwepo (aliye ghaibu).

Ewe mwanangu! Ufikapo wakati wa swala, basi usiicheleweshe kwa ajili ya jambo lolote. Basi iswali na ujipumzishe nayo. Kwa hakika swala hiyo ni deni, na swali ukiwa katika jamaa japokuwa ukiwa juu ya ncha ya mkukuki au mshale. Na jihadhari kulala juu ya mnyama wako, hakika kufanya hivyo huharakisha kujeruhiwa mgongoni mwake au kuangamia kwake, na hilo si katika matendo ya watu wenye hekima, isipokuwa ukiwa kwenye kipando ambacho unaweza kujinyoosha kwa ajili ya kuituliza misuli na maungio ya viungo.

Na unapokaribia kufika nyumbani, basi teremka kutoka juu ya mnyama wako, hakika mnyama huyo hukusaidia, na

anza kumlisha chakula chake kabla yako mwenyewe kwa hakika mnyama huyo ni sawa na wewe mwenyewe (nafsi yako). Na mnapotaka kuweka kituo mahala fulani, basi ni juu yenu kuchagua sehemu ya ardhi yenye rangi nzuri, na yenye udongo laini, na yenye majani mengi.

Na unapofika na kuweka kituo anza kwa kuswali rakaa mbili kabla hujakaa na kupumzika. Na ukitaka kukidhi haja zako, basi nenda sehemu ya mbali tafuta sehemu ya ardhi iliyo mbali, na unapo ondoka na kuanza safari basi swali rakaa mbili, kisha iage ile ardhi ambayo uliweka kituo hapo na kupumzika. Na toa swalamu kwa ajili ya ardhi hiyo na watu wake, hakika kila kipande cha ardhi kina kundi la malaika (kina matarajio ya kufikiwa na malaika), na ikiwa utaweza kutokula chaku mpaka uanze kwa kutoa sadaka katika chakula hicho basi fanya hivyo.

Na ni juu yako kusoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu mtukufu maadamu utakuwa umepanda juu ya mnyama wako. Ni juu yako kumsabihi Mwenyezi Mungu wakati unapofanya kitendo au amali fulani na kusoma dua pamoja na kuomba maadamu huna chochote ukifanyacho (hauna kazi). Jihadhari na kutembea au kuanza safari mwanzoni mwa usiku, na ni juu yako kupumzika na kutembea usiku au kufanya safari usiku, kuanzia nusu ya usiku hadi mwisho wake. Jihadhari na kunyanyua sauti unapokuwa safarini au unapotembea.

Ewe mwanangu! Safiri ukiwa na upanga, (silaha), viatu (khofu), kilemba, hema, kinywaji, sindano, nyuzi na kitoboleo chako na jiwekee akiba ya dawa. Utanufaika nayo na kukusaidia wewe na walio pamoja nawe, na kuwa mwenye kuwafikiana na rafiki zako na mwenye kufuatana

nao, isipokuwa katika maasi ya Mwenyezi Mungu.[1]

Ewe mwanangu! Fahamu ya kuwa wewe utaulizwa kesho utakaposimama mbele ya Mwenyezi Mungu kuhusu mambo manne: Ujana wako umeumaliza kwa kufanya nini, umri wako umaumaliza na kuutumia vipi, na mali yako umeichuma kutokana na nini na umeitumia vipi. Basi jiandae kwa ajili ya kujibu maswali hayo, na wala usiyasikitikie mambo ya kidunia yaliyokupita, hakika kitu kidogo cha dunia hakidumu na kubakia milele, kingi nacho hakiepukiki na kusalimika na mabalaa yake au mitihani na majaribio yake. Basi tahadhari na fanya juhudi katika jambo lako, na ondoa pazia usoni na machoni mwako, na yatekeleze na kukumbuka mema ya mola wako. Fanya juhudi katika kutubia, na jifiche katika muda wako wa faragha kabla ya kukusudia kufanya ulikusudialo kulifanya, hukumu yako kutolewa, na kuwekwa kizuizi kati yako na yale uyakusudiayo kuyafanya.

Ewe mwanangu! Fahamu ya kuwa mimi nimewahudumia manabii mia nne na nikachukua katika maneno yao maneno manne kama yafuatayo: Pindi utakapo kuwa katika swala uhifadhi moyo wako, ukiwa kwenye meza ya chakula hifadhi koromeo lako, utakapokuwa katika nyumba ya mtu mwingine hifadhi jicho lako na pindi ukiwa kati ya viumbe (watu) basi hifadhi ulimi wako.[2]

Ewe mwanangu! yaweke makosa yako mbele ya macho yako hadi utakapokufa, ama mema yako jighafilishe nayo kwa hakika ameyahesabu asiye yasahau.[3]

---

[1]-al-Mahaasin-juzuu 2 –Kitaabus-Safar- mlango wa 22 ukurasa 107- na mlango wa 36 ukurasa 126.
[2]-Ithnaa Ashariyyah fil-Mawaaidhil-Adadiyyah ukurasa 177.
[3]-al-Kashkuul cha Bahai (Mungu amrehemu) juzuu 2 \ 262.

Ewe mwanangu! kila kitu kina alama ikitambulishacho na kukishuhudia, na kwa hakika dini ina alama tatu: Elimu, imani na matendo. Na imani ina alama tatu: Imani ya Mwenyezi Mungu (kumuamini Mwenyezi Mungu), vitabu vyake na mitume wake. Mwanazuoni ana alama tatu: Kumjua Mwenyezi Mungu, kuyajua ayapendayo na kuyachukia. Na mfanya amali ana alama tatu: Swala, funga (saumu) na zaka.

Na mwenye kujikalifisha ana alama tatu: Huzozana na aliye juu yake, husema asiyoyajua na hujipatia na kuvitamani asivyoweza kuvipata.

Na Dhalimu ana alama tatu: Humdhulumu aliye juu yake kwa kumuasi na kutotii amri zake na aliye chini yake kwa kumghilibu na kuwasaidia madhalimu.

Na mnafiki ana alama tatu: Ulimi wake hupingana na moyo wake, moyo wake hupingana na matendo yake, na dhahiri yake hupingana na siri zake au ndani na batini yake.

Na mfanyamadhambi ana alama tatu: Hufanya khiyana, na kusema uongo, na huenda kinyume na ayasemayo.

Na mwenye kujionyesha ana alama tatu: Huwa mnyonge na mvivu anapokuwa peke yake, na kuwa mchangamfu na mtanashati watu wanapokuwa kwake (au anapokuwa na watu), na hujisifu katika kila jambo, (hulisifu kila jambo).

Na Hasidi ana alama tatu: Anapoghibu husengenya, na huwa laini na mpole anapokuwa hadhihiri (anaposhuhudia), na hufurahia kutokea msiba.

Na mfanya-israfu ana alama tatu: Hununua visivyokuwa vyake, na huvaa visivyo vyake, na hula visivyo vyake.

Na mvivu ana alama tatu: huzembea na kudhoofu hadi kupita kiasi (kupindukia), na hupitukia hadi kupoteza haki,

na hupoteza haki hadi kupata dhambi.

Na mwenye mghafala ana alama tatu: Usahaulivu, kupendelea upuuzi, na mwingi wa kughafilika na kusahau.[1]

Ewe mwanangu! Jihadhari na kukerekwa na tabia mbaya na kuwa mchache wa subira, mwenye vitu hivi kamwe hanyooki katika mwenendo wake, na ifanye nzuri tabia yako kwa watu wote.

Ewe mwanangu! Ikiwa hutakuwa na kitu cha kuunga udugu na watu wako wa karibu na jamaa zako na cha kutoa na kuwapatia ndugu zako, basi usikose kuwa na tabia njema na kuwa na bishira kwao[2]. Kwa hakika mwenye kuifanya njema tabia yake hupendwa na watu wema na watu waovu kujiepusha naye, na kinaika na kutosheka na kile akupacho Mwenyezi Mungu, maisha yako yatakuwa mema na safi, na ikiwa utataka kukusanya utukufu wa dunia, basi vikatie tamaa vitu vya watu. Kwa hakika manabii mitume na swiddiquun walifika walipofikia kwa kukata tamaa zao.

Ewe mwanangu! Hakika dunia ni ndogo na umri wako ni mfupi.

Ewe mwanangu! Jihadhari na husuda, isiwe ni katika tabia zako na mambo usifikayo nayo, na jiepushe na tabia mbaya, jihadhari isiwe ni katika tabia yako na maumbile yako. Kwa hakika wewe hutadhuru kwa mambo hayo isipokuwa nafsi yako, na ikiwa wewe ndiwe mwenye kuidhuru nafsi yako basi utakuwa umemtosheleza adui yako jambo lako, kwa sababu uadui wako kwa nafsi yako ni

---

[1]-al-Khiswaal: juzuu 1 \ mlango wa 3 \ 121-122.

[2]-Mutanabbi amesema katika shairi lake:Ikiwa hutakuwa na farasi (mnyama) wala mali ya kuitoa kama zawadi basi yafanye mema maneno yako (zungumza vizuri) ikiwa hali yako haikuwa njema. Wafayaatul-Aayan cha Ibnu Khalaqaan juzuu 4 \ 22 Daaruth-Thaqafah-Beirut.

wenye madhara zaidi juu yako kuliko uadui wa mtu mwingine asiyekuwa wewe.

Ewe mwanangu! Bwana na seyyid wa tabia, maadili na hekima ni dini ya Mwenyezi Mungu mtukufu, na mfano wa dini ni sawa na mfano wa mti uliothabiti na imara. Imani ya Mwenyezi Mungu ndiyo maji yake, swala ndiyo mizizi yake, zaka ndio mti wake, kufanya udugu kwa jili ya Mwenyezi Mungu ndio matawi yake, tabia njema ndiyo majani yake, kutoka kwenye maasi ya Mwenyezi Mungu ndiyo matunda yake na mti haukamiliki isipokuwa kwa kuota matunda mazuri. Vile vile dini haikamiliki isipokuwa kwa kujitenga na kujiondoa kwenye mambo yaliyoharamishwa.[1]

Ewe mwanangu! Tumbo linapojazwa chakula basi fikra hulala, hekima kuwa bubu na viungo kulegea katika kutekeleza ibada.[2]-[3]

Ewe mwanangu! Hakika mwizi anapoiba Mwenyezi Mungu humzuilia riziki yake, humuandikia dhambi ya kuiba kwake na kumlipa juu ya wizi wake, na lau kama angevumilia na kusubiri angeipata riziki hiyo na ingemjia kupitia njia yake iliyo safi.[4]

[1]-Qiswasul-Anbiyaa cha Rawandiy ukurasa 195-196.

[2]-Na kwa sababu hii ndio maana baadhi ya watu wenye hekima wakasema: Hakika hekima ni sawa na bibi harusi ambaye hutaka nyumba iliyo wazi isiyo na kitu.

[3]-Jaamiul-Akhbaar mlango wa 141 ukurasa 215 chapa ya Hajariyyah.

[4]-Ibnu Abil-Hadid amepokea ya kuwa Imam Ali (AS) aliingia msikitini, na akamwambia mtu mmoja: Nishikie mnyama wangu huyu (Nyumbu), akatoa lijam yake na kwenda nayo, Ali (AS) baada ya kumaliza swala yake akatoka, akiwa na dirhamu mbili mkononi mwake ili ampatie mtu yule kama malipo ya kazi yake. Mara akamkuta mnyama wake akiwa amevuliwa kamba yake (hana lijam), basi zile dirhamu mbili akampatia mmoja kati ya vijana na watumishi

Ewe mwanangu! Kuwa na ikhlasi na nia safi katika kumtii Mwenyezi Mungu hadi isichanganyike na chembe yoyote ya maasi kisha upambe utiifu wako kwa kuwafuata watu wa haki. Hakika utiifu wao umeungana na kufungamana na Mwenyezi Mungu.

Na Luqman akasema! Nimebeba jiwe kubwa na chuma na vyote ni vizito, lakini sikuwahi kubeba kitu kizito zaidi kuliko jirani mbaya. Nemeonja machungu yote, lakini sijawahi kuonja kitu kichungu zaidi kuliko ufukara.

Ewe mwanangu! Usimfanye mjinga mjumbe, ikiwa hukumpata mwenye akili na mwenye hekima ili awe mjumbe wako, basi kuwa mjume wa nafsi yako wewe mwenyewe.

Ewe mwanangu! Ni vyema aliyepungukiwa na yakini yake na aliyedhoofu katika juhudi na taabu zake za kutafuta riziki afanye mazingatio na kutambua ya kwamba, Mwenyezi Mungu mtukufu amemuumba katika hali tatu katika, na akampatia riziki yake hali ya kuwa yeye hakuwa ni mwenye kuitafuta riziki hiyo katika hali yoyote kati ya hali hizo na wala hakuwa na hila yoyote, na kwamba Mwenyezi Mungu atamruzuku katika hali ya nne pia. Ama hali ya kwanza kati ya hali hizo ni pale, alipokuwa tumboni mwa mama yake akimruzuku huko katika mahala palipo tulia, kiasi kwamba hakuna baridi wala joto vilivyokuwa vikimuudhi, kisha akamtoa kwenye hali hiyo, na

wake, ili anunue lijam au kamba nyingine. Mara yule kijana akaiona ile kamba na lijam iliyoibiwa ikiwa sokono, ikiwa imeuzwa na bwana yule kwa dirhamu mbili, nae akaichukua kwa dirhamu mbili na kurudi kwa bwana wake. Imam Ali (AS) akasema: Hakika mja hujinyima na kujiharamishia yeye mwenyewe riziki ya halali kwa kutokuwa na subira, na wala haizidi riziki ile aliyokadiriwa kuipata – Sharhu Nahjul-Balagha juzuu 3 \ 160.

akamtiririshia kupitia kwenye maziwa ya mama yake chakula akimlea bila yeye kuwa na uwezo wala nguvu yoyote. Kisha akaachishwa kunyonya maziwa akampatia riziki yake kupitia uchumaji wa wazazi wake kwa upole na rehma yake nyoyoni mwao hadi alipokuwa mkubwa na kuwa na akili timamu na kujichumia riziki yake mwenyewe. Hapo ndipo alipoanza kuhisi kuwa kwenye dhiki, na akawa na dhanna mbali mbali mbaya kwa mola wake. Alianza kupuuza haki zilizoko kwenye mali yake na kujinyima yeye mwenyewe pamoja na familia yake kwa kuogopa ufukara.[1]

Ewe mwanangu! Chukua mawaidha kutoka kwa watu kabla ya watu hawajapata mawaidha kutoka kwako.

Ewe mwanangu! Chukua mawaidha (jifunze) kutokana na kitu kidogo kabla hujafikwa na jambo kubwa .

Ewe mwanangu! Jihadhari na kuchukua deni kisha ukafanya khiyana katika deni hilo.

Ewe mwanangu! Ifanye dunia kuwa ni jela yako ili uifanye akhera kuwa pepo yako.

Ewe mwanangu! Kuwa jirani wa watu masikini na jihusishe na mafukara na masikini kati ya Waislamu.

Ewe mwanangu! Kuwa kwa yatima kama baba mpole na kwa mjane (aliyefiwa na mumewe) kama mume mwenye huruma.

Ewe mwanangu! Kwa hakika si kila asemaye: Nisamehe husamehewa, hakika Mwenyezi Mungu hamsamehi mja isipokuwa yule aliyemtii Mola wake (aliyetekeleza twaa).

Ewe mwanangu! Lau kama majumba yangekuwa juu ya toroli (mkokoteni) basi mtu kamwe asingekaa na jirani mbaya.

[1]-Qiswasul-Anbiyaa cha Rawandiyh (Mungu autukuze utajo wake - aliyefariki dunia mwaka 573 Hijiria) ukurasa 196-197.

Ewe mwanangu! Ni nani ambaye alimuabudu Mwenyezi Mungu naye akamtelekeza na kumuacha? Na ni nani huyo ambaye alimtaka Mwenyezi Mungu na kutompata?

Ewe mwanangu! Ni nani huyo ambaye alimtaja na kumkumbuka Mwenyezi Mungu naye asimkumbuke? Na ni nani ambaye alimtegemea Mwenyezi Mungu naye kumtelekeza kwa mwingine? Na ni nani ambaye alimnyenyekea Mwenyezi Mungu aliye takasika naye asimrehemu?

Ewe mwanangu! Mtake ushauri mtu mkubwa na wala usione aibu na haya kumtaka ushauri mdogo.

Ewe mwanangu! Jihadhari kufuatana na mafuska (watu waovu), wao ni kama majibwa wakikuta kitu kwako hukila, la sivyo hukutukana na kukufedhehesha, na kwa hakika mapenzi yao kati yao ni ya saa moja.

Ewe mwanangu! Kuwafanyia uadui waumini ni bora zaidi kuliko kufanya urafiki na mafasiki (watu waovu).

Ewe mwanangu! Muumini unamdhulumu na wala hakudhulumu wewe na humuomba radhi na kukuridhia au kukusamehe, na fasiki hamuogopi, hachungi wala kumchelea Mwenyezi Mungu, vipi atakuogopa wewe na kulinda haki zako?

Ewe mwanangu! Anza kuwatolea watu salamu na kupeana mkono nao kabla ya kuzungumza nao.

Ewe mwanangu! Usizozane katika elimu ya Mwenyezi Mungu, kwa hakika elimu ya Mwenyezi Mungu haifikiwi wala kuhesabiwa.[1]

[1]-Huenda makusudio ya elimu ambayo ni sifa ya dhati si sifa ya kitendo na dhati yake hiwezekani kwa mtu yeyote kuifahamu kikomo chake, kiasi kwamba hakuna mnasaba wowote kati yake na kati ya kitu kingine kati ya walimwengu kwani dhati ya uhakika wake haidirikiwi na kufahamika hata kidogo. Wala haiwezekani kufahamu

Ewe mwanangu! Usifichue siri zako kwa mkeo na usiufanye mlango wa nyumba yako kuwa ndio makao yako (mahala pako pa kukaa).

Ewe mwanangu! Wanawake ni wa aina nne: Wawili ni wema na wawili wengine ni wenye kulaaniwa. Ama mmoja wa wale walio wema ni mtukufu katika kaumu na jamaa zake na aliye dhalili katika nafsi yake, ambaye akipewa hushukuru na akifikwa na mitihani huvumilia na kusubiri. Kichache kilichoko mikononi mwake ni kingi na ni mwema nyumbani kwake. Na wa pili ni yule mwenye mapenzi na mwenye kuzaa. Huwa ni kheri na mwema kwa mumewe, yeye ni kama mama mpole huwahurumia wakubwa na kuwahurumia wadogo. Huwapenda watoto wa mumewe hata kama ni wa mama mwingine, ni mtulivu na asiye na papara na mwenye kurekebisha mambo yaliyo tawanyika. Ni mwenye kumridhia mume wake, mwenye kuirekebisha nafsi na ahli na mwenye matumizi mazuri ya mali na watoto. Kwa hivyo yeye ni kama dhahabu nyekundu, wema ulioje wa yule aliye ruzukiwa mke kama huyo! Akimuona mumewe na kuwa naye karibu humsaidia na akiwa hayupo na kuwa mbali naye humlinda na kumhifadhi. Ama mmoja kati ya wawili waliolaaniwa ni mtukufu nafsini mwake dhalili kwa kaumu na watu wake, ambaye akipewa huchukia na akinyimwa hukemea na kuchukia. Mumewe huwa kwenye mtihani na balaa

kikomo chake, na kwa sababu hii baadhi ya maurafaa wanasema:Ama dhati ya Mwenyezi Mungu manabii na mawalii wote walishindwa na kutatizwa kuifahamu na kufikia kikomo chake. Kama alivyosema Mtume (SAW): Hatukukufahamu ukweli na ukomo wa maarifa yako (hatukukufahamu kama unavyostahili kufahamika), na hatukukuabudu kama unavyostahili kuabudiwa. Sharhu Fusuusul-Hikam cha Qaiswariy juzu 1 \ 172.

kutokana na mwanamke huyo na jirani yake huwa kwenye taabu. Yeye huwa ni kama samba ambaye ukikaa kando yake atakula na ukimkimbia atakuua. Wa pili aliyelaaniwa ni yule anayekuwa kwa mumewe lakini utashi na mapenzi yake huwa kwa jirani yake. Yeye ni mwepesi wa kukasirika na kuchukia, ni mwepesi wa kulia. Anapokuwa na mumewe na kumuona au kuwa karibu naye hamnufaishi wala kumsaidia, na akighibu na kutokuwepo au kuwa mbali naye humfedhehesha. Yeye ni sawa na ardhi yenye unyevunyevu (umajimaji) ikimwagiliwa maji basi hutoa maji na kufurika na kuzama kwenye maji, na ikiachwa hushikwa na kiu na kuhitajia maji. Akiruzukiwa mtoto mwanamke huyo hanufaiki naye.

Ewe mwanangu! Usiwatukane watu wasije wakawa wale uliowatukana ni wazazi wako.

Ewe mwnangu! Kubali usia wa baba mwenye kukuhurumia na mpole kwako.[1]

Na Luqman akasema kumwambia mwanawe: Kuwa mnyenyekevu kwa ajili ya haki utakuwa ni mtu mwenye akili sana kati ya watu, na hakika mtu mwenye busara na akili huiendea na kuifuata haki.[2]

[1]-al-Ikhtiswaas ukurasa 336-340.

[2]-Amesema Swadrul-Muta Allihiin (Mwenyezi Mungu autukuze utajo wake): Kuwa mnyenyekevu kwenye haki au kuinyenyekea haki ni kwamba mja asiione nafsi yake kuwa ipo na ina nguvu na uwezo isipokuwa kuwepo na nguvu zote ni za mwenye haki (Mwenyezi Mungu. Na mwmanadamu kila anavyokuwa mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu na kujidogesha katika nafsi yake na kujiona si chochote basi Mwenyezi Mungu humzidishia utukufu na ubora na sharafu. Kisha akasema: Na kauli yake isemayo:Na hakika mwenye akili na busara kwenye haki busara na akili yake ni ndogo. Yaani kwamba akili ya mtu na busara yake nayo ni akili yake na ufahamu wake ni mdogo sana kwenye haki (Mbele ya Mwenyezi Mungu)

Ewe mwanangu! Hakika dunia ni bahari yenye kina kirefu, kwa hakika wamezama humo walimwengu wengi basi jahazi lako liwe ni taqwa (ucha Mungu), na mizigo yake iwe ni imani[1], na matanga[2] yake yawe ni kutawakali kwake na kumtegemea Yeye, na muongozaji wake iwe ni akili, na dalili yake ni elimu, na wakazi wake ni subira na uvumilivu.[3]

Ewe mwanangu! Usiutegemeze moyo wako kwenye maridhio ya watu na sifa zao na makemeo yao, hakika hilo halitaweza kupatikana, hata kama mtu atafanya juhudi kubwa kwa ajili ya kulifikia jambo hilo kwa uwezo wake wote.

Na mwanawe akamwambia maneno yenye maana haya yafuatayo: Ninapenda kuona mfano wa hilo au kitendo au kauli.

Akamwambia: Ninatoka mimi na wewe.

---

hauna kiwango chochote na mwenye nafasi na hadhi mbele ya Mwenyezi Mungu ni unyenyekevu na utulivu na khudhui na kutokuwa na uwezo na kuhitajia kwake. Kwa sababu hii ikasemwa: Mwisho na lengo la wenye kuabudu ni kusahihisha upande wa kuwezekana na kuhitajia kwake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa hivyo basi kila mwenye elimu na mwenye akili na ufahamu anayedai ya kuwa yupo (mwenye kujiona kuwa ana hadhi fulani) na ana ukamilifu wa aina yoyote tofauti na kuwa kuwepo kwake ni tone kati ya matone ya bahari ya kuwepo kwake Mwenyezi Mungu na tafadhuli zake, basi yeye atakuwa kwenye kizuizi na kizibo kikubwa na hijabu kubwa ya kutofahamu ukweli ulivyo. (Sharhu Usuululkafiy ukurasa 55 chapa ya Hajariyyah.

1Yaani uvipakizavyo kwenye jahazi hilo.

2- Hiki ni kipande cha kitambaa kikubwa na kipana kiwekwacho juu ya mti kipulizwacho na upepo na kulitia kasi jahazi katika mwendo wake (Tanga).

3-Usuulu Minal-Kafiy juzuu 2 \16- Kitabul-Akli wal-Jahli h 12.

Wakatoka wote wawili wakiwa na mnyama[1], na Luqman akampanda mnyama yule na akamuacha mwnawe akitembea nyuma yake, wakapita kando ya watu fulani, wakasema: Huyu ni shekh mwenye moyo mgumu, mwenye huruma ndogo, yeye anapanda mnyama, naye ni mwenye nguvu sana kuliko mtoto huyu, na anamuacha mtoto huyu mdogo akitembea nyuma yake, hakika huyu ni upangiliaji mbaya na utovu wa busara).

Akasema kumwambia mwanawe:Umesikia maneno yao na upingaji wao kupanda kwangu na kutembea kwako? Akasema: ndio, akasema: Panda wewe ewe mwanangu ili mimi nitembee kwa miguu. Luqman akatembea kwa miguu na mtoto kupanda, mara wakapita kwa watu wengine, wakasema: Huyu ni mtoto mbaya sana na huyu ni mzazi mbaya sana. Ama baba yake, kwa hakiki yeye hakumuadabisha mtoto huyu hadi akapanda mnyama, na kumuacha baba yake akitembea kwa miguu nyuma yake, na baba au mzazi ndiye mwenye kustahili kuheshimiwa na kupanda mnyama. Ama mtoto kwa hakika yeye amemkosea adabu baba yake kwa kitendo hiki na kwa hali hii tuionayo, basi wote wawili wamefanya vitendo vibaya.

Luqman akasema kumwambia mwanawe: Je, umesikia? Akasema: Ndio. Luqman akasema: Basi sote wawili tupande mnyama. Wote wawili wakampanda mnyama yule, na wakapita kwa watu fulani. Wale watu wakasema: Watu hawa wawili waliopanda mnyama hawana chembe ya huruma katika nyoyo zao, na hawana kheri yoyote kwa Mwenyezi Mungu. Hivi kweli wanathubutu wote wawili kumpanda mnyama huyu, wakiukata na kuuvunja mgongo

---

[1]-al-Bahiim: ni myama ambaye yuko kama vile punda au mfano wa huyo.

wake, na wanambebesha vitu vilivyo juu ya uwezo wake! Lau kama angepanda mmoja na mwingine kutembea kwa miguu ingekuwa ni bora na kufaa zaidi.

Luqman akasema, je, umesikia? Yule mtoto Akasema: Ndio. Hebu tumuache mnyama atembee peke yake bila sisi kumpanda. Basi wakamtanguliza mnyama mbele yao na wao wakitembea, mara wakavuka na kupita kwa watu fulani, wakasema: Hiki ni kitendo cha ajabu kifanywacho na watu hawa wawili, wanamuacha mnyama akitembea bila kubeba chochote na bila kupandwa na yeyote, na wao wakitembea kwa miguu?! Wakawakemea juu ya kitendo hicho kama walivyowakemea juu ya kila kilichofanyika.

Luqman akasema kumwambia mwanawe: Je, unadhani kuna hila yoyote ya mwenye hila ya kuweza kupata ridhaa yao wote? Basi usiwasikilize na kuyatilia maanani matakwa yao, wewe jishughulishe na radhi ya Mwenyezi Mungu tu. Katika ridha ya Mwenyezi Mungu hushughulika mwenye kushughulika, na jishughulishe na saada na mwenye kuielekea dunia na jishughulishe kwa ajili ya siku ya hesabu na siku utakayoulizwa.[1]

Ewe mwanangu! Kaa na wanazuoni, na wasonge songe kwa magoti yako, hakika Mwenyezi Mungu Aliyetakasika anahuisha nyoyo kwa nuru ya hekima kama ambavyo aihuishavyo ardhi kwa mvua za mbunguni.[2]

Ewe mwanangu! Usimdharau mtu yeyote kwa sababu ya kuchakaa kwa nguo zake hakika Mola wako na Mola wake ni mmoja.[3]

[1]-Fat'hul-Abwaab ukurasa 307-308-kutoka kwake Buhari juzuu 13 \ 433 h 27, juzuu 71 \ 461 h 4.
[2]-Raudhatul-Waaidhiin cha Fitaali an-Naisaburiy ukurasa 11.
[3]-Chanzo hicho hicho ukurasa 455-Mishkaatil-Anwaar cha Tuusiy ukurasa 229.

Ewe mwanangu! Ikiwa unadai ya kuwa maneno yanatokana na fedha hakika kunyamaza kunatokana na dhahabu.[1]

Ewe mwanangu! Hakika watu kabla yako walikusanya kwa ajili ya watoto wao na havikubaki walivyovikusanya wala hawakubaki waliowakusanyia. Kwa hakika wewe ni mja uliyeajiriwa, umeamrishwa kufanya kazi na ukaahidiwa malipo kwa amali ma kazi hiyo. Basi tekeleza kazi yako na uchukue malipo yako, na usiwe katika dunia hii kama mbuzi aliyeingia kwenye mazao au shamba lenye majani akala hadi kunenepa na kifo chake kikawa katika unene au kunenepa kwake. Ifanye dunia sawa na daraja liloko juu ya mto ulivuka juu ya mto huo kupitia daraja hilo kisha ukaiacha na hukurudi tene kwenye dunia hiyo hadi mwisho wa maisha (hadi milele). Basi liharibu wala usilijenge na kuliimarisha, hakika wewe hukuamrishwa kulijenga na kuliimarisha.[2]

Ewe mwanangu! Kwanza rafiki kisha njia (au mtu wa njiani).[3]

Ewe mwanangu! Jogoo asiwe ni mwenye akili zaidi kukuliko wewe, huamka wakati wa usiku wa manane na kuomba msamaha huku wewe ukiwa umelala.[4]

Ewe mwanangu! Weka muda maalumu katika siku zako mchana na usiku na katika masaa yako kwa ajili ya kutafuta elimu, hakika wewe hutajikuta kuwa ni mwenye kupoteza

[1]-Sharhu Usuulul-Kafiy juzuu 8 \ 320 cha Mawlaa Muhammad Swaalih al-Maazandaraniy- al-Wasaaili juzuu 8 \ 528.
[2]-Chanzo kilichotangulia ukurasa 382.
[3]- Mustadrakul-Wasaail juzuu 8 \ 210.
[4]-Mustadrakul-Wasaail juzuu 12 \ 146.

muda huo kama ambavyo ungeacha kuitafuta elimu hiyo.[1]

Ewe mwanangu! Kushiba sana hukuzuia na kukutoa kunako mazingatio, na huuzuia ulimi wako kuzungumza hekima, na hukufanya mzito katika kutekeleza ibada.

Hudhuria kwenye maombolezo na maatam, na wala usihudhurie kwenye sherehe za harusi, hakika maombolezo na maatam hukumbusha akhera, na sherehe za furaha hukumbusha dunia.[2]

Ewe mwanangu! Jifunze hekima utapata utukufu kwa hekima hiyo, hakika hekima inajulisha juu ya dini na humtukuza mtumwa na kumfanya awe mbora zaidi kuliko muungwana (mtu aliye huru), humuinua masikini juu ya tajiri, humtanguliza mdogo juu ya mkubwa, humkalisha masikini vikao vya wafalme, sharifu na mtukufu humuongezea na kumzidishia utukufu wake na sayyidi humzidishia ukarimu na sifa ya utajiri. Ni vipi mwanadamu anadhani ya kuwa mambo ya dini na maisha yake yatamtengemea bila kutumia hekima? Na kamwe Mwenyezi Mungu hataliandaa jambo la kidunia na akhera isipokuwa kwa hekima. Mfano wa hekima bila ya utiifu ni sawa na mwili isiokuwa na nafsi, na ni sawa na udongo wa mfinyanzi usiokuwa na maji. Hauna faida yoyote mwili usiokuwa na nafsi wala udongo wa mfinyanzi usiokuwa na maji wala hekima isiyo kuwa na utiifu.[3]

Ewe mwanangu! Mzazi kumpiga mtoto wake ni sawa na

[1]-al-Aamaliy cha Shekh Mufiid ukurasa 292, na al-Amaaliy cha Shekh Tuusiy ukurasa 68, na ad-Durrun-nadhiim ukurasa 640.

[2]-Aadabun-Nafsi juzu 1 \ 185-189- cha Sayyid Muhammad al-Ainathiy (Mungu autukuze utajo wake).

[3]-al-Muuminuun fil-Qur'an juzuu 1 \ 198- Kutoka kwa Buhar juzuu 78 \ 458 mlango 33 h 27.

mbolea kwa mimea [1]. Mwenye kusema uongo basi maji ya uso wake (heshima yake) hutoweka, (yaani huaibika), na mwenye kuwa na tabia mbaya basi ghamu yake huzidi na kuongezeka, na kuhamisha mawe makubwa kutoka kwenye sehemu zake ni kwepesi zaidi kuliko kumfahamisha asiyefahamu.

Usiruhusu kuliwa chakula chako ila na Wacha Mungu na watake ushauri maulamaa na wanazuoni kuhusu mambo yako.

Ewe mwanangu! Ikiwa utataka kufanya udugu na mtu yeyote basi mkasirishe kabla ya kufanya naye urafiki. Ikiwa atakuwa muadilifu na mwenye insafu kwako wakati akiwa amechukia na mwenye ghadhabu basi fanya naye urafiki la sivyo, jihadhari naye.

Na maneno yako yafanye mazuri na ufanye uso wako uwe mkunjufu utakuwa ni mwenye kupendwa sana kwa watu kuliko awapaye kitu fulani.[2]

Ewe mwanangu! Mwenye kupata elimu ni kitu gani kilichomkosa au alichokikosa? Na aliyepitwa na kukosa elimu ni kitu gani alichokipata?

Ewe mwanangu! Muogope Mwenyezi Mungu Mtukufu uogopaji ambao lau siku ya kiama utapewa au kuletewa wema wote na matendo yote ya majini na watu ungeogopa asikuadhibu, na mtaraji Mwenyezi Mungu Mtukufu matarajio ambayo lau kama siku ya kiama utakuja na madhambi ya majini na watu ungetaraji Mwenyezi Mungu akusamehe.

[1]-Imepokelewa hadithi kama hii pia kutoka kwa Amiril-Muuminiin (AS), angalia: Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil-Hadiid juzuu 20 \ 325.

[2]-Ruuhul-maaniy- juzu 21 \ 83-84- cha Aalusiy AL-baghdadiy- Daru ihyaait-turaathil-arabiy –Bairuti.

Mwanawe akamwambia: Ewe baba yangu! Vipi nitaliweza hilo wakati ambapo nina moyo mmoja? Luqman akasema: Ewe mwanangu! Lau kama moyo wa Muumini ungetolewa na kupasuliwa ungekutwa una nuru mbili ndani yake nuru ya khofu na nuru ya matarajio, na lau kama zote mbili zingepimwa na kuwekwa kwenye mizani basi mojawapo isingekuwa nzito zaidi kuliko nyingine kwa kitu chochote walau kwa uzito wa chembe moja. Basi mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu na kuyakubali na pia kuyaswadikisha aliyoyasema Mwenyezi Mungu Mtukufu, hufanya aliyoyaamrisha na Mwenyezi Mungu. Na asiefanya aliyoamrisha Mwenyezi Mungu wala kuyakubali na kuyaswadikisha aliyoyasema Mwenyezi Mungu, hakika tabia hii inaishuhudia nyingine. Basi mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu imani ya kweli hufanya matendo kwa aikhlasi Yake, na mwenye kufanya amali kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwa akhlasi akitoa nasaha na akimuamini Mwenyezi Mungu na mwenye kumswadikisha, na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu mtukufu humuogopa, na mwenye kumuogopa kwa hakika amempenda na mwenye kumpenda hufuata amri Zake na mwenye kufuata amri Zake huwajibikiwa pepo na maridhio Yake. Na asiyefuata maridhio ya Mwenyezi Mungu kwa hakika amemfanyia khiyana Mwenyezi Mungu, na mwenye kumfanyia khiyana Mwenyezi Mungu atawajibikiwa ghadhabu na adhabu Yake - twajikinga na Mwenyezi Mungu kutokana na ghadhabu, udhalilishaji na maangamizo Yake (ghadhabu na mateso Yake)[1]

[1]-Tafsiir Ali bin Ibrahiim juzuu 2 \ 164, Tafsiirul-Burhaan juzuu 3 \ 273 na katika ukurasa 272 kutoka kwa Kulainiy Thiqatu-Islaam kwa sanadi yake hadi kwa Haarithi binil-Mughiirah au baba yake kutoka

Ewe mwanangu! Amali yoyote haiwezekani kutekelezwa isipokuwa kwa kuwa na yakini, na mtu hafanyi kitendo isipokuwa kwa kiwango cha yakini yake.[1] Mfanya amali asizembee na kufanya uvivu hadi ipungue na kudhoofu yakini yake. Kwa hivyo yakini ikawa bora zaidi kuliko elimu, kwa sababu yakini ndiyo imuitayo mtu kwenye amili au kutenda matendo, na kiitiacho kwenye matendo na amali kitakuwa ni bora zaidi kuitia kwenye ibada na utumwa kwa Mwenyezi Mungu, na chenye kuitia kwenye uja na utumwa kitakuwa ni chenye kuitia kwenye utekelezaji wa haki za uungu na kuitia kwenye ukamilifu wa hadhi fulani au sehemu fulani ya yakini.[2]

Ewe mwanangu! Jihadhari na kujifunga kitambaa kichwani kwani tendo hilo ni lenye kutisha na kuogopesha usiku na lenye kutia udhalili mchana.

Ewe mwanangu! Zidisha kutaja kauli isemayo: Ewe Mola wangu! 'Nisamehe makosa yangu', hakika Mwenyezi Mungu ana saa maalumu ambayo hujibu maombi ya muombaji.

Ewe mwanangu! Akikujia shetani kupitia shaka na tahayari basi mshinde kwa kushikamana na yakini na nasaha, na akikujia kupitia kwenye njia ya uvivu na

kwa Abi Abdillahi (AS) amesema: Nilimwambia: Ni yapi yaliyokuwa katika usia wa Luqman? Akasema: Kulikuwa na maajabu na lilokuwa la ajabu zaidi katika usia huo ni kwamba alisema kumwambia mwanawe: Muogope Mwenyezi Mungu khofu ambayo lau kama ungemjia na wema wa Majini na watu wote basi angekuadhibu na mtaraji Mwenyezi Mungu matarajio ambayo lau kama ungemjia na madhambi ya majini na watu wote basi angekurehemu na kukuhurumia.

[1]-Yaani kwa kiwango anachokiitakidi, na kutokana na haya ndio maana ikatofautiana kati ya elimu na yakini kwani ya pili ni mahususi zaidi (Akhas).

[2]-tafsiirul-qur'anil-kariim cha Swadrul-muta'allihiin juzu 3 \ 268.

matatizo au mitihani basi mshinde kwa kutaja habari za kaburi au kwa kukumbuka kaburi na siku ya kiama, na ikiwa atakujia kupitia mapenzi na khofu au woga basi mfahamishe ya kwamba dunia ni yenye kufarakana na sisi na ni yenye kuachwa na kutengwa.

Ewe mwanangu! Ifanye takwa ya Mwenyezi Mungu kuwa ni biashara ikuleteayo faida bila ya kuwa na bidhaa uichuuzayo.

Ewe mwanangu! Usichelewe kutubia au kufanya tauba, hakika mauti na kifo huja ghafla.

Ewe mwanangu!Usichukizwe sana na mtu mwenye mikono miwili mikubwa na mipana anayemwaga damu za waumini. Hakika mtu huyo ana mbele ya Mwenyezi Mungu muuaji asiyekufa.

Ewe mwanangu! Hakika hekima imewakalisha masikini vikao au mahala na sehemu za wafalme.

Ewe mwanangu! Kaa na watu wema kati ya waja wa Mwenyezi Mungu, kwa hakika wewe utapata kheri kwa kukaa nao, na huenda kheri ya mwisho uwezayo kuipata kwenye vikao hivyo ni kuteremkiwa pamoja nao na rehma.

Ewe mwanangu! Usikae na watu waovu na wenye shari, hakika wewe hutopatwa na kheri kwenye vikao vyao bali huenda mwishoni mwa vikao hivyo wakateremkiwa na adhabu na wewe kupatwa na adhabu hiyo pia.

Ewe mwanangu! Ufikapo kwenye mkusanyiko na mjumuiko wa watu basi wapige kwa mshale wa Uislamu kisha kaa pembezoni mwao. Ikiwa Watajishughulisha na kumtaja Mwenyezi Mungu basi kaa nao, na ikiwa watajishughulisha na mambo mengine yasiyo ya kumtaja na

kumtukuza Mwenyezi Mungu basi jiepushe nao[1]

Ewe mwanangu! Akikujia mtu yeyote hali ya kuwa macho yake hayaoni basi usimhukumu mpaka aje mgomvi wake, huenda akaja hali ya kuwa ameng'oa na kutoa macho manne.[2]

Ewe mwanangu! Simamisha swala, hakika mfano wa swala katika dini ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa nguzo ya hema. Nguzo inapokuwa imara huzinufaisha kamba na vigingi na vivuli, na kama haikuwa imara haitazinufaisha nguzo, vigingi, kamba wala kivuli.

Ewe mwanangu!Fuatana na maulamaa na kaa nao kwenye vikao vyao na watembelee majumbani mwao huenda ukafanana nao nawe kuwa miongoni mwao.

Fahamu ewe mwanangu: Hakika mimi nimeonja uvumilivu na subira na aina tofauti za machungu na sikuona kitu kilicho kichungu sana kuliko ufukara. Kwa hivyo basi, ikiwa siku moja utakuwa fukara basi uweke ufukara wako kati yako na Mwenyezi Mungu na wala usiwasimulie watu ufukara wako na wewe kuwa dhalili kwao. Kisha waulize watu je, kuna yeyote aliyemuomba

---

[1]-Imekuja kutoka kwa Hassan bin Ali bin Abi Harb banil-As'wad ad-Dualiy kwamba:Tulikuwa tumekaa kwa Abi Amru bin al-Alaa basi akamkumbuka Sayyid Himyariy aliyekuwa mshairi na mwenye kuwapenda Ahlul-Baiti (AS) na akaja na kukaa na tukazama katika kuzungumzia mazao na mitende kwa muda wa saa moja akasimama nasi tukasema: Ewe Aba Haashim, kwa nini umesimama na kutoka? Akasema: Hakika mimi ninachukia kukaa sana bila kutaja kwenye kikao hicho fadhila za Aali Muhammad.
Kikao ambacho hatajwi ndani yake Ahmad na wasii wake na watoto wake hicho ni kikao kilichokaliwa na watu waliotokana na watu wenye mbegu mbaya.
Hakika yule ambaye anawasahau na kutowataja katika kikao chake hadi kutoka kwenye kikao hicho basi mtu huyo si mwenye kuongoka.
[2]-ad-Durrul-Manthuur juzuu 5 \ 162-165.

Mwenyezi Mungu na asimjibu na kumuitikia, au alimuomba na hakumpatia?

Ewe mwanangu! Kuwa na imani ya kweli na Mwenyezi Mungu (kuwa na thiqa na Mwenyezi Mungu). Kisha waulize watu je, kuna yeyote aliyekuwa na imani ya kweli na Mwenyezi Mungu naye asimjibu?

Ewe mwanangu! Tawakali kwa Mwenyezi Mungu, kisha waulize watu, ni nani ambaye alitawakali na kumtegemea Mwenyezi Mungu naye asimtosheleze?

Ewe mwanangu! Mwenye kutaka maridhio ya Mwenyezi Mungu huikasirisha sana nafsi yake, na asiyeikasirisha nafsi yake hamridhishi Mola wake, na asiyevunja ghadhabu yake humfurahisha adui yake.

Ewe mwanangu! Ni nani ambaye alimtaka Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na asimpate, na ni nani ambaye alijitegemeza na kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu naye asimtetee na kumkinga na madhara.

Ewe mwanangu! Ninakuhimiza juu ya mambo sita, hakuna jambo lolote kati ya mambo hayo isipokuwa hukukaribisha kwenye maridhio ya Mwenyezi Mungu na kukuepusha au kukuweka mbali na ghadhabu Yake. Jambo la kwanza: Umuabudu Mwenyezi Mungu na usimshirikishe na chochote. La pili: Kuridhia hukumu na kadari ya Mwenyezi Mungu na makadirio yake katika yale uyapendayo na uyachukiayo. Jambo la tatu: Upende kitu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na ukichukie kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. La nne: Uwapendee watu ukipendacho wewe mwenyewe na uwachukie yale uyachukiayo wewe. La tano: Uvunje ghadhabu yako na umfanyie wema aliyekukosea na kukutendea ubaya. Na jambo la sita: Kuacha matamanio ya nafsi na kupingana na matamanio ya

nafsi na mambo mabaya yenye kuangamiza.[1]

Imepokelewa kutoka kwa Imamu wa Sita Imam Jaafar Swaadiq (AS) ya kwamba Luqman Hakiim alikuwa akimpatia mawaidha mwanawe Maathaan hadi akavimba na kupasuka[2] na hii ni kinaya ya kuathirika kwa kiasi kikubwa na mawaidha hayo.

[1]-Kanzul-Fawaaid cha al-Karaajikiy ukurasa 214, 215, 272-chapa ya Hajariyyah.
[2]-Tafsiirul-Burhaan juzuu 3 \ 273.

WAFALME WA AFRIKA SI MADHALIMU NA ARDHI YA AFRIKA NI ARDHI YA UKWELI

Kwa hakika Mtume wetu mkarimu (SAW) aliishi zama moja na wafalme kadhaa waliotawala ulimwenguni, kama vile Mfalme Harqol wa Roma, Mfalme Khosro wa Ufarsi (Uajemi), Mfalme Najashiy wa Uhabeshi ambayo hivi leo hujulikana kama Ethiopia na maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi hiyo, na Mfalme Muqawqis wa Iskandariyyah huko Misri na ambaye alijulikana kwa adabu yake nzuri na kuelewana kwake na Mtume wa Mwenyezi Mungu mtukufu (SAW) - Haatwib bin abi Baltaa'ah.[1]

Kwa hakika Mtume (SAW) alimuandikia barua Muqawqis kiongozi na rais wa kabila la Qibtwi na ambaye alikuwa ni Mkiristo na mfalme aliyekuwa akifuata ufalme wa Roma. Akaja na barua Haatwib hadi akaingia Misri na kutofanikiwa kumkuta huko. Akaeelekea Iskandariyyah na kupewa habari ya kuwa yeye yuko kwenye kikao kilicho karibu na bahari. Basi Haatwib akapanda jahazi na kuelekea mahali alipokuwa na akamuashiria kwa barua. Muqawqis alipomuona Haatwib akaamuru aletwe mbele yake. Alipoletwa kwake aliiangali barua hiyo akaifungua na kuisoma na kisha kumuuliza Haatwib: Ni jambo gani lililomzuia ikiwa ni Mtume kuwaombea maangamizi waliompinga au waliomtoa kwenye mji wake na kwenda kwenye mji mwingine maombi ya kuwatawala na kuwadhibiti? Yakamtoka maneno kisha akanyamaza.

Haatwib akamuuliza: Je, si wewe unashuhudia kuwa Isa

[1]-Angalia Tarikhu peyambar aislaam: ukurasa 494.

bin Maryam ni Mtume wa Mwenyezi Mungu? Basi ni kwa nini hakumwomba Mwenyezi Mungu awaangamize watu wake walipojaribu kumuua hadi Mwenyezi Mungu alipompaisha kwake?

Akasema: Asante sana inaonekana wewe ni mtu mwenye hekima utokaye kwa mtu mwenye hekima.

Kisha Haatwib akamwambia: Hakika kabla yako kuna aliyekuwa akidai kuwa yeye ni mungu mkuu (yaani Farauni) na Mwenyezi Mungu akamchukua na kumshika kwa adhabu ya wa mwisho na wa mwanzo (ikiwa ni mazingatio ya wa mwanzo na wa mwisho), na akalipiza kisasi kumuadhibu, kisha akalipiza kisasa kutoka kwake basi chukua ibra na fanya mazingatio kutoka kwa wenzako, na wala wenzako wasichukue ibra na mazingatio kutoka kwako. Hakika Mtume huyu aliwaita watu na kuwalingania na watu waliokuwa wakaidi na maadui wakubwa kwake ni Makuraishi, na maadui wakubwa zaidi kwake walikuwa ni Mayahudi. Waliokuwa karibu zaidi kwake ni Wakiristo. Ninaapa kwa umri wangu kwamba bishara ya Musa ya kuja kwa Isa (juu yao rema na amani) ni kama ilivyokuwa bishara ya Isa kuhusiana na kuja kwa Muhammad (SAW). Haukuwa wito na ulinganio wetu kwako kuikubali Qur'an isipokuwa ni kama ulivyo wito na ulinganio wako kwa watu wa Taurati kuikubali Injili. Kila mtume au nabii aliyekutana na kuuona umma fulani basi watu hao na umma huo ni katika umma wake. Basi ni wanawajibika kumtii, na wewe ni miongoni mwa watu waliomdiriki na kumuona Mtume huyu na hatukuzuii na kukukataza kufuata dini hii ya Ukiristo bali tunakuamuru uifuate vilivyo.

Muqawqisi akasema: Hakika mimi nimezingatia suala la

mtume huyu na nikamkuta kwamba haamrishi mambo ambayo watu hujitenga nayo, na wala hakatazi mambo wayapendayo watu, na wala sikumkuta kuwa ni mchawi aliyepotoka wala kama kuhani aliye muongo. Nimemkuta akiwa na chombo cha utume kwa kutoa habari zilizofichika na habari za njozi, na nitaangalia. Kisha akaichukua barua ile na akaiweka kwenye (hukku)[1] chombo kilichotengenezwa kwa pembe ya tembo na kuziba au kukifunika na kumpatia mjakazi wake.[2]

Lakini ambaye alikuwa ni mbora kuliko wote ni Najashiy Mfalme wa Uhabeshi.

Imeelezwa katika Siiratu Ibn Is'haq (85-151 h) ya kwamba Mtume Mtukufu (SAW) alipowaona maswahaba wake wakipata na kupambana na matatizo, shida na mabalaa makubwa, na kwamba Mwenyezi Mungu alikuwa amemuepusha na hayo, na kwamba yeye hakuwa na uwezo wa kuwazuia na kuwakinga na maudhi ya watu wao, na kwamba hakukuwepo katika kaumu zao watu waliokuwa na uwezo wa kuwazuia mateso hayo kama alivyofanyiwa yeye na ami yake Abu Twalib (AS) (baba yake Amiril-muuminiin AS), aliwaamuru kuhajiri na kwenda Uhabeshi au kuhamia Uhabeshi, na akiwaambia:

إِنَّ بِهَا مَلِكاً لاَ يُظْلَمُ النَّاسُ بِبِلاَدِهِ، فِي أَرْضِ صِدْقٍ؛ فَتَحَرَّزُوا عِنْدَهُ حَتَّى يَأْتِيَكُمُ اللهُ عَزَّ وَجَلَّ بِفَرَجٍ مِنْهُ وَيَجْعَلَ لِي وَلَكُمْ مَخْرَجاً.

Hakika katika ardhi hiyo kuna mfalme ambaye hakuna

[1]-al-Huqqu: Ni chombo kidogo chenye kifuniko kitengenezwacho kutokana na pembe ya tembo au chupa au kitu kingine tofauti na vitu hivyo viwili vilivyotajwa.

[2]-Angalia kitabu kiitwacho Makaatibur-Rasuul (SAW) juzuu 2 \421-322.

mtu yeyote adhulumiwaye kwenye nchi yake, ni ardhi ya ukweli. Basi kimbilieni huko na jikingeni na ngome yake mpaka Mwenyezi Mungu Aliyetakasika akuteremshieni faraja na kutunusuru sote.

Kikundi fulani cha maswahaba wake wakahamia kwenye Ardhi ya Uhabeshi kwa kuogopa fitina,na wakakimbilia kwa Mwenyezi Mungu wakiwa wamehifadhi dini yao.[1]

Na Bwana Qutubddini Saidi bin Hibatulaah ar-Rawandiy (Mungu autukuze utajo wake - aliyefariki mwaka 573 Hijiria) amesema kwamba: Pindi maudhi ya Makuraishi dhidi ya Mtume (SAW) na maswahaba wake yalipopindukia aliwaamuru watoke na kuelekea Uhabeshi, na akamuamuru Jaafar bin Abi Twalib[2] awaongoze. Jaafar akatoka akiwa na wanaume sabini na kutumia vyombo vya baharini. Pindi Maquraishi walipofikiwa na habari za kugura kwao walimtuma Omar Binil-Aasi na Ammarah bin Waliid kwenda kwa Najashiy na kumtaka awarudishe kwa Makuraishi. Waliingia kwa Najashiy na kumpelekea zawadi. Amru akasema: Ewe Mfalme, hakika watu fulani kati ya jamaa zetu wametupinga katika dini yetu na kukimbilia

[1]-Siiratu ibni Is'haaqa ukurasa: 174.

[2]-Jaafar bin Abi Twalib ni nduguye Amiril-Muuminiin (AS) na alikuwa ni mkubwa wake (AS). Alikuwa ni miongoni mwa maswahaba wakubwa na kati ya mashahidi wa mwanzo. Ni mtu aliyehajiri mara mbili hijira ya kwanza ni ya Uhabeshi na ya pili ni ya Madina. Alikufa shahidi katika vita vya Muutah vilivyopiganwa na Warumi mwaka wa nane Hijiria, akiwa na umri wa miaka arubaini na moja na pindi walipoufikia mwili wake walimkuta akiwa na majeraha na mapigo tisini (90) kati ya kuchomwa kwa mkuki na kupigwa kwa panga au jambia. Alikatwa mikono yake katika vita na Mwenyezi Mungu mtukufu kumpatia mbawa mbili atakazopaa nazo peponi na kupewa laqabu ya Dhal-Janahaini.

kwako, basi turudishie watu hao.

Na hapo Najashi akamtumia Jaafar ujumbe na kutaka aletwe mbele ya mfalme, akasema: Ewe Jaafar! Hakika watu hawa wananiomba nikurudisheni na kukukabidhini kwao. Akasema: Ewe mfalme! Waulize je, sisi ni watumwa wao? Amru akasema: Hapana bali ni wtu walio huru na watukufu wenye heshima zao. Akasema waulize je, wana madeni wanayotudai kwa hivyo wanataka tuwalipe madeni yao? Akasema: Hapana hatuna madeni tunayowadai. Akasema: Je, kuna damu wazitakazo zilizoko mabegani mwetu? Amru akasema: hatuna damu zozote tuzitakazo zilizoko mabegani mwao na wala hatuwadai kitu chochote walichokiharibu. Akasema: Sasa ni nini wakitakacho kwetu? Amru akasema: Wametupinga katika dini yetu na kutia mfarakano katika jamaa zetu, basi turudishie watu hawa.

Jaafar akasema: Ewe Mfalme! Tumepingana nao kutokana na Mtume aliyetumwa na Mwenyezi Mungu kwetu. Ametuamuru kujivua na miungu mingine tofauti na Mungu mmoja au miungu mfano wake (Andaad)[1] na kuacha kujitibu kwa kupiga bahati nasibu (korokoro)[2]. Ametuamuru kuswali, kutoa zaka na akaharamisha dhulma na ujeuri na kumwaga damu bila ya haki, kuzini, riba, damu na mzoga, na akatuamrisha kufanya uadilifu na kutenda wema na kuwapa watu wa karibu haki zao.

[1]-Masanamu na mifano amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na wakamuwekea mifano na miungu mingine) (Sura ya 41 \ 9).

[2]-Kwani katika zama za ujahili walipokuwa wakikusudia kufanya jambo hupiga vikombe vitatu vya korokoro visivyo na nyoya wala mpini huandikwa kwenye kimoja wapo (Mwenyezi Mungu ameniamuru) na kingine huandikwa (Mola amenikataza) na cha tatu hakiandikwi chochote. Basi ikitoka ya amri hufanya kwa mujibu wake na ikitoka ya kukataza huacha jambo hilo na ikitoka ya tatu hupiga tena kwa mara ya pili ili itoke moja wapo kati ya mbili zilizoandikwa.

Anakataza maovu na mambo machafu na uzinifu (tendo la ngono kinyume cha sheria).

Najashiy akasema: Kwa ajili ya haya Mwenyezi Mungu alimtuma Isa (AS) pia. Kisha akasema: Ewe Jaafar je, umehifadhi chochote kati ya baadhi ya aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu kwa mtume wako?

Akasema: Ndio. Akasema: Soma. Jaafar akamsomea Suurat Maryam, na alipofika kwenye kauli yake Mwenyezi Mungu isemayo:

ى ى ي ي

(Na jitikisie shina la mtende utakuangushia tende mbichi tamu).[1]

Akasema: Huu ndio ukweli na haki ilivyo.

Amru akasema: Ewe Mfalme! Hakika huyu ameacha dini yetu, mrudishe kwetu na nchini kwetu. Najashi akainua mkono wake na kumpiga usoni mwake, kisha akasema: Ukimtaja kwa ubaya nitakuua, Amru akatoka huku damu ikitiririka juu ya nguo yake.

Akasema:[2] Na Ammarah alikuwa na sura nzuri na Amru alikuwa ametoka pamoja na mkewe au ahli yake, na walipokuwa kwenye jahazi walikunywa pombe. Ammarah akamwambia Amru: Mwambie mkeo anibusu, Amru akasema: Je, inajuzu na inafaa kufanya hivyo? Na pindi Ammarah alipolewa Alimtupa Amru baharini, na kujishikiza kwenye kifua au sehemu ya mbele ya jahazi na wakamtoa. Kisha pindi walipokuwa kwa Najashiy kulikuwa na mjakazi aliyesimama kichwani kwake akimkinga na kumlinda na akimuangalia Ammarah na alikuwa ni kijana

[1]-Suurat Maryam aya 25.

[2]-Akimuashiria na kumuelezea Ali bin Ibrahiim bin Haashim mwanazuwoni wa Fiqhi aliyemuaminifu (Thiqah).

wa kuvutia na mzuri. Amru aliporudi nyumbani kwake alimwambia Ammarah: Unaonaje ukimtuma mjakazi wa mfalme, akafanya hivyo nayekuitika wito wake na kumkubalia. Amru akasema: Mwambie akuletee manukato kidogo ya mfalme, yule mjakazi akamletea manukato hayo na Amru akayachukua. Kitendo alichokifanya Ammarah kilikuwa moyoni mwake kwani alimtupa baharini, kasha akayaleta manukato yale kwa Najashiy na kusema: Hakika swahibu na rafiki yangu ambaye yuko nami alimtumia ujumbe mjakazi wako na akamhadaa na haya ni manukato yake. Hapo Najashiy akakasirika sana na kukusudia kumuua Ammarah kisha akasema: Haifai kumuua, kwa sababu wameingia katika nchi yangu kwa amani. Akaamuru wamfanyie jambo lolote lililo kubwa zaidi kuliko kifo, wakamchukua na kumpulizia kwenye matako yake kwa (ziibaq) akawa ni mnyama.

Amru akarudi kwa Makuraishi na kuwafahamisha habari zake, na Jaafar akabaki katika ardhi ya Uhabeshi akiwa katika hali tukufu kabisa na akiwa ni mwenye kukirimiwa. Aliendeleea kuwa huko hadi ilipomfika habari ya kuwa Mtume (SAW) amewekeana na Makuraishi makubaliano ya amani na suluhu. Hapo akarudi akiwa na watu wote waliokuwa naye na wakakutana na Mtume wa Mwenyezi Mungu hali ya kuwa ameikomboa Khaibar[1]. Jaafar alipata mtoto aitwae Abdallah bin Jaafar kutoka kwa Asmaau binti Umaisi alipokuwa Uhabeshi[2].

Na Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mungu autukuze utajo

[1]-Na hayo yalikuwa katika mwaka wa saba (7) ya mwezi wa Muharram.
[2]-Qiswasul-Anbiyaai cha Rawanbdiy ukurasa 322-323.

wake) amepokea hadithi kutoka kwa Ali bin Ibraahim, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa Haroun bin Muslim, kutoka kwa Mas'adah bin Swadaqah, kutoka kwa Abi Abdillahi (AS) kwamba: Najashiy alimwita Jaafar bin Abi Twalib na maswahaba wake na wao wakamjia akiwa nyumbani kwake na akiwa amekaa juu ya udongo huku akiwa amevalia nguo zilizoloa[1]. Jaafar akasema: Tukamuogopa pindi tulipomuona akiwa katika hali ile, na wakati alipoona hali tuliyokuwa nayo na kubadilika kwetu pia kugeuka kwa nyuso zetu akasema:

Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye amemnusuru Muhammad na kuyafurahisha macho yake. Je, nikupeni bishara? Nikasema: Ndio ewe Mfalme! Akasema: Hakika amenijia mpelelezi mmojawapo kati ya wapelelezi wangu wa huko hivi sasa kutoka nchini kwenu.[2] Amenipatia habari ya kuwa Mwenyezi Mungu Aliyetakasika amemnusuru Mtume wake Muhammad (SAW) na amemuangamiza adui wake na fulani na fulani na fulani wameshikwa mateka na walikutana katika bonde liitwalo: Badru[3]-Kathiirul-Araak,[4] na mimi kana kwamba ninamuangalia na kumuona[5] kwani nilikuwa nikimchungia bwana

[1]-Yaani nguo zenye maji.
[2]-Yaani jasusi au mpelelezi.
[3]-Hili ni jina la sehemu iliyoko kati ya Makkah na Madinah.
[4]-al-Araak ni mti ambao hutumika vijiti vyake kwa kupigia mswaki.
[5]-Kauli yake: Kana kwamba mimi ninamuangalia. Baadhi wamekuwa na ihtimali ya kuwa haya ni maneno ya Najashiy, kwa sababu wao walitaja na kusema ya kuwa baba yake Najashiy alikuwa ni mfalme wa Uhabeshi na hakuwa na mtoto mwinginewe tofauti na huyo, na Najashiy alikuwa na Ami yake (baba yake mdogo) aliyekuwa na watoto kumi na mbili, watu wa Uhabeshi wakasimama na kumuua baba yake Najashiy na kumtii ami yake na kumfanya kuwa mfalme na kwamba Najashiy alikuwa akimtumikia ami yake. Watu wa Uhabeshi

wangu (Sayyid wangu) huko naye ni mtu mmoja katika kabila la bani Dhamrah. Jaafar akamwambia: Ewe mfalme! Vipi nakuona ukiwa umekaa juu ya udongo na ukiwa na nguo hizi zilizoloa? Akamwambia: Ewe Jaafar! Hakika sisi tunaona kati ya mambo yaliyoteremshwa kwa Isa (AS), ya kwamba, ni haki ya Mwenyezi Mungu kwa waja wake wamnyenyekee pindi anapowaletea neema. Na wakati Mwenyezi Mungu aliponipatia neema kwa kuja Muhammad (SAW) nikafanya hivi au nikawa katika hali hii. Pindi jambo hilo lilipomfika Mtume (SAW) akasema kuwaambia maswahaba wake: Hakika sadaka humzidishia mwenye kuitoa wingi basi toeni sadaka Mungu akurehemuni, na kwa hakika unyenyekevu humuongezea mwenye aliye nao daraja na utukufu, basi kuweni wanyenyekevu Mwenyezi Mungu atakuinulieni daraja zenu, na kwa hakika usamehevu humuongezea mwenye aliye nao

wakasema kumwambia mfalme: Hakika sisi hatutakuwa na amani kwa mtoto huyu atutawale kwa muda wa siku moja na kututaka sisi fidia ya damu ya baba yake basi muue.
Mfalme akasema: Jana Mlimuua baba yake na hivi leo nimuue mwanawe, mimi siridhii kufanya hivyo na ikiwa mtataka basi muuzeni kwa mtu mgeni amtoe kwenye mji wenu. Wakafanya hivyo na baada ya muda yule mfalme akapatwa na mshutuko na kufariki na hakukuwa na yeyote kati ya watoto wake mwenye uwezo wa kutawala. Wakalazimika kuja na kumchukua Najashiy kwa siri kutoka kwa bwana wake aliyemnunua bila kutoa thamani na kumrudisha kwenye nchi yao na kumfanya kuwa mfalme. Mara bwana wake akaja na kumdai au kuwataka wamrudishe na kulifikisha suala lake kwa Najashiy bila ya kumfahamu na akatoa hukumu dhidi yao. Aliwaambia: Imma mumpe kijana wake au thamani, na hapo wakampatia thamani yake,- Angalia kitabu kiitwacho Mir'aatil-Uquul, juzuu 8 \ 245- Baadhi ya wanahistoria wanasema kuwa kuna uwezekano kwamba yalikuwa ni katika maneno ya jasusi, na huenda ihtimali hii ndiyo iliyo karibu zaidi na ukweli.

utukufu na izza, basi kuweni wasemehevu mwenyezi Mungu atakutukuzeni.[1]

Na Abu Bakri Muhammad bin Jaafar bin Sahli as-Saamiriy aliye maarufu kwa jina la al-Kharaaitwiy (240-327 h) amesema: Tumesimuliwa na Hassan bin Yazid al-Jaswas, tumesimuliwa na Abu Swalamah Hammad bin Swalamh, tumesimuliwa na Zakaria bin Abi Zaaidah kutoka kwa Abi Is'haaq, kutoka kwa Said bin Maabad amesema: Nilisimuliwa na As'maau binti Umaisi ya kwamba, Jaafar alimjia walipokuwa katika ardhi ya Uhabeshi, huku akilia, nikamuuliza, 'una nini au umepatwa na nini?' Akasema: Nimemuona kijana mnene mwenye neema na mali nyingi kati ya watu wa Uhabeshi alipita kwa mwanamke mmoja na kumwaga unga aliokuwa ameubebea, na ukapeperushwa na upepo, nikasema: Ninakuacha hadi siku ambayo mfalme ataketi juu ya kiti chake na kuichukua haki ya mwenye kudhulumiwa kutoka kwa dhalimu.[2]

Hadi ilifikia kwamba Mtume Mtukufu (SAW) alimtuma Amru bin Umayyah Adhwamriy – na alikuwa ndiye balozi wa kwanza aliyetumwa na Mtume (SAW) kwa wafalme akiwaita na kuwalingania kwenye Uislamu- kwa Najashiy aliyechukua barua ya Mtume (SAW) na kuiweka juu ya macho yake na kuteremka kutoka kitandani kwake kisha akakaa juu ya ardhi kwa unyenyekevu kisha akasilimu na kushuhudia shahada ya haki na akamuandikia barua Mtume (SAW) juu ya kuitika kwake na kuswadikisha kwake ujumbe wake na kusilimu kwake mbele ya Jaafar bin Abi

[1]-Al-Kafiy –juzuu 2 \ 121-babut-tawaadhui.
[2]-Masaawiul-Akhlaaq- ukurasa 249-chapa ya Muassasatul-Kutubit-Thaqaafiyyah –Beirut- chapa ya kwanza mwaka 1993 h.d.

Twaalib nduguye Amiril-muuminiin Ali (AS).[1]

Kwa hakika Mtume wetu Mtukufu (SAW) alimuandikia Najashiy barua na kuituma kupitia kwa Amru bin Umayyah kuhusu suala la Jaafar bin Abi Twalib na maswahaba wake na imekuja kwenye barua hiyo kama ifuatavyo:

'Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu. Kutoka kwa Muhamma Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenda kwa Najashiy al-Adhkham kiongozi wa Uhabeshi amani iwe juu yako. Hakika mimi ninamsifu Mwenyezi Mungu kwako ambaye ni Mfalme, Mtakasifu, Muumini Mwenye kutawala mambo yote. Na ninashuhudia ya kwamba Isa bin Maryam ni roho ya Mwenyezi Mungu na ni neno lake alililoliweka kwa Maryamul-Batuul-aliyehifadhiwa na uchafu, aliye mwema na mwenye kuhifadhika na maasi, na kubeba mimba ya Isa, na kumuumba kutokana na roho yake na kumpulizia roho yake kama alivyomuumba Adam kwa mkono wake (uwezo wake) na kumpulizia ndani yake roho. Kwa hakika mimi ninakuita na kukulingania kwa Mwenyezi Mungu wa pekee asiye na mshirika, na kumtawalisha kwa kumtii, na kwamba unifuate mimi na uniamini na yale yaliyonijia, kwa hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Nimetuma kwenu mtoto wa ami yangu Jafar bin Abi Twalib, akiwa na kundi la Waislaamu, wakikujia basi kiri na kusalimu amri kwake[2] na acha kujigamba kwa ukubwa (kiburi). Kwa hakika mimi ninakuita wewe na watu wako kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kwa hakika nimefikisha na kunasihi, basi

[1]-Angalia Taarikhu Payambar Islaam ukurasa 494 na Makaatibur-Rasuul (SAW) juzuu 1 \.

[2]-Yaani mthibitishie uislaam wako, na huenda neno hilo likatokana na neno Al-qira lenye maana ya kuwapokea kama wageni na ikiwa ni hivyo hapo tutalisoma bila ya kutia shadda kwenye ree.

kubalini nasaha zangu na amani iwe juu ya mwenye kufuata uongofu.'

Na Najashi akamuandikia: Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu. Barua kuelekea kwa Muhammad Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) kutoka kwa Najashiy Adhkham bin Abhar. Amani iwe juu yako ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu kutoka Kwake na rehama za Allah na baraka zake! Hapana Mola wa haki isipokuwa Yeye ambaye ameniongoza kwenye Uislamu. Kwa hakika nimefikiwa na barua yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kuhusiana na uliyoyataja kuhusu suala la Isa, ninaapa kwa Mola wa mbingu na ardhi hakika Isa hazidi na kuyapituka uliyoyataja, na kwa hakika tumefahamu uliyotumwa nayo kwetu. Tumemkirimu na kumpokea kama mgeni wetu mtoto wa ami yako na maswahaba wake, na ninashuhudia ya kwamba wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa ukweli na mwenye kuswadikisha, na kwa hakika nimekupa baia (kiapo cha utiifu) na nimempa baia mtoto wa ami yako. Nimesilimu mbele yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, na kwa hakika nimemtuma kwako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ariiha bin Adhkham bin Abhar. Hakika mimi sina ninachokimiliki isipokuwa nafsi yangu, ukitaka nije kwako nitafanya hivyo ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Kwa hakika mimi ninashuhudia ya kuwa uyasemayo ni haki na kweli.

Kisha akamtumia zawadi Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), na akamtumia kijakazi aitwaye Mariya Qibtwiyyah[1]

[1]-Hii ni tofauti na ilivyo maarufu kati ya waandishi wa historia ya kwamba Maria Qibtwiyyah alikuwa ni moja ya zawadi za Muqawqisi

mama yake Ibraahim (AS). Alimtumia nguo na manukato mengi na farasi, na akamtumia watu thalathini kati ya makasisi ili wakayasikilize na kuyachunguza maneno, makao na kinywaji chake au (kifaa kinyweacho maji). Watu wale wakasafiri hadi Madinah, na Mtume (SAW) akawaita na kuwalingania kwenye Uislamu, wakaamini na kurejea Uhabeshi.[1]

Bwana Zurarah amepokea hadithi kutoka kwa Abi Jaafar al-Baaqir (AS) ya kwamba amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) alikuwa amemtuma kabla ya kwenda Khaibar, Amru bin Umayyah Adhwamriy kwa Najashiy mkuu wa Uhabeshi, na kumuita pia kumlingania kwenye dini ya Kiislamu, naye akasilimu, na alikuwa amemuamuru Amr atangulie pamoja na Jaafar na sahaba zake, na Najashiy akamuandalia Jaafar na sahaba zake maandalizi mazuri na akaamuru waletewe mavazi (nguo) na akawabeba kwenye majahazi mawili.[2]

Kisha imepokelewa ya kwamba Mtume (SAW) alipojiwa na Jibrilu alimfahamisha msiba wa Najashiy[3] akalia sana na kumhuzunikia na akasema: Hakika ndugu yenu As'ham (Nalo ni jina la Najashiy) amefariki. Kisha akatoka hadi mahala paitwapo Jabanah na kumsalia, akapiga takbira mara saba na Mwenyezi Mungu akamshushia kila kilichokuwa kirefu hadi akaliona jeneza lake hali ya kuwa

mkubwa wa kabila la Qibtwi kama ambavyo tutaelezea hapo baadaye Inshaallah taala chini ya anwani (Ukwe wa Mtume (SAW) kwa watu wa Afrika).

[1]-Qiswasul-Anbiyaai cha Rawandiy ukurasa 324.

[2]-Makaatiibur-rasuul (SAW) juzuu 2 \ 445.

[3]-Imepokelewa ya kwamba hilo lilifanyika katika mwezi wa Rajabu mwaka wa tisa Hijiria- Makatiibur-Rasuul juzuu 2 \ 438.

yuko Uhabeshi.[1]

Tunasema: Amesema Kiongozi wa Watu (viumbe) na Saiful-Islaam na Bendera ya Wanazuoni Shekh Jaafar Kaashiful-Ghitwaa (Mungu autukuze utajo wake - aliyefariki dunia mwaka 1228 Hijiria) kwamba: Na wala haisihi (yaani kumsalia maiti) aliyeghaibu, na tukio la kumsalia Najashi hali ya kuwa yuko ghaibu ni suala lihusikalo na tukio hilo tu, au kwa twayyir-ardhi, au kuhudhuria kama vile upepesuaji wa jicho la Balqisi - bila ya kuona - na hayo yote mawili hayako mbali na uwezo wa Bwana wa majini na watu.[2]

Na kutokana na kisa cha Najashiy tunafaidika na kupata natija ya kwamba, sehemu ya kwanza kuenea Uislamu nje ya Bara Arabu, ni katika nchi za Afrika, na hiyo ni kutokana na ubora wa kusilimu kwa Najashiy na watu wake au maswahaba wake. Wakati huohuo mjumbe wa kwanza kutumwa kwa wafalme ni mjumbe ambaye alitumwa kwa Najashiy na kumjibu na kumpokea kwa wema, na hili linatujulisha usafi wa watu hawa watukufu, wakarimu, wateule na usalama wa maumbile yao.

Kama ambavyo tunafaidika kutokana na kisa cha Najashiy pia ya kwamba, Afrika ilikuwa ni sehemu na ardhi nzuri na bora ulimwenguni kwa upande wa ukimbizi wa kisiasa na kiitikadi kwa ajili ya Waislaamu katika zama zile.

[1]-Safiinatul-Buhaar-Madda: Najasha.

[2]-Kashful-Ghitaa juzuu 2 \ 281.

UKWE WA MTUME MTUKUFU (SAW) KWA WATU WA AFRIKA

Ni jambo lililo maarufu kati ya wanazuoni wa Fiqhi au mafuqaha ya kwamba, mama wa mjakazi aliyeingiliwa kimwili ni haramu kwa mtu aliyemuingilia hata kama kizazi chake kitaendelea juu na kuwa kikubwa, awe ni mama wa upande wa baba au wa mama (yaani nyanya yake mjakazi aliyeingiliwa kutoka pande zote mbili za mama na baba yake). Haya ndiyo waliyoyataja katika hukumu za mambo yaharamishwayo kwa sababu ya kuoleana au kwa sababu ya ukwe katika vitabu vyao vya fiqihi.[1]

Kwa msingi huo, baada ya Mtume Mtukufu (SAW) kumtuma mjumbe wake (Haatwib bin Abi Balta'ah) kwenda kwa Muqawqis mkuu wa kabila la Qibtwi[2] huko Misri, amlinganie kwenye Uislamu jibu la mfalme huyo halikuwa jingine isipokuwa alimtumia Mtume habari akimfahamisha ya kuwa yeye anaitakidi ya kwamba atadhihiri mtume, na kwamba amempokea mjumbe wake kwa mambo yaliyo wajibu kwake kuyafanya kama vile kumkirimu na kwamba amemtuma na zawadi ya : wajakazi wawili na nyumbu mweupe na punda na kiasi fulani cha pesa na baadhi ya kheri na mambo mazuri ya Misri. Ama wajakazi wawili mmoja wapo alikuwa ni Maariyah binti Sham'uun al-Qibtwiyyah ambaye Mtume (SAW) alimuoa na baadaye kumzalia mtoto aliyeitwa Ibrahiim.[3]

[1]-Angalia Jawaahirul-Kalaam juzuu 29 \ 349. Na al-Uruwatul-Wuthqaa juzu 5 \, kipengele katika watu walioharamu kwa kuwa wakwe , ukurasa 543.

[2]-Qibtwi ni wakazi wa Misri wa asili, na neno (Qibtwi) asili yake ni Kiyunani lenye maana ya wakazi wa Misri-Muujamul-Wasiit.

[3]-Angalia Muruujudh-dhahabi juzu 2 \ 289-na Hayaati Muhammad (s.a.w.w): 364. Na baadhi wamesema ya kwamba:(Muqauqisi) alimtuma mganga akiwa na zawadi ali akawatibie waislaam waliokuwa wagonjwa, Mtume (s.a.w.w) akamwambia: Rejea kwa jamaa zako, hakika sisi ni watu ambao hatuli mpaka tunapokuwa na njaa, na pindi tunapo kula hatuli hadi kushiba-Makaatibur-rasuul juzu 2 \ 426.

Na huenda ni kutokana na sababu hii ndio maana ikapokelewa kutoka kwa Mtume (SAW) ya kwamba amesema: Pindi mkiikomboa Misri basi usianeni kheri kwa watu wa kabila la Qibtwi hakika wana dhimma [1] na heshima na kizazi.[2]

Imepokelewa pia ya kwamba Imam Hussein (AS) alizungumza na Muawiah kuhusiana na fidia (Jizya) ya watu wa kijiji cha mama yake Ibrahiim mtoto wa Mtume (SAW) kilichoko Misri na akawaondolea fidia hiyo (yaani akawaondolea kulipa jizya).[3]

Na kwa vyovyote itakavyokuwa kwa hakika Mtume na Nabii wa Uislamu alifungua njia nyingine kati ya njia za kuwaongoa watu kuelekea kwenye nchi za Afrika kwa kumuoa kwake Maariyah al-Qibtwiyyah, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

[1]-Dhimmah ina maana ya ahadi, amani, uharamu na haki. Huenda neno lililo kabla ya neno la mwisho ndilo lililo kusudiwa japokuwa neno la mwisho haliko mbali pia.

[2]- Futuuhul-Buldaan ukurasa 220

[3]- Chanzo hicho hicho.

MUUMINI WA KIAFRIKA NI TOSHELEZO LA MUUMINI YEYOTE

Kwa hakika ulikuja Uislamu na kuvunja au kuangamiza milla nyingi (mambo yaliyo kuwa yakifanyika kwa kawaida) na desturi mbali mbali ambazo hazikuwa zimesimama na kujitegemeza kwenye vipimo na misingi ya kiutu na maumbile aliyoyaumba Mola. Kwa mfano mtu mweupe hakuwa akimuoza binti yake mtu mweusi kwa ujumla, hata kama mtu huyo alikuwa ni mwenye kuheshimiwa na mtukufu kwenye jamii yake. Lakini kwa kuja Uislamu na Mtume (SAW) kupiga vita hali na mila hizi potofu wanadamu wakaweza kuishi maisha mema na yenye saada.

Kwa mfano huyu hapa Juwaibar Muafrika pamoja na kuwa alisilimu na kujifunga na Uislamu na akawa muumini kwa maana halisi ya neno hilo, lakini Muarabu mmoja alikataa kumuozesha binti yake kwa sababu ya weusi wa Juwaibar. Lakini Mtume Mtukufu (SAW) aliingilia kati na kuiondoa hali ile ambayo haikufaa.

Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mungu autakase utajo wake aliyefariki dunia mwaka 328 Hijiria) anasimulia kwa sanadi sahihi kutoka kwa Muhammad bin Yahya, kutoka kwa Ahmad bin Muhammad bin Isa, kutoka kwa Hassan bin Mahboub kutoka kwa Maaliki bin Atwiyyah, kutoka kwa Abi Hamzah ath-Thamaliy kwamba: Abu Jaafar amesema (yaani Imam Baqir) (AS): Hakika mtu mmoja aliyekuwa ni mkazi wa Yamamaha[1] aliyekuwa akiitwa Juwaibar alimjia

[1]-al-Yamaamah ni mji katika nchi ya Yemen na kidhahiri kama tutakavyoeleza hapo baadaye ni kwamba aliishi hapo kwa muda kadhaa, laa sivyo asili yake ni katika nchi ya Sudan mji wa Afrika kama tutakavyoeleza.

Mtume wa Mwenyezi Mungu akitaka kusilimu, na akasilimu na kuwa Muislamu mzuri. Alikuwa ni mtu mfupi, mwenye sura mbaya[1], maskini, ambaye hakuwa na nguo za kuvaa na alikuwa ni kutoka katika sehemu ya Sudan iitwayo Qibaah[2]. Mtume akamkaribisha kwake kutokana na kuwa kwake mgeni, kutokuwa na mavazi ya kuvaa na alikuwa akimpatia chakula kibaba kimoja cha tende kwa kibaba au pishi ya kwanza inapomalizika.[3] Akamvisha vikoi viwili[4] na kumuamuru akae msikitini na alale humo wakati wa usiku na akakaa katika hali hiyo kwa muda mrefu.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) siku moja alimuangalia Juwaibar kwa upole na huruma na kumwambia: Ewe Juwaibar unaonaje ukioa mwanamke na ukaweza kuuhifadhi kupitia kwake utupu wako na akakusaidia katika dunia yako na akhera yako? Juwaiba akamjibu Mtume (SAW): Ewe mtume wa Mwenyezi Mungu! Naapa kwa jina la baba na mama yangu na kuuliza, ni nani atakaenipenda mimi? Wallahi! Sina hadhi nzuri, nasaba tukufu, mali wala uzuri. Ni mwanamke gani atakayenipenda nimuoe? Mtume (SAW) akamwambia: Ewe Juwaibar! Hakika Mwenyezi Mungu kupitia Uislamu amempa hadhi yule aliyekuwa katika ujahili zamani,

[1]- Yaani mwenye sura mbaya: Na huku si kumdharau na kumuhini bali ni kutaja ukweli ulivyo ili iweze kubainika hapo baadaye utukufu wa Uislaamu kuhusiana na watu wote.

[2]-Akiashiria mahala katika nchi ya Sudan.

[3]-Ilivyo maarufu ni kwamba, Pishi au kibaba: ni sawa na vibaba au pishi nne yaani sawa na kilo tatu. Lakini imepokelewa katika hadithi ya kwamba: Kibaba au pishi ya Mtume (SAW) ilikuwa ni sawa na vibaba au pishi tano: Angalia Majmaul-Bahraini kwenye mada Swawaa'a.

[4]-Haya ni aina ya mavazi ya wanaume.

amemtukuza yule ambaye katika ujahilia alikuwa ni mtu duni, amemtukuza na kumpa izza yule ambaye katika zama za ujahili alikuwa ni dhalili na mnyonge na kuondoa mambo yote ya kiburi, kujigamba au kujifakharisha kwa makabila na nasaba zilizodai kuwa ni bora na tukufu.[1] Kwa hivyo hii leo watu wote wawe ni weupe, weusi, Makuraishi, Waarabu Waajemi (wasio waarabu) wote ni sawa na wanatokana na Aadam. Kwa hakika Adam ameumbwa na Mwenyezi Mungu kutokana na udongo, na mtu mwenye kupendwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu siku ya kiama ni yule mtiifu na mcha Mungu zaidi miongoni mwao. Ewe Juwaibar! simfahamu yeyote hivi leo kati ya Waislamu mwenye fadhila kukuliko wewe isipokuwa aliyekuwa mcha Mungu zaidi kukuliko wewe na mtiifu zaidi kwa amri za Mwenyezi Mungu. Kisha akamwambia: Ewe Juwaibar! Nenda kwa Ziyaad bin Lubaid, hakika yeye ni mtu mtukufu sana kati ya Bani Bayaadhah na mwenye hadhi kati yao. Mwambie: Hakika mimi ni mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwako naye anasema kwamba: Muozeshe Juwaibar binti yako mwenye pua dogo na zuri.

Akasema: Juwaibar akaondoka akiwa na barua ya Mtume wa Mwenyezi Mungu hadi kwa Ziyaad bin Lubaid na akamkuta akiwa nyumbani kwake na akiwa na kikundi cha watu wa kabila lake. Akaomba idhini na kuruhusiwa naye akaaingia na kumtolea salamu kisha akasema: Ewe Ziyaad bin Labaad! Mimi ni mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwako katika haja yangu. Je, niseme wazi au nikwambie kisiri? Ziyaad akamwambia: Bali iseme waziwazi, hakika kufanya hivyo ni utukufu na ni fakhari kwangu. Juwaibar akamwambia: Hakika Mtume wa Mwenyezi

[1]-Yaani mwenye nasaba tukufu.

Mungu anakwambia ya kwamba: Muoze Juwaibar binti yako mwenye pua dogo na zuri. Ziyad akamwambia: Hivi kweli Mtume wa Mwenyezi Mungu amekutuma kwangu na ujumbe huu? Akamwambia: Ndio sikuwa ni mwenye kumsemea na kumzulia uongo Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW). Ziyad akamwambia: Hakika sisi hatuwaozi mabinti zetu isipokuwa watu wenye kulingana na sisi kati ya Maanswari. Nenda zako ewe Juwaibar hadi nitakapokutana na Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na kumfahamisha udhuru wangu. Na Juwaibar akaondoka hali ya kuwa anasema: Wallahi! Hakika Qur'an haikuteremka kwa haya wala haukudhihiri utume wa Muhammad (SAW) kwa mambo kama haya. Dhulfa binti wa Ziyaad akasikia maneno yale akiwa chumbani kwake na akamuomba baba yake aje kwake. Ziyaad akaingia chumbani kwa binti yake na yule binti akamuuliza: Ni maneno gani haya ambayo nimeyasikia ukimwambia Juwaibar? Ziyaad akamjibu binti yake: Ameniambia ya kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) amemtuma akitaka nikuoze wewe kwake. Yule binti akamwambia: Wallahi! Juwaiba hakuwa ni mtu mwenye kumuongopea na kumzulia Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) uongo. Tuma hivi sasa mjumbe amrudishe Juwaibar. Ziyad akamtuma mjumbe na yule mjumbe akamfuata Juwaibar na kumuwahi njiani. Ziyad akamwambia: Ewe Juwaibar karibu sana na kuwa mtulivu mpaka nitakapo rudi kwako.

Kisha Ziyad akaondoka hadi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) akamwambia: Naapa kwa jina la baba na mama yangu! Juwaibar amenijia na ujumbe wako na kusema kuwa umemtuma nimuoze binti yangu. Sikuwa laini kwake kwa kauli niliyomjibu na nikaona ni vyema

nikutane na wewe. Sisi hatuwaozi isipokuwa wenzetu katika Maanswari. Mtume (SAW) akamwambia: Ewe Ziyaad! Juwaibar ni muumini na muumini ni mwenye kumstahili muumini wa kike na Muislamu wa kiume ni mwenye kumstahili Muislamu wa kike. Ewe Ziyaad! muoze na wala usimchukie. Akasema: Ziyaad akarejea nyumbani kwake na akaingia chumbani kwa binti yake akamwambia aliyoyasikia kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu. Yule binti akamwambia baba yake: Hakika wewe ikiwa utamuasi Mtume wa Mwenyezi Mungu utakuwa umekufuru, basi muoze Juwaibar.

Ziyaad akatoka na kuushika mkono wa Juwaibar kisha akamtoa kwa jamaa wa kabila lake na kumuoza juu ya sunna ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake (SAW) naye kuchukua dhamana ya mahari yake. Akasema: Ziyaadi akamuandalia binti yake na wakamuandaa kisha wakamtuma na kumpeleka kwa Juwaibar na wakamuuliza, je, unayo nyumba tumpeleke mkeo nyumbani kwako? Akasema: Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu mimi sina nyumba. Akasema: Wakamuandaa binti yule na wakamuandalia nyumba na wakaweka ndani yake tandiko na vitu vya matumizi, wakamvisha Juwaibar nguo mbili, wakamuingiza Dhulfaau nyumbani kwake na Juwaibar akaingizwa kwa mkewe wakati wa usiku uliotulia. Alipomuona mkewe, aliitazama kwa makini nyumba na vifaa vilivyokuwepo pamoja na kuhisi upepo mwanana uliovuma humo. Akasimama pembeni na kuanza kusoma Qur'an huku akirukuu na kusujudu hadi ikachomoza alfajiri. Aliposikia wito wa adhana akatoka na mkewe akamfuata kwenda kwenye swala akatawadha na kuswali swala ya asubuhi na akaulizwa yule bibi harusi: Je,

amekugusa (amekukaribia)? Akasema: Hakuacha kusoma Qur'an akirukuu na kusujudu hadi aliposikia adhana ya alfajiri akatoka. Ulipoingia usiku wa pili akafanya hivyohivyo kama alivyofanya usiku uliotangulia. Wakamficha Ziyad habari zile (yaani wakamficha baba yake), na ilipofika siku ya tatu akafanya vile vile Juwaiba. Akamfahamishwa habari hizo baba yake yule binti, naye akenda hadi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) kumuelezea hali ya mambo. Akamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Umeniamrisha kumuoza Juwaibar, na naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kamwe hakuwa ni katika watu wanaostahili kuoa kwetu, lakini nikamuoza kutokana na kukutiii wewe. Mtume (SAW) akamwambia: Mmeona jambo gani kutoka kwake? Akasema: Hakika tumemuandalia nyumba na vitu vya matumizi na nikamuingiza binti yangu nyumbani kwake, lakini pamoja na hayo hajazungumza naye, kumuangalia wala kumkaribia bali amesimama kwenye kona ya nyumba na kusoma Qur'an akirukuu na kusujudu hadi aliposikia adhana ya alfajiri akatoka kisha akafanya hivyo hivyo katika usiku wa pli na wa tatu. Hajamkaribia wala kumzungumzisha hadi hivi nilipokujia, na hatumuoni kama anahitaji wanawake basi lizingatie suala letu hili.

Ziyad akaondoka na Mtume (SAW) akatuma mjumbe kwa Juwaibar akamwambia: Je, wewe hauwakaribii wanawake? Juwaibar akasema: Bila shaka ninawakaribia wanawake, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu. Hakika mimi ni mwenye hamu na matamanio makubwa ya kumuingilia mwanamke na mwenye pupa na wanawake.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) akamwambia: Hakika nimepewa habari tofauti na ulivyojisifia wewe

mwenyewe. Nimeambiwa kwamba wamekuandalia nyumba na tandiko na vitu vya matumizi na wakakuletea binti mzuri sana, mwenye kupendeza na kuvutia, na ukaja usiku wa manane hukumuangalia wala kumzungumzisha na wala hukumkaribia. Ni lipi lililokupata? Juwaibar akamwambia: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! niliingia kwenye nyumba pana na kubwa na nikaona tandiko na vifaa vya matumizi na binti mrembo, mzuri na mwenye kupendeza. Mara tu nikakumbuka hali yangu ambayo nilikuwa nayo kabla ya hapo, ugeni wangu, umasikinii wangu, uduni wangu, mavazi yangu pamoja na watu wageni na masikini. Kwa hivyo mwanzo nilipendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na aliyonipatia na nijikurubishe kwake kwa shukrani ya dhati. Kwa hivyo nikasimama kwenye kona ya nyumba na nikaendelea na swala huku nikisoma Qur'an, nikirukuu na kusujudu nikimshukuru Mwenyezi Mungu hadi niliposikia wito wa dhana ya alfajiri. Nikatoka na ilipofika asubuhi nikaona ni vyema kufunga siku ile na nikafanya hivyo kwa muda wa siku tatu na nyusiku zake. Ninaona kwamba jambo hilo ni dogo sana nikililinganisha na yale aliyonipatia Mwenyezi Mungu, lakini pamoja na hayo, usiku wa leo nitamridhisha na kuwawaridhisha wao inshaallah.

Na hapo Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) akatuma mjumbe kwa Ziyaad na yeye kuja kwa Mtume na Mtume akamfahamisha aliyoyasema Juwaibar na hapo nafsi zao kufurahi. Akasema: Na Juwaibar akatekeleza aliyoyasema na kuyaahidi.

Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) akatoka kwenda kwenye vita akiwa pamoja na Juwaibar na kufa shahidi, rehma ya Mwenyezi Mungu iwe juu yake.

Hakukuwa kati ya Maanswari mjane aliyekuwa akichumbiwa na kutolewa mapesa mengi kwa ajili ya mahari yake kuliko Dhulfaau[1] baada ya Juwaibar kuaga dunia.[2]

Tunasema: Hadithi hii inathibitisha utukufu na ukubwa wa Juwaibar katika pande mbalimbali, hadi Mwenyezi Mungu alipomrejesha kwake akiwa shahidi mbele ya Mtume mtukufu (SAW). Ni watu wachache sana wenye kushukuru neema na kuzithamini kama alivyofanya Juwaibar radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Kwa vyovyote vile, hili ni somo na kigezo kwetu na kila mwenye kutaka kuufuata Uislamu na kuishi maisha mazuri na mema duniani na akhera.

---

[1]-al-Yamm: Mwanamke asiyeolewa. Na maana yake ni kuwa hakuna mwanamke yeyote aliyefiwa na mumewe aliyekuwa aking'ng'aniwa kuolewa na kuchumbiwa kuliko mwanamke huyo. Na hakuna mwanamke mwingine aliyekuwa akitolewa mahari mengi kama Dhulfaau.

[2]-al-Kafiy-Kitabun-Nikaah-Baab Annal-Muumin Kuf'ul-Muumin-h 1.

MJA MWEMA,
BILAL WA UHABESHI

Bilal wa Uhabeshi ni Bilal bin Rabah, kunia yake ni Abu Abdillah, na inasemekana kuwa ni Abu Amru. Huitwa kwa jina la Abu Abdul-Kariim, Mtumwa wa Mtume Mtukufu na Muadhini wake. Alifahamika kwa imani yake ya kweli kwa Mola wa viumbe wote na kuwatawalisha kwake Ahlul-Bait (AS).

Na imepokelewa kutoka kwa Ibnu Is'haq kwamba: Nimesimuliwa na Hishaam bin Ur'wah kutoka kwa baba yake amesema: Waraqah bin Naufal alikuwa akimpitia Bilal huku akiadhibiwa kwa kusilimu kwake, huku akisema: Ahadun, Ahadun, na Waraqah akisema: Ahadun, Ahadun (Mwenyezi Mungu ni mmoja). Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu ewe Bilal! Hakika hutokufa wala kumalizika. Kisha akimgeukia yule mtu aliyekuwa akumuadhibu na aliyekuwa akitoka katika kabila la Bani Jamh na pia kumgeukia Umayya na kusema: Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, ikiwa mtamuua juu ya hali hii basi nitamchukua kwa kumuonea huruma.[1]

Tunasema: Kauli yake: Nitamchukua kwa kumuonea huruma, huenda maana yake na makusudio yake ni kuwa: Nitalifanya kaburi lake kuwa ni sehemu ya ziara au kufanyia ibada na mahala pa kuombea rehma.

Na Ibnu Is'haq amesema: Na nikafikiwa na habari ya kuwa Ammar bin Yaasir alisema hali akimtaja Bilal bin Rabaah: Mwenyezi Mungu amlipe kheri Bilal na sahibu wake mkongwe na amuadhibu na kumdhalilisha Faakih na

[1]-Siiratu Ibni Is'haaq, ukurasa 190 chapa ya Muassasatu Ismailiyaan Qumil-Muqaddasah.

Aba Jahli. Walimkusudia Bilal wakati wa asubuhi kwa uovu, na hawakujihadhari wala kuogopa akiogopacho mtu mwenye akili. Kwa kumpwekesha kwake Mola wa viumbe na kauli yake isemayo: Ninashuhudia ya kwamba Mwenyezi Mungu ni Mola wangu nikiwa ni mwenye utulivu. Ikiwa mtaniua mtaniua hali ya kuwa sikuwa ni mwenye kumshirikisha Rahman (Mwenyezi Mungu) kwa kuogopa au kuchelea kuuwawa. Ewe Mola wa Ibrahiim na Mwenye kuabudiwa na Yunus na Musa na Isa! Niokoe kisha usimchoke yule anayeendelea kupenda uovu kati ya watu wa kabila la Ghaalib ambaye si mfanya-mema wala si mfanya-uadilifu.[1]

Na pia akasema ya kuwa mtu wa kwanza kuadhini ni Bilal.[2]

Na imepokelewa kutoka kwa Shekh Mufiid (Mungu autakase utajo wake) ya kuwa amesema: Na amesema kuhusiana naye Abu Abdillah Jaafar bin Muhammad (AS): Mwenyezi Mungu amrehemu Bilal hakika yeye alikuwa akitupenda sisi Ahlul-Bait.[3]

Na Abu Amru Muhammad bin Abdil-Aziz al-Kishiy amepokea hadithi kutoka kwa Abi Abdillah Muhammad bin Ibrahiim, kuwa: Nimehadithiwa na Ali bin Muhammad bin Yazid al-Qumiy, amesema: Nimesimuliwa na Abdllah bin Muhammad bin Isa, kutoka kwa Ibnu Abi Umair, kutoka kwa Hishaam bin Saalim kutoka kwa Abi Abdillah (AS) amesema: Bilal alikuwa ni mja mwema.[4]

Na miongoni mwa wema wake wa kidhahiri na ndani ni

[1]-Chanzo kile kile ukurasa 191.
[2]-Chanzo hicho hicho ukurasa 299.
[3]-al-Ikhtiswaas ukurasa 73.
[4]-Ikhtiyaar Maarifatir-Rijaal Shaikhut-Twaaifah ukurasa 38-39-Hadithi ya 79. chapa ya Jaamiatu Mash'had-Iran

yale yaliyopokelewa na al-Haafidh al-Mundhiriy (aliyefariki mwaka 656 Hijiria) kutoka kwa Mtume Mtukufu (SAW) ya kuwa amesema kumwambia Bilal: Ewe Bilal! Nisimulie tendo ambalo una matarajio nalo sana ulilolitenda katika Uislamu, hakika mimi nimesikia milio ya kanda mbili zako mbele yangu peponi.

Akasema: Sikufanya amali ambayo nina matarajio nayo sana isipokuwa ni kwamba hakika mimi sifanyi twahara yoyote katika saa yoyote ya usiku au mchana isipokuwa husali kwa twahara hiyo swala nilizofaradhishiwa kuziswali.

Imepokelewa na Bukhariy na Muslim.[1]

Tunasema: Kwa hakika amepokea hadithi hii Sayyid Mwanairfani Haidar al-Mamuliy (Mungu autukuze utajo wake aliyefariki dunia katika karne ya nane Hijiria) kwa namna nyingine kwani amesema: Imepokelewa katika hadithi sahihi kutoka kwa Mtume (SAW) ya kuwa amesema kumwambia Bilal: Ewe Bilal! Ni kwa kitu gani umenitangulia peponi, kwani sikukanyaga wala kuingia humo na kukanyaga sehemu yoyote (sikuingia peponi kamwe) isipokuwa nilisikia mlio wa mwendo wako mbele yangu? Akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Sikupatwa na hadathi kamwe isipokuwa nilitawadha au kufanya udhu, na wala sikufanya udhu kamwe isipokuwa niliswali rakaa mbili. Mtume wa Mwenyezi Mungu akasema: Kwa vitu viwili hivi (yaani kwa hivi tu) umenitengulie.

Kisha mwanairfani huyo akasema baada ya hadithi hii: Tukafahamu ya kuwa hiyo ilikuwa ni pepo iliyokuwa imewekwa maalumu kwa ajili ya amali hiyo, na Mtume (SAW) kana kwamba alikuwa akimwambia Bilal: Ni kwa

[1]-at-Targhiib wat-Tarhiib juzuu 1 \ 101-102.

kitu gani umeweza kupata nafasi ya kuwa mbele yangu ukinizuia, ni vipi umeweza kupata nafasi hii ya kunitangulia kwenye pepo hii? Na alipomwambia vile, Mtume (SAW) akamwambia kwa vitu viwili hivyo umeipata pepo hii.

Na hakuna faradhi yoyote wala sunna yoyote, wala kitendo chochote cha kheri, wala kuacha jambo la haramu na makruhu isipokuwa mwenye kufanya hivyo hudhaminiwa pepo maalum na neema makhsusi atakazozipata mwenye kuingia kwenye pepo hiyo.[1]

Na Allama at-Tustariy (Mungu autukuze utajo wake) amesema ya kwamba, Mahashawiyya wote - akiwemo al-Jaahidh katika kitabu chake al-Uthmaniyah - : (Hakika Bilal alikuwa ni mtwana wa Abi Bakri na yeye ndiye aliyemuachia huru) na Iskafiy akalipinga hilo - kati ya wahakiki wao -akampinga katika kupingana kwake na kitabu al-Uthmaniyyah, na akasema: Ameachiwa huru na Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na bwana Waaqidiy amepokea hivyo na Ibnu Is'haq na wengineo.[2]

Tunasema: Na lau kama tutakubali ya kuwa Abubakar ndiye ambaye alimuachia huru na kumkomboa, kwa hakika Bilal alikataa na kupinga kumpa baia kwa sababu yeye aliuvaa ukhalifa kama kanzu pamoja na kuelewa kwake vyema kwamba nafasi ya Amiril-Muuminiin Ali bin Abi Twalib (AS) kwenye ukhalifa huo, ni sawa na nafasi ya mpini kwenye jiwe la kusagia. Alivumilia kufukuza kutoka Madina yakiwa ni matokeo na natija ya msimamo wake huu shupavu.

Kwa hakika Wahiid Bahbahaniy amenukuuu kutoka kwa

[1]-Tafsiirul-muhiitil-aadham juzu 3 \ 403.

[2]-Qaamusir-Rijaal cha Allamah Tustariy (Mungu autukuze utajo wake) juzu u2 \393 chapa ya Muassasatun-Nashril-Islaamiy-Qum.

al-Majlisiy wa kwanza, kuwa: Nimeona katika baadhi ya vitabu vya masabibu wetu, kutoka kwa Hishaam bin Saalim, kutoka kwa Swaadiq (AS), kutoka kwa Abil-Bukhturiy, kutoka kwa Abdallah bin Hassan: Hakika Bilal alikataa kumpa baia Abubakar na kwamba Omar alimshika kwenye mifupa yake ya shingo, na akamwambia: Ewe Bilal! Haya ndiyo malipo ya Abubakar kutoka kwako kutokana na kukukomboa wewe? Na hutaki kuja kumpa baia! Akasema: Ikiwa Abu Baker amenikomboa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu basi aniache kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na ikiwa amenikomboa kwa ajili ya jambo lingine tofauti na hilo, basi mimi niko hapa! Ama kuhusiana na kumpa baia: Sikuwa ni mwenye kumpa baia mtu ambaye hakupewa ukhalifa na Mtume (SAW).

Na mtu ambaye amepewa ukhalifa na Mtume (SAW) baia yake iko shingoni mwetu hadi siku ya kiama. Omar akamwambia: Huna baba wewe! Usikae na sisi, ondoka uende zako Sham (Syria)[1].

Na Ibnu Abdul-Barri amepokea habari kuhusina na Abubakar kumkomboa Bilal, na katika habari yake ameeleza kama ifuatavyo: Pindi Mtume (SAW) alipofariki dunia, Bilal alitaka kutoka kuelekea Sham, Abubakar akamwambia: Bali utabakia kwangu. Akasema: Ikiwa ulinikomboa kwa ajili yako basi nizuie nisiende, na ikiwa ulinikomboa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Aliyetakasika, basi niachilie niende kwa Mwenyezi Mungu Aliyetakasika. Abubakar akasema: Nenda, naye akaenda Sham, na

[1]-Taalika ya Wahiid al-Bahbahaniy, kilicho chapishwa katika mfumo wa makala: ukurasa 72 - kutoka kwenye Kaamusir-Rijaal 399-juzuu 2 \. Pia yametajwa na Allamah al-Mamaqaniy (Mungu autukuze utajo wake) katika kitabu Tanqiihul-Mmaqaal: Maadat Bilal bin Ribah juzuu 1\ 182 chapa ya Hajariyyah.

alibakia huko hadi alipofariki dunia.[1]

Na katika Tafsirul-Imam Ali (AS) imepokelewa kwamba, Bilal alinunuliwa na ABubakar kutoka kwa ABi Quhafah kwa ajili ya watumwa wake wawili weusi na akarudi kwa Mtume (SAW). Bilal akawa anamsifu na kumtukuza Ali bin Abi Twalib kuliko alivyomsifu Abu Baker. Mafisadi wakasema: Ewe Bilal! Umekufuru na kuvunja taratibu za ulipaji wa fadhila? Abubakar ni bwana wako ambaye alikununua na kukuacha huru na kukuokoa kutoka kwenye adhabu na akaipatia heshima nafsi yako na mali yako uliyoichuma. Ali bin Abi Twalib hakukufanyia lolote kati ya mambo haya, na wewe unamheshimu Abal-Hassan Ali kwa yale usiyomheshimu nayo Aba Bakar. Hakika huku ni kukufuru neema na kutojua utaratibu wa fadhila.

Bilal akasema: Itanilazimu kumheshimu Ababakar zaidi ya vile ninavyomuheshimu Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW)?

Wakasema: Tunajikinga na Mwenyezi Mungu.

Akasema: Kauli yenu hii inapingana na kauli yenu ya kwanza. Ikiwa haijuzu kwangu kumfadhilisha Ali (AS) kuliko Abubakar kwa sababu Abubakar amenikomboa na kuniacha huru, hivyo hivyo haijuzu kwangu kumfadhilisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) kumliko Abubakar kwa sababu Ababakar amenikomboa na kuniacha huru!

Wakasema: Hawako sawa, hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) ni kiumbe bora zaidi kati ya waja wote wa Mwenyezi Mungu.

Bilal akasema: Na wala hawako sawa pia Abubakar na Ali (AS), hakika Ali ni nafsi ya mbora wa viumbe vya Mwenyezi

[1]-Qaamusir-Rijaal ukurasa juzuu 2\ 399.

Mungu.[1] Hivyo basi, yeye pia ni mbora wa viumbe wa Mwenyezi Mungu baada ya Mtume Wake (SAW) na ni kiumbe chenye kupendwa zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu mtukufu, kutokana na kula kwake ndege pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) pale alipoomba na kusema: Ewe Mwenyezi Mungu! Niletee kiumbe au mtu apendwaye zaidi kwako, naye awe ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu mwenye kufanana na Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa kumfanya kwako nduguye katika dini ya Mwenyezi Mungu. Abubakar hadai yale mnayoyadai nyinyi, kwa sababu yeye anafahamu katika fadhila za Ali msiyoyajua, yaani anafahamu ya kwamba haki ya Ali (AS) kwangu ni kubwa zaidi kuliko haki yake, kwa sababu yeye aliniokoa kutoka kwenye utumwa wa adhabu ambayo lau kama ingeendelea na mimi kuivumilia basi ningekwenda kwenye pepo ya Adni, lakini wakati huohuo Ali (AS) ameniokoa kutoka kwenye utumwa wa adhabu ya milele na hivyo kuniwajibikia kumuamini, kumtawalisha na kumfadhilisha yeye kutokana na kupata neema ya milele.[2]

Na Muhaddith an-Nuuriy amenukuu kutoka kwenye kitabu Uddatud-Daiy ya kwamba, Mtu mmoja alikuja kwa Amiril-Muuminiin (AS) na kusema: Ewe Miril-Muuminiin (AS)! Hakika Bilal hii leo alikuwa akijadiliana na fulani na akawa anakosea katika maneno yake na fulani akifurahi na kumcheka fulani. Amiril-Muuminiin (AS) akasema: Hakika jambo litakiwalo ni kuyairabisha maneno (kuyafafanua) na kuyatathmini ili kuyarekebisha matendo na kuyasawazisha.

[1]-Na hiyo ni kutokana na kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu isemayo:

(Aal-Imraan aya 61)

[2]-Nafsur-Rrahman ukurasa 92 chapa. Hajariyyah.

Irabu humunufaisha nini fulani ikiwa matendo yake ni mabaya? Na ni kitakachomduru Bilal kwa kukosea kwake ikiwa matendo yake ni mema, yaliyoko kwenye njia ilionyooka, yaliyo mazuri na yenye kutengamaa sawa sawa?[1]

Na imepokelewa kuwa pindi Bila alipoletwa kutoka nchini Uhabeshi hadi kwa Mtume (SAW), alimuimbia shairi Mtume kwa lugha ya Kihabeshi lisemalo:

Areh bereh konkereh – karaakirii mandareh

Akamwambia Hassan: Bainisha maana yake kwa Kiarabu na Hassan akasoma shairi na kusema:

Tabia njema zinapotajwa na kuzungumziwa kwetu, hakika wewe hupigiwa mfano kati yetu.[2]

Na Shekh Swaduuq (Mungu autukuze utajo wake) amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) alikuwa na waadhini wawili mmoja wao ni Bilal na mwingine ni Ibnu Ummi Maktuum, na Ibnu Ummi Maktuum alikuwa ni kipofu, na alikuwa akiadhini kabla ya asubuhi. Na Bilal alikuwa akiadhini baada ya asubuhi, Mtume (SAW) akasema: "Hakika Ibnu Ummi Makhtuum anaadhini usiku basi mtakaposikia adhana yake kuleni na kunywa hadi msikie adhana ya Bilal". Na Masunni wakaigeuza hadithi hii na kuitoa kwenye muelekeo wake na wakasema: Hakika Mtume (SAW) alisema: Hakika Bilal ataadhini usiku na mtakaposikia adhana yake kuleni na kunywa hadi mtakaposikia adhana ya Ummu Maktuum.

Na imepokelewa kwamba: Alipofarikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), Bilal alikataa kuadhini na akasema: Siadhini kwa ajili ya mtu yeyote baada ya Mtume

[1]-Nafsur-Rahmaan ukurasa 92 chapa. Hajariyyah.

[2]-al-Kushkuli cha Bahaiy (Mungu autukuze utajo wake) juzuu 2 \ 34 chapa ya muassasatul-iilamiy- Bairut, Lebanon.

wa Mwenyezi Mungu (SAW), na kwamba Fatuma (AS) siku moja alisema:Hakika mimi ninapenda kusikia sauti ya muadhini wa baba yangu (SAW) akiadhini na habari hizo zikamfikia Bilal naye akaanza kuadhini,[1] na wakati aliposema: 'Allahu Akbar, Allahu Akbar,' Fatuma akamkumbuka baba yake (SAW) na siku alizokuwa hai na hapo hakuweza kujizuia na kulia. Alipofikia kwenye kauli isemayo: 'Ash'hadu anna Muhammadar-Rasuulullah' alipiga ukulele mkubwa na kuanguka kifudifudi na kuzimia. Watu wakamwambia Bilal: Ewe Bilal! Acha kuadhini, hakika binti ya Mtume (SAW) ameaga dunia. Walidhania kuwa amefariki na Bilal akakatiza adhana yake bila ya kuikamilisha. Fatuma (AS) akazindukana na akamuomba aikamilishe adhana hiyo lakini hakufanya hivyo. Bilal akamwambia Fatuma: Ewe mbora wa wanawake! Hakika mimi ninaogopa na kukuchelea kuhusiana na yale unayoyawaza moyoni pindi unakaposikia nikiadhini. Kwa hivyo Fatuma akamsamehe na kumkubalia asikamilishe adhana hiyo.[2]

Na Abu Baswiir amesema kuhusiana na mmoja wao (AS) ya kwamba: Hakika Bilal alikuwa ni mja mwema, na akasema: Sitamuadhinia yeyote baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na kuanzia siku hiyo ibara isemayo 'hayya ala khairil-amal' ikaachwa na kutolewa (kwenye adhana).[3]

[1]-Huenda tukio hili ni kabla ya kufukuzwa kwenda Sham na omar kwa kuzingatia yaliyo tangulia.

[2]-al-Faqiihu juzuu 1 \297 hadithi ya 906 na 907 chapa ya Muassasatun-Nashril-Islaamiy Qum.

[3]-al-Faqiihu juzuu 1 \ hadithi ya 283 na hadithi ya 872. Imepokelewa na kuelezwa kwenye hashia ya hadithi hii pale aliposema (AS): 'Kuanzia hapo au siku hiyo ikaachwa', yaani kuanzia siku yalip sikika maneno hayo kutoka kwa Bilal kwa kudai kwao ya kuwa watu ikiwa wataitakidi ubora wa swala hawatatilia hima suala la jihadi na kuacha ibara isemayo 'hayya alaa khairil-amal' kwa ajili ya maslahi na kwa ajili ya uzuri waliouona wao na kufanya ijtihadi mbele ya dalili na nassi ya wazi kabisa, na badala yake wakaweka katika adhana ya asubuhi kauli isemayo, 'aswalaat khairum-minan-naum', yaani sala ni bora kuliko usingizi.

Na baada ya haya, Bilal aliye maarufu pia katika baadhi ya vitabu kwa jina la Bilal bin Hamaamah al-Habashiy alifariki dunia akiwa katika mji wa Damascus ambao katika zama zetu hizi ni mji mkuu wa Syria mwaka wa 18 au 20 Hijiria, akiwa na umri wa miaka sitini na kitu hivi. Ibnu Jubairi amesema katika msafara wake ya kwamba kuomba dua katika sehemu hii tukufu (yaani mahala alipozikiwa Bilal na watu wengine waliozikwa pembezoni mwake) hupelekea dua na maombi kujibiwa, na hilo limethibiti mara nyingi sana na kujaribiwa na mawalii na watu wa kheri wenye kutabarruku kwa kuwazuru watu hawa.[1]

[1]-Rihlatu Ibnu Jubairi ukurasa 251-Daarus-Swaadir Bairut mwaka 1964 A.D.

USAWA KATIKA UTOAJI WA AMIRIL-MUUMINIIN (AS) KATI YA MWEUPE, MWEUSI NA MWEKUNDU

Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mwenyezi Mungu autukuze utajo wake aliyefariki mwaka 328 hijira) amepokea kutoka kwa mashahibu wetu kadhaa, kutoka kwa Sahli bin Ziyaad, kutoka kwa Yaaqub bin Yaziid, kutoka kwa Muhammad bin Jaafar al-Aqabiy kwamba: Amiril-Muuminiin alitoa khutba na kumhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifia kisha akasema: Enyi watu! Hakika Adam hakuzaa mtumwa wala mjakazi na kwamba watu wote wako huru lakini Mwenyezi Mungu amewafanya baadhi yenu kuwasaidia na kuwatumikia wengine. Kwa hivyo mwenye kuwa na balaa na akasubiri na kuvumilia katika kheri [1] basi asimsimbulie Mwenyezi Mungu kwa mali hiyo.[2] Fahamuni ya kuwa nimefikiwa na fungu fulani[3] na sisi sote tuko sawa katika fungu hilo kati ya mweusi na mwekundu. Mar'wan akamwambia Twalha na Zubairi: Hakumkusudia kwa haya mtu mwingine isipokuwa nyinyi wawili. Akasema: Akampatia kila mmoja dinari tatu na akampatia mtu wa Kianswari dinari tatu na baadaye akaja kijana (mtumwa) mweusi akampatia dinari tatu.

Maanswari wakasema: Ewe Amiril-Muuminiin! Huyu ni mtumwa (ghulam) niliyemuachia huru jana unanifanya mimi na yeye kuwa sawa?!

Amiril-Muuminiin akasema: Hakika mimi nimeangalia katika kitabu cha Mwenyezi Mungu na sikupata kwamba

[1]- Yaani mwenye neema ya mali na mfano wake akasubiri na kuvumilia hutumia katika njia ya Mwenyezi Mungu.

[2]-Yaani yeyote asimsimbulie Mwenyezi Mungu kwa yale anayompa bali atoe ili ajichukulie ujira wake katika akhera.

[3]-Yaani nimefikiwa na fungu la mali au pesa.

mtoto wa Ismaili ana fadhila juu ya mtoto wa Is'haq.[1]

Na imepokelewa pia kwa sanadi yenye kuzingatiwa kutoka kwa Ali bin Ibrahiim kutoka kwa baba yake Ibrahiim bin Haashim, kutoka kwa Ibnu Abi Umairi, kutoka kwa Abdur-Rahmaan bin al-Hajjaj, kutoka kwa Muhammad bin Muslim, kutoka kwa Abi Abdillah (AS) kwamba: Pindi Ali (AS) alipochukua uongozi na utawala alipanda juu ya mimbari akamhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifia kisha akasema: Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, hakika mimi sipunguzi chochote katika fungu lenu hata kiwango cha dirhamu moja kwa muda wote nitakaokuwa na mitende katika mji wa Yathrib (Madina). Basi hebu nafsi zenu zikuswadikisheni, je, mwaniona nikijizuilia mimi mwenyewe nafsi yangu na kukupeni nyinyi?

Akasema: Aqiil akasimama na kwenda kwake (Karrama Allahu wajhahu) na akamwambia: Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, hivi kweli unanifanya mimi na mtu mweusi wa Madinah kuwa sawa?!

Akasema: Kaa chini. Je, hakukuwa na yeyote mwingine wa kuzungumza tofauti na wewe. Kwani una ubora gain juu yake isipokuwa kutangulia katika imani (kwenye dini) na ucha-Mungu?[2]

Tunasema: Kuhusu kauli yake isemayo (Ar'za'ukum) yaani (si) mwenye kukupunguzieni, na Faiu ni ghanima yaani mali na ngawira. [3] Na al-adhqu: ni mtende na Yathriba ni jina la mji wa Mtume (SAW), na makusudio ya jumla hii ni kuwa: Hakika mimi sitakupunguzieni wala kukupunjeni katika ghanima zenu na mali yenu na kodi yenu kwa muda wote nitakaobakia kuwa na mitende katika mji wa Madinatul Munawwarah. Basi zirejeleeni nafsi zenu, na mfanyieni uadilifu na insafu khalifa wenu na ziacheni

[1]-Raudhatul-Kafiy ukurasa 57 h 26.

[2]-Raudhatul-Kafiy-ukurasa 158-hadithi ya 204.

[3]-Ni aina moja wapo ya kodi.

nafsi zenu ziseme na kukwambieni ukweli kuhusu hilo.

Ni kutokana na hayo ndio maana wakati Aqiil aliposimama na kumwendea nduguye na kumwambia: Utanifanya mimi na yule mtu mweusi kuwa sawa katika kipato pamoja na ukaribu au ujamaa uliopo kati yangu na wewe na ukaribu wangu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), Amiril-Muuminiin (AS) akamwambia ya kwamba, ubora si wa nasaba ili ukufanye uweze kujifakharisha nao kwa wengine. Wala ubora si wa rangi bali ubora ni kwa kutangulia kwenye Uislamu na kutekeleza mafundisho yake.

Uadilifu huu wa Imam Ali (AS) uko wapi (ni wa juu mno) ukiulinganisha na ule wa watawala waliomtangulia, kama itasemekana kuwa walikuwa ni waadilifu. Kwani imethibiti katika historia ya kwamba, Khalifa wa Pili alikuwa akiwafadhilisha watu fulani katika utoaji na kipato na akiwafadhilisha Muhajirina kuliko Maanswari na alikuwa akiwafadhilisha Waarabu kuliko Waajemi (wasio kuwa Waarabu) kama vile Wafursi, Waafrika na wengineo?[1]

Ama Khalifa wa Tatu alikuwa akiwafadhilisha watu wa karibu na jamaa zake wa Bani Umayyah kuliko watu wote. Hilo ni jambo lililo wazi kabisa. Hali hiyo ilimpelekea hadi kumpatia mtoto wa ami yake Marwaan binil-Hakam, dinari laki moja na mbuzi watano kutoka ardhi ya Afrika[2] wakati ilipotekwa na Waislaamu.[3]

[1]-Angalia: Sharhu Tajriidul-Iitikad cha Allamah Al-Qawshajiy (aliye fariki mwaka 879 Hijiria) ukurasa 374.

[2]-Angalia:Dalaailus-Swidq cha Allamah Mudhwaffar-juzuu 3\267-akinukuu kutoka kwenye as-Siiratul-Halabiyyah juzuu 2 \ 82.

[3]-Kwa ajili ya maelezo zaidi angalia kitabu al-Kaamilu fit-Taariikh cha Ibnu Athiir juzuu 3\88-91. Chapa ya Daru Swaadir Beirut mwaka 1965 A.D na vinginevyo.

KUOKOLEWA KWA MWANAMKE WA KIAFRIKA NA AMIRIL-MUMINIIN (AS) KUTOKANA NA ADHABU YA KUPOPOLEWA KWA MAWE

Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mungu autukuze utajo wake) amepokea kutoka kwa Muhammad bin Yahya, kutoka kwa Muhammad bin Hussein, kutoka kwa Hassan bin Ali, kutoka kwa Zakaria al-Mumin, kutoka kwa Ibnu Maskaan, kutoka kwa baadhi ya Maswahibu wetu, kutoka kwa Abi Abdallahi (AS) kuwa amesema: Mtu mmoja alikuja na kumleta mkewe kwa Omar na akasema: Mke wangu huyu ni mweusi na mimi ni mweusi naye amezaa mtoto mweupe. Omar akawambia waliokuwa wamehudhuria kwake: Mnasemaje kuhusiana na kadhia hii?

Wakasema: Tuonavyo ni kuwa mpopoe kwa mawe hakika yeye ni mweusi na mumewe ni mweusi na mtoto wake ni mweupe. Akasema: Mara Amirul-Muuminiin (AS) akaja hali ya kuwa mwanamke huyo akipelekwa kupopolewe mawe, na akauliza: Ni lipi lililotokea? Wakamsimulia naye akamuuliza yule bwana mweusi, je, unamtuhumu mkeo? Akasema: Hapana. Akauliza: Je, ulimuingia hali ya kuwa ni mwenye hedhi? Akasema: Kwa hakika aliniambia hivyo usiku mmoja kuwa ni mwenye hedhi nikadhania ya kuwa anaogopa baridi[1] nami nikamuingilia. Amiril-Muuminiin akamuuliza yule mwanamke: Je, alikuingia hali ya kuwa uko kwenye hedhi? Akasema: Ndio, muulize kwa hakika nilimtatiza[2] na kumkatalia. Amiril-Muuminiin akasema:

[1]-Yaani kwa kuogopa kuoga katika kipindi cha baridi akasema ya kuwa yuko kwenye hedhi.

[2]-Tahriij:Ni kukataa na kupinga yaani sikumfanyia wepesi.

Basi nendeni zenu hakika ni mtoto wenu, bali damu iliizidi mbegu ya uzazi kwa hivyo mtoto akatoka akiwa mweupe, na ikiwa atataharuki na kukua atakuwa mweusi. Pindi alipofikia baleghe[1] akageuka na kuwa mweusi.[2]

Tunasema: Kutokana na hadithi hii tunafaidika na mambo yafuatayo:

1-Hakika lau kama kweli maswahaba wote wa Mtume (SAW) wangekuwa ni kama nyota basi baadhi yao wasingemhukumu mwanamke huyu masikini kwa hukumu hii ngumu na ya kiovu kwa sababu ni kuhukumu bila ya elimu, muongozo wala yenye kufuata Kitabu chenye kutoa nuru na kitakatifu cha Mwenyezi Mungu. Je, Mwenyezi Mungu amewapa idhini ya kutoa hukumu kama hizo au wanamzulia tu mambo yasiyohusiana Naye?

2- Inathibitisha kusihi kwa hadithi iliyopokelewa kutoka kwa Mtume Mtukufu (SAW) isemayo ya kwamba Ali (AS) ndiye mwenye kuhukumu vyema kati ya Umma au mjuzu zaidi wa hukumu katika Umma.[3]

3- Inathibitisha imani ya wote wawili kati ya mume na mke kuyaelekea mafundisho ya Mwenmyezi Mungu Aliyetakasika na kujifungamanisha nayo, kwani mwanaume alikuwa akifahamu ya kwamba kumkaribia au kumuingilia mkewe wakati akiwa kwenye hedhi ni haramu lakini alidhania ya kwamba mwanamke huyo anajizuilia na kukataa kwa kuogopa kuoga na kwenda bafuni kutokana na baridi. Naye mkewe hakujilegeza kwake. Ni kutokana na hayo ndio maana Amiril-Muuminiin (AS) akatoa hukumu

[1]-Yaani alipofikia hatua ya kubaleghe akarudi kwenye asili yake na mwili wake kuwa mweusi.
[2]-Furuu'ul-kafiy juzuu 1 \-kitabun-nikaah-baab Nawaadir-h 46.
[3]- Angalia:Fadhaailul-Khamsah min Swihaahis-Sittah-juzuu2 \ 262.

ya kuachiwa huru mwanamke huyo na kutoruhusu auawe na hivyo kumuokoa yule mwanamke kutokana na utekelezaji wa hukumu ile ya kiovu na kidhalimu.

4-Sentensi isemayo: 'Na pindi alipofikia baleghe akawa mweusi', kidhahiri ni kuwa ni katika maneno ya Imam Swaadiq (AS).

KUVUTIWA KWA FATUMA ZAHRAA (AS) NA BAADHI YA MILA NA ADA ZA KIARFIKA

Jambo linapoaswa kufahamika vyema ni kuwa, ada, mila au desturi ni kukaririka kwa kitendo fulani kwa mtindo na mbinu moja kwa nanma ambayo hatimaye kitendo hicho hutendwa bila ya kufanyika jitihada kubwa wala usumbufu unaochukiza. Na mila ni ya aina mbili. Aina ya kwanza ni ile yenye kusifiwa na nyingine ni yenye kukemewa. Mila yenye kusifiwa kati ya ada na desturi hizo ni ada zile zilizoletwa na sheria au kupitishwa na sheria, na zilizo tofauti na hizo ni zenye kukemewa.

Miongoni mwa mila na ada zilizokubaliwa na kupitishwa na sheria takasifu ni kuhusiana na Naash, nacho ni kitanda ambacho huwekwa juu yake maiti na kubebwa hadi kaburini. Hili ni jambo lililokuwa likitekelezwa na kuenea miongoni mwa Waafrika. Kwani Muhammad bin Muhammad binil-Ash'ath mmoja kati ya wanazuoni wa karne ya nne amepokea hadithi na kusema: Nimesimuliwa na Musa bin Ismaili, amesema tumesimuliwa na baba yangu, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa jaddi yake (babu yake) Jaafar bin Muhammad kutoka kwa baba yake, kutoka kwa jaddi yake Ali bin Hussein, kutoka kwa baba yake kutoka kwa Ali bin Abi Twalib (AS): Hakika Fatuma bint wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) pindi alipofariki Mtume (SAW) alipatwa na ugonjwa wa macho[1] kutokana na huzuni juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW), na kuishi baada yake kwa muda wa siku sabini. Kwa hakika

[1]-as-Sabalu: ni ugonjwa wa macho, al-Kamadu:ni huzuni isiyokoma. Na huenda ni kutokana na kumlilia sana baba yake mtukufu (SAW) kwa msiba uliomfika.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) alikuwa amemwambia ya kwamba: Mtu wa kwanza kabisa kuungana na mimi kati ya Ahli zangu ni wewe ewe Fatuma.

Fatuma akamwambia (As'maau binti Umaisi): Nifanye nini hali ya kuwa nimekuwa mifupa mitupu na ngozi imekaukia juu ya mifupa?

As'maau akasema: Niwe fidia yako, mimi nitakutengenezea kitu ambacho kwacho hutofautishwi mwanamke na mwanamume, pindi utakapobebwa juu ya kitanda (naashi) chako cha mauti. Nilikiona katika ardhi ya Uhabeshi wakimuweka mwanamke juu yake (Naash-kitanda cha maiti au jeneza). Akasema: Ninapenda unitengenezee kitu hicho. Naye akatengeneza naash (kitanda). Kwa hivyo kitanda cha kwanza (naash) kilichotengenezwa katika Uislamu ni jeneza la Fatuma (AS) binti wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW).[1]

Tunasema: Allamah al-Majlisiy (Mungu autukuze utajo wake amenukuu hadithi hii katika kitabu Biharul-Anwaar juzuu 43 ukurasa 189 na ikanukuliwa na Muhaddithi an-Nuuriy (Mungu autukuze utajo wake) katika kitabu al-Mustadrak juzuu 1 \ ukurasa 129.

Lakini Abu Ali Muhammad bin Ahmad au Hassan bin Ali al-Fattal an-Naisaburiy (Mungu autukuze utajo wake), mmoja kati ya wanazuoni wa karne ya sita Hijiria amepokea na kusimulia ya kwamba, Sayyidah Fatumah (AS) alimwambia Amiril-Muuminiin (AS) pindi alipopewa habari ya kifo chake na nafsi yake: Ninakuusia ewe mtoto wa ami unitengenezee naash (jeneza). Kwa hakika nimewaona malaika wakinionyesha picha yake. Imam Ali akamwambia Fatuma: Basi nifahamishe kilivyo.

[1]-al-Jaafariyyat, babu Ibtidaaun-Naash kaifa kaana. Ukurasa 337.

Na yeye akamsifia kilivyo naye kumtengenezea. Kwa hivyo naash au jeneza la kwanza lililo tengenezwa hapa ardhini ni jeneza lile na hakuna yeyote aliyewahi kuona naasha yoyote kabla ya hiyo na hakuna yeyote aliyewahi kutengeneza mfano wake.[1]

Na ni jambo lisilofichika kuipa kipaumbele na nguvu kauli ya kwanza kuliko ya pili kutokana na mlolongo wa utafiti wa kielimu. Hiyo ni kutokana na chanzo cha kwanza kuwa ni cha kale zaidi kinyume na cha pili. Kisha kukitegemeza kwake au kukipa sanadi pamoja na umbali wa madhumuni ya kile cha pili kwa sababu yaliyomtangulia Sayyidah Fatuma (AS) ni sawa au ni kama yale ya Sayyidah Maryam (AS) kwani ni yenye kumstahilia yeye pia. Zingatia.

[1]-Raudhatul-Waaidhiin, Majlis fii dhikri Fatwimah (a.s) ukurasa 130.

ADABU NA TABIA ZA MAIMAMU WA AHLUL-BAITI (AS) KWA WAAFRIKA

Al-Hurril-Aamiliy (Mungu autukuze utajo wake) (aliyefariki dunia mwaka 1104 hijira), amepokea kwa sanadi yake hadi kwa Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mungu autukuze utajo wake) kutoka kwa maswahibu wetu kadhaa kutoka kwa Ahmad bin Muhammad kutoka kwa Abdallah bin Swalti kutoka kwa mtu mmoja kati ya watu wa Balkh[1] kwamba: Nilikuwa pamoja na Ridhaa (AS) katika safari yake ya kuelekea Khorasani.[2] Siku moja akawaita watu kwenye meza ya chakula na kuwakusanya watumwa wake kwenye meza hiyo kati ya watu weusi na wengineo.

Nikasema: Unaonaje lau kama utawatengea watu hawa meza yao?

Imam (AS) akasema: Nyamaza[3], hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mmoja na mama ni mmoja na baba ni mmoja na malipo ni kutokana na matendo na amali.[4]

Tunasema: Hukumu ya mafaqihi wetu kwa mujibu wa hadithi hii na mfano wake ni kuwa, ni makruhu kutenga meza ya chakula kwa ajili ya watu ambao ni tofauti na sisi katika rangi ya ngozi. Ni kwa sababu hii, ndipo Allamah Shekh Muhammad bin Hassan al-Hurril-Amiliy (Mungu autukuze utajo wake (aliyefariki mwaka 1104 Hijiria) akaweka mlango mahususi katika kitabu chake, Wasaailush-Shia aliouita 'karaha ya kutenga meza ya chakula kwa ajili ya watu weusi, wahudumu na mabwana katika faragha.'[5]

[1]-Balakha: ulikuwa mji wenye hadhi kubwa katika zama za kale na katika zama za kati. Na hivi leo uko nchini Afghanistan.

[2]-Khorasani: Ni neno lililounganishwa kutokana na neno (Khora) yaani Jua na (Saan) yaani mashariki. Ni eneo ambalo zinaligawana Iran, Afghanistan na Turkmanistan.

[3]-Yaani nyamaza.

[4]-Wasaailush-Shia-juzuu 16- Kitaabul- At'imah wal-Ashribah, babu 13 min abwaab Aadabil-Maaidah h1 ukurasa 423.

[5]-Wasaailush-Shia juzuu 16 \ 423- Kitaabul-At'imah wal-Ashribah, baabu 13 min abwaab Aadabuil-Maaidah h 1.

KITENDO CHA MAIMAMU (AS) CHA KUWATAKA USHAURI WAAFRIKA

Kwa hakika Qur'an Tukufu imesisitiza juu ya kushauriana katika mambo ambayo hayana hukumu ya kisheria moja kwa moja isipokuwa kujuzu na kuwa mubaha utekelezaji wake kwa ujumla kama vile mambo ya kidunia. Ni kwa sababu hii ndio maana Mwenyezi Mungu akasema: 'Na mambo yao ni mashauriano kati yao'[1], yaani mambo ya dunia na maisha yao na wala sio mambo ya Mwenyezi Mungu kama vile ukhalifa na uimamu.[2]

Kuhusiana na suala hili, pamoja na kuwa tofauti kati ya mambo ya Mwenyezi Mungu na mambo yanayowahusu wanadamu, iko wazi, lakini yaliwachanganya baadhi ya watu na kuwapelekea kupotea na wakati huohuo kuwapoteza wengine. Ala kulli hali, kwa hakika Maimamu wetu walituwekea mipaka ya mashauriano na mtu ambaye inapaswa kumtaka ushauri na nasaha.

Msimuliaji Mtukufu Thiqah Abu Jaafar Ahmad bin Muhammad bin Khaalid al-Barqiy (Mugnu autukuze utajo wake aliyefariki dunia mwaka 274 Hijiria) amepokea hadithi kutoka kwa Ahmad bin Nuh, kutoka kwa Shuaib an-Naisaburiy, kutoka kwa Ubaidullah bin Abdallah ad-Dahqaan, kutoka kwa Ahmad bin Aaid, kutoka kwa al-Halabiy, kutoka kwa Abi Abdillah (AS) kwamba: Hakika mashauriano hayafanyiki isipokuwa kwa kuzingatia mipaka yake. Basi mwenye kuyaelewa mashauriano azingatie mipaka yake, la sivyo madhara yake yatakuwa ni mengi zaidi

[1]-Suratush-Shuraa aya 38.
[2]-Kwa sababu ni uongozi wa ujumla katika dini na dunia na ulikuwa ni lutfi na ukawa ni wajibu kutoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu.

kwa mwenye kutaka ushauri kuliko manufa yake kwake. Sharti la kwanza ni kuwa: Mtu umtakae ushauri awe ni mwenye akili na busara, la pili, awe huru na mwenye kushikamana na mafunzo ya dini, la tatu, awe ni rafiki na ndugu na sharti la nne umfahamishe siri zako, hivyo elimu yake na kufahamu kwake siri zako kuwe ni kama vile unavyojifahamu wewe mwenyewe, kisha ayafiche hayo na kuyafanya kuwa ni siri. Akiwa ni mtu mwenye akili na busara utanufaika na ushauri wake, na akiwa huru na mwenye kushikamana na dini atajitahidi ili akupe nasaha, na akiwa ni rafiki mpenzi na ndugu atazificha siri zako pale utakapomfahamisha siri hizo, na ukimfahamisha na kumfichulia siri zako, na akazifahamu kama vile unavyozifahamu wewe mwenyewe, hapo mashauriano yatakuwa yametimia na nasaha kukamilika.[1]

Tunasema: Baada ya kupitia riwaya hii tukufu, njoo pamoja nami ewe msomaji mtukufu ili tuone sira na mwenendo wa Maimamu Maasumu (AS) wakiwa pamoja na watumwa wao kati ya ndugu wa Kiafrika.

Kwa hakika al-Barqiy amepokea pia kutoka kwa maswahibu kadhaa, kutoka kwa Ali bin Asbaat, kutoka kwa Hassan bin al-Jahm, kwamba: Tulikuwa kwa Abil-Hassan Ar-Ridhaa (AS), na tukamtaja na kumkumbuka baba yake (AS).[2]

Akasema: Akili yake ilikuwa hailingani na kupimwa na akili ya mtu yeyote, na wakati mwingine akimtaka ushauri mtu mweusi pamoja na weusi wake. Akaulizwa: Je, Unamtaka ushauri mtu kama huyu?!

[1]-Al-Mahaasin cha al-Barqiy juzuu 2 \ h 28 ukurasa 438 -438-439 Baabul-Istisharah.
[2]-Akimuashira Imam Musa al-Kaadhim (AS).

Akasema: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu huenda akafungua busara kupitia katika ulimi wake. Akasema: Na wakati mwingine huenda walikuwa wakimshauri kwa jambo fulani, na kulitekeleza au kufuata ushauri huo katika mashamba yake na mabustani yake.[1]

Tunasema: Hadithi hii na iliyotangulia inatubainishia wazi ya kwamba, watumwa ambao walikuwa kwa Maimamu wetu (AS) walikuwa ni sawa na watu waliokuwa huru, bali ni uhuru gani ulio bora zaidi kuliko kuishi mtu chini ya uangalizi wa Imamu wake ambaye amefaradhishiwa utiifu, dhihirisho la rehma ya Mwenyezi Mungu na usaidizi wa Mola mlezi? Hii ni kwa upande mmoja.

Na pili: Kuheshimu maoni ya watu wengine na kuyatekeleza au kuyaanyia kazi wakati yanapokuwa ni ya haki hata kama yatatoka kwa mtu ambaye ni duni kuliko mwenye kuyatumia, ni jambo zuri na hii ni tabia nzuri na ya kuvutia iliyoonyeshwa na Maimamu wetu Watukufu (AS) ambao kamwe hawawezi kulinganishwa na kupimwa na yeyote katika Umma huu.

Pamoja na isma na elimu yao ya kuyafahamu vyema mambo yaliyo ya sawa, tunakuta kwamba walikuwa wakiwataka ushauri watu wengine ili kupandikiza hali ya uaminifu na thiqah katika nafsi zao na ili liwe ni somo kwa watu wengine ya kwamba, hakuna uhusiano wowote unaopaswa kuwekwa kati ya rangi ya ngozi na imani, akili na fikra za mtu. Mweupe si mwenye akili zaidi kumliko mweusi wala kinyume chake na vilevile imani na mambo mengine ya ukamilifu. Kwa hivyo watu wote wameumbwa kutokana na nafsi moja na uhakika wa aina ya pekee.

[1]-al-Mahaasin cha al-Barqiy juzuu 2 \ h 23 ukurasa 437 Babul-Istisharah.

Amesema Mwenyezi Mungu mtukufu katika Kitabu chake chenye hekima:"Enyi watu mcheni Mola wenu (muogopeni) ambaye amekuumbeni kutokana na nafsi moja).[1]

[1]-Suuratun-Nisaai aya 1.

UJITOLEAJI MUHANGA WA WAAFRIKA ROHO ZAO KWA AJILI YA KUTETEA HESHIMA YA AHLUL-BAIT (AS)

Ni watu wachache sana wanaofahamu vyema heshima ya Ahlul-Baitil-Ismah na haki zao kwa viumbe wote na wasijitolee nafsi zao wakati wa dharura kwa ajili ya kuwatetea watukufu (AS). Utakuta kwamba, baadhi ya wale ambao walizitakasa nafsi zao kwa ajili yao (AS) na wakatoa kila kilicho na thamani kwao kwa ajili yao ikiwa ni kama alama na kigezo kwa ajili ya vizazi vijavyo. Na hapa tutataja baadhi ya wale waliotoka kwenye nchi za Kiafrika na kuzielekeza nyuso zao upande wa Ahlul-bait (AS) kutokana na na mapenzi na kujitolea kwao kwa ajili yao.

FEDHAH MNUBI WA AFRIKA

Na kabla ya kumzungumzia Sayyidah Fedhwah, Mnubi ambaye alikuwa ni mjakazi wa Fatimah Zahraa (AS), inabidi kwanza tuashirie kidogo kuhusiana na ardhi ya Unubi kwa sababu tutaitaja hapo baadaye katika sehemu kadhaa na hasa tutakapozungumzia maswahibu wa Imam wa Zama anayesubiriwa, Mwenyezi Mungu aharakishe kudhihiri kwake.

Kwa hivyo basi, Nubah ni eneo katika Afrika linalotanda kwenye Mto Nile kati ya Aswaan na Dankalah huko Sudan, na linagawanyika semu mbili, Nuubah ya Chini, nayo ni sehemu au eneo lililoko Misri kati ya As'waan na bonde la Hulafai, na Nuubah ya Juu, nalo ni eneo lililoko Sudan. Uislamu uliingia katika eneo hilo katika karne ya kwanza tangu kuhajiri kwa Mtume (SAW).

Na Wanubi wanasifaka kwa sifa nyingi nzuri na za aina yake nazo zinathibitisha kuendelea kuwepo kwa maumbile salama ambayo watu wa kabila hili waliumbwa nayo. Tunaziona sifa hizi zikiwa zimekusanyika katika baadhi ya makabila ya watu hao na pia kutawanyika kwa watu wengine, nazo ni kama ifuatavyo:

1- Wao ni watu wa amani hawapendi kumfanyia mtu uchokozi na uadui isipokuwa katika kujilinda na kutetea nafsi zao.

2- Kukinaika na kidogo wanachokipata na kutohuzunika kupita kiasi pindi yanapotokea na kuwapata matukio yasiyo ya kawaida na mabalaa na njaa.

3- Ushujaa na kujitokeza katika kazi ya jeshi au uaskari. Kama ambavyo wao wanasifika kwa maumbo makubwa na afya njema.

4- Kuheshimu mila, ada na tamaduni za jamii nyingine.

Kuhusiana na suala hilo, tunaona kwamba kuna makabila mengine mengi yasiyo kuwa ya Kinubi ambayo yamekuwa yakiishi pamoja nao tangu zama za kale bila matatizo yoyote.

5- Kuwa waaminifu na wenye ikhlasi katika utekelezaji wa kazi na majukumu yao.

6- Wao huitikia viathiri vya kiutamaduni na kubadilika kuelekea kwenye hali iliyo bora zaidi pindi wanapolifahamu hilo. Na kauli hii inasisitizwa na kutiliwa mkazo na kufutika pamoja na kutoweka kwa ada na mila nyingi potovu na zenye kukemewa pale tu ulipoenea Uislamu katika miji hiyo.[1]

Kwa vyovyote vile, Fedhwah Mnubi[2] alikuwa kwenye daraja fulani la ukamilifu na upevu wa kifikra na kiakili, vitu vilivyomuandaa na kumfanya awe ni mwenye kuwapenda Ahlul-Bait (AS). Aliidhalilisha nafsi yake kwa ajili ya kuwatumikia huku akitarajia kunufaika na elimu yao na pia kufufuliwa nao siku ya kiama akiwa katika daraja la juu kabisa.

Kwa mfano katika kitabu al-Iswaabah cha Ibnu Hajar al-Askalaniy (aliyefariki mwaka 852 Hijiria) ametsema kwamba imepokelewa kutoka kwa Swaadiq (AS) kutoka kwa baba zake kutoka kwa Ali (AS) kwamba: Hakika

[1]-Kwa ajili ya kupata maelezo zaidi, angalia takriri ambayo imekuja kuhusiana na milima ya Unubi katika jarida la al-Aalam-toleo namba 339, la mwaka 1990 ukurasa32.

[2]-Imeelezwa na kutajwa kwenye kitabu (Mashaariq anwaarul-yaqiin ukurasa 80) ya kwamba Fedhwa ni binti wa mfalme wa India na huenda kauli hii ikawa mbali na ukweli, kwa sababu katika zama zile India ilikuwa haija angukia mikononi mwa waislaam na hatukufahamu ya kuwa iliangukia mikononi mwa watu wengine tofauti na waislaam kisha binti wa mfalme akamuuza kwa waislaam ili awe mhudumu hapo baadae.

Mtume wa Mwenyezi Mungu alimuwekea binti yake Fatima mhudumu mjakazi aliyekuwa akiitwa Fedhwah Mnubi, na alikuwa akimsaidia kazi au akigawana naye kazi nusu kwa nusu, na Mtume (SAW) akamfundisha dua atakayoitumia kuomba. Fatima akamwambia Fedhwah: Je, utakuwa ukikanda unga au kuoka mikate? Akasema: Bali nitakuwa nikikanda unga ewe sayyidah wangu na kukusanya kuni. Basi akatoka na kukusanya kuni. Akiwa na fungu au mzigo wa kuni alitaka kuubeba lakini akashindwa basi akaomba kwa ile dua ambayo alifunzwa na Mtume (SAW) nayo ni kama ifuatavyo: 'Ewe uliye mmoja asiyekuwa na mfano! Unamfisha kila mmoja na wewe ukiwa juu ya arshi yako mmoja, asiyesinzia wala kulala.' Mara akaja bedui mmoja kana kwamba anatoka kwenye kabila la Azdi Shanuuah na kubeba mzigo ule wa kuni hadi kwenye mlango wa Fatimah (AS).[1]

Na kwa hakika Fedhwah Mnubi alifikia kwenye ukamilifu na kujihusisha na Qur'an tukufu kwani alifikia hatua ya kwamba alikuwa hazungumzi isipokuwa kwa Qur'an. Kwa mfano imepokelewa kutoka kwa Abil-Qaasim al-Qushairiy (aliyefariki dunia mwaka 465 Hijiria) kwamba: Baadhi yao walisema: Niliachwa na msafara katika vijiji vya mbali mara nikamkuta mwanamke, nikamuuliza: Wewe ni nani? Akasema: "Na sema: Salaamu mtafahamu."[2] Basi nikamsalimia, na nikasema: Unafanya nini hapa? Akasema: "Na mwenye kuongozwa na Mwenyezi Mungu hakuna wa kompoteza."[3] Nikasema: Je, wewe ni katika majini au watu?

[1]-Al-Iswaabah-juzuu 4 \ 387.

[2]-Surat Zukhruf aya 89.

[3]-Hatukupata aya katika Qur'an kwa lafdhi hii na aya iliyopo ni katika Suurat Zumar aya 37 (na mwenye kuongozwa na Mwenyezi Mungu hana wa kumpoteza).

Akasema: "Enyi wana wa Adamu! Chukueni mapambo yenu."[1] Nikasema: Umetokea wapi? Akasema: "Wanaitwa kutokea sehemu ya mbali."[2] Nikasema: Unakwenda wapi? Akasema: "Na ni amri ya Mwenyezi Mungu juu ya watu kuhiji nyumba."[3] Nikasema: Ni wakati gani umekatika na kuachana na msafara? Akasema: "Kwa hakika tuliiumba mbingu na ardhi kwa muda wa siku sita."[4] Nikasema: Je, unatamani au una hamu ya chakula? Akasema: "Na wala hatukuwajaalia miili isiyokula chakula."[5] Basi nikampatia chakula, kisha nikasema: Nenda taratibu na wala usiharakishe. Akasema: "Mwenyezi Mungu hamkalifishi mtu isipokuwa kwa kadiri ya uwezo wake."[6] Nikasema: Je, nikupandishe au nikubebe pamoja na mimi? Akasema: "Lau kama kungekuwa na miungu tofauti na Mwenyezi Mungu mmoja basi mbingu na radhi vingeharibika."[7] Basi nikateremka na kumpandisha yeye. Akasema: "Ametakasika yule ambaye ametutiishia mnyama huyu."[8] Na tulipoufikia msafara nikasema: Je, unaye yeyote unayemfahamu kwenye msafara huu? Akasema: "Ewe Daud! Hakika sisi tulikufanya kuwa khalifa katika ardhi."[9] "Na hakuwa Muhammad isipokuwa ni mtume tu."[10]"Ewe Yahya! Chukua kitabu"[11]

[1]-Suuratul-Aaraf aya 29.
[2]-Suurat Fuswilat aya 44.
[3]-Surat A ali Imran aya 91.
[4]-Surat Qaaf aya 37 kwa kuzidi neno wamaa baina huma.
[5]-Suratul-Anbiyaa aya 8.
[6]-Suratul-Baqarah aya 286.
[7]-Suratul-Anbiyaa aya 22.
[8]-Surat Zukhruf aya 12.
[9]-Surat Swad aya 25.
[10]-Surat Aali Imran aya 138.
[11]-Surat Maryam aya 13.

"Ewe Musa! Hakika mimi ndiye Mwenyezi Mungu."[1] Nikapiga kelele nikiita majina haya, ghafla nikajikuta mbele ya vijana wanne wakimuelekea yeye. Nikamuliza: Ni akina nani hawa na wana uhusiano gani na wewe? Akasema: "Mali na watoto ni pambo la maisha ya Dunia."[2] Na walipomfikia akasema: "Ewe baba yangu mkodishe na umpe ujira hakika mtu mwema anayefaa kukodishwa ni yule mwenye nguvu na muaminifu."[3] Basi wakanipatia vitu kama malipo kwa kazi niliyoifanya. Yule bibi akasema: "Na Mwenyezi Mungu humuongezea amtakae."[4] basi wakaniongeza na kunizidishia, nikawauliza kuhusu mwanamke huyo wakasema: Huyu ni mama yetu Fedhwah mjakazi wa Zahra (AS) tangu miaka ishirini iliyopita hajazungumza neno lolote kamwe tofauti na Qur'an.[5]

Na wamtosha utukufu na imani yake kwa Ahlul-Bait walio maasumu na watwaharifu (AS) ya kwamba, Mwenyezi Mungu aliteremsha kuhusiana na Fedhwah akimfuatia Amiril-Muuminiin na mkewe mtwaharifu Zahra (AS) na Hassan na Hussein (AS) sura ya Qur'an itakayoendelea kusomwa hadi siku ya kiama ili awe ni kigezo kwa watu wote wenye kutaka kuwa na uhusiano mzuri na nyumba hii iliyo maasumu na kuhifadhiwa.

Na Bwana Baidhwawiy ash-Shafiiy (aliyefariki dunia mwaka 691 Hijiria) amepokea hadithi kutoka kwa Ibnu Abbas radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao ya kwamba: Hassan na Hussein radhi za Allah ziwe juu yao waliugua na

[1]-Surat Twaha aya 11-13.
[2]-Suratul-Kahf aya 44.
[3]-Suratul-Qasas aya 26.
[4]-Suratul-Baqarah aya 263.
[5]-Baitul-ahzaan ukurasa 41, Fatwimatuz-zahraa (a.s) bahjatu qalbil-mustwafaa (s.a.w.w) ukurasa 674.

Mtume (SAW) kwenda kuwatembelea kwa ajili ya kuwaona na akawasalimia watu na wakasema: Ewe baba wa Hassan unaonaje lau kama utaweka nadhiri juu ya watoto wako, Ali na Fatima radhi za Allah ziwe juu yao na Fedhwah mjakazi wao wakatia nadhiri ya kufunga siku tatu ikiwa watapona kutokana na ugonjwa wao? Basi Hassan na Hussein wakapona hali ya kuwa hawakuwa na chochote ndani ya nyumba. Ali akajikopesha kutoka kwa Shamuun al-Khabiir vibaba vitatu vya shairi na Fatima kusaga kibaba au pishi moja na kupika mikate mitano na wakaiweka mbele yao kwa ajili ya kufuturi mara wakasimamiwa na maskini mmoja akiomba. Wakaonelea ni bora wajinyime na kumpatia yeye na wakalala bila ya kuonja chochote isipokuwa maji na wakaamka wakiwa wamefunga. Ilipofika jioni na kuweka chakula kwa jili ya kufuturu mara akawasimamia yatima akiomba na wakampa chakula kile. Kisha wakasimamiwa katika siku ya tatu na mateka na kufanya kama walivyofanya siku zilizopita, mara Jibril (AS) akateremka akiwa na sura hii (yaani Suuratul-Insaan) na akasema: Ichukue ewe Muhammad! Mwenyezi Mungu anakupongeza kwa Watu wa Nyumbani Kwako).[1]

Tunasema: Kauli ya Jibril (AS): Mwenyezi Mungu anakupongeza katika Ahlil-Bait wako au Watu wa Nyumbani Kwako inaweka wazi na kukata shauri kati ya ule ugomvi usemao kuwa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu isemayo: "Hakika si jambo jingine Mwenyezi Mungu anataka kukuondoleeni uchafu enyi Watu wa Nyumba ya Mtume na kukutwaharisheni kikamilifu)[2] kwamba iliteremka kuhusiana na watu wengine tofauti na wao.

[1]-Tafsiirul-Baidhwawiy juzuu 5 \ 270 na 271.
[2]-Suratul-Ahzaab aya 33.

Ndio:

Hao ni mababa zangu basi niletee na unijie na mfano wao pindi mikusanyiko itakapotujumuisha na kutukusanya ewe jariru.[1]

[1]-Asaasul-Balagha, madda: Jama'a kati ya mashairi ya Farazdaq.

MWENYEZI MUNGU ANALO JESHI MIONGONI MWA WAAFRIKA LENYE KUWANUSURU AHLUL-BAITI (AS)

Muhammad bin Musa ad-Damiriy ash-Shafiiy (aliyefariki mwaka 672 hijira) amenukuu kutoka kwa Ibn Khalkaan katika tarjuma ya Imam wa saba Musa al-Kaadhim (AS) ya kwamba: Haroun Rashiid alimuweka jela katika mji wa Baghdad kisha siku moja alimuita msimamizi wa jeshi lake la polisi na kumwambia: Nimeona katika ndoto yangu jeshi likinijia likiwa pamoja na harbah (jambia) na akasema: Ikiwa hukumuachia huru Musa bin Jaafar nitakuchinja kwa jambia hili. Basi nenda na umuachie huru na umpatie dirhamu elfu thalathini na umwambie: Ikiwa utataka kubakia hapa kwetu basi utapata ukitakacho kutoka kwangu na ukipenda kwenda Madina basi nenda.

Mkuu wa polisi akasema, nikafanya vile nilivyoagizwa, na nikamwambia: Kwa hakika nimeona maajabu kuhusiana na wewe. Akasema: Mimi nitakufahamisha wakati nilipokuwa nimelala mara nikajiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na kusema: Ewe Musa! Umefungwa hali ya kuwa ni mwenye kudhulumiwa, basi sema na kariri maneno haya kwa hakika wewe usiku huu hutalala katika jela, sema: Ewe msikivu wa kila sauti! Ewe mwenye kukitangulia kila chenye kupita! Ewe mwenye kuivisha mifupa nyama na mwenye kuifufua baada ya kufariki! Ninakuomba kwa majina yako matukufu na makubwa na kwa jina lako lilo kubwa zaidi (aadham) na kubwa zaidi lililo hifadhiwa na kufichwa, ambalo hakuna yeyote aliyewahi kuliona wala kulielewa kati ya viumbe. Ewe mpole mwenye huruma isiyokadiriwa! Ewe mwenye wema ambaye wema wake haukomi wala kukatika

milele na wala hatuwezi kuuhesabu! Nifariji. Basi likatokea ulionalo.[1] Kisha ad-Dumairiy akasema:

Na Musal-Kaadhim alikufia Baghdad kwa sumu na imesemekana kwamba yeye alikufia jela. Shafii alikuwa akisema: Kaburi la Musal-Kaadhim ni dawa iliyo mujarrab.[2]

Tunasema: Kauli ya Shafii ambaye ni mmoja kati ya maimamu wa madhehebu manne: Kaburi la Musal-Kaadhim ni dawa iliyo Mujarrab - yaani ni dawa yenye manufaa na faida ambayo ameijaribu na kutumiwa na watu wengi na kunufaika nayo kwa kufanya tawassuli kupitia kwake – ilikuwa ni katika kuwajibu wale ambao wanaharamisha kufanya tawasuli kupitia makaburi ya mawalii wema, bila ya kuwa na elimu, ujuzi,muongozo wala kitabu chenye kuwaangazia, na wanashikamana na baadhi ya riwaya dhaifu ambazo Shafii na wengine mfano wake hawakuzijali wala kuzitilia umuhimu.

---

[1]-Angalia Wafayaatul-aayaan cha ibnu Khalaqaan juzu 5 \ 309 kwni amenukuu kutoka kwenye kitabu Muruujudh-dhahab cha Masoud juzu 3 \ 346.

[2]-Hayaatul-hayawaan cha Dumairiy juzu 1 \ 184-mada: Al-bauudhu.

KUSALLIM AMRI KIJANA WA KIAFRIKA MBELE YA AMRI YA MOLA WA VIUMBE NA KUZAMA NA KUJITOLEA UHAI WAKE KWA AJILI YA AMIRIL-MUUMINIIN (AS)

Msimuliaji An-Nuriy (Mungu autukuze utajo wake - aliyefariki dunia mwaka 1320 Hijiria) amepokea hadithi na kusimulia kutoka kwa As'bagh bin Nubatah kwamba: Niliingia katika mojawapo ya siku kwa Amiril-Muuminiin (AS) katika msikiti wa Jaamiul-Kufah, mara nikaona kundi kubwa akiwemo mtwana mweusi, wakasema: Ewe Amiril-Muuminiin! Mtwana huyu ni mwizi. Imam akamwambia: Ewe mtumwa (ghulam)! Je, wewe ni mwizi? Akasema: Ndio. Akamuuliza kwa mara ya pili: Ewe mtumwa! Je, wewe ni mwizi? Akasema: Ndio ewe mtawala wangu! Imam akamwambia: Ukiyasema hayo mara ya tatu nitaukata mkono wako wa kulia. Akamuuliza: Je, wewe ni mwizi ewe ghulam?! Akasema: Ndio ewe maula wangu! Imam akaamuru akatwe mkono wake wa kulia. Ukakatwa mkono wake wa kulia naye akauchukua kwa mkono wake wa kushoto hali ya kuwa unachuruzika damu. Mara Ibn al-Kuwa ambaye alikuwa akimchukia sana Amiril-Muuminiin (AS) akakutana naye, akamwambia: Ni nani aliyekata mkono wako wa kulia? Akasema: Aliyeukata ni yule mwenye kipara na tumbo kubwa (mwenye kitambi)[1] na mlango wa wacha Mungu, na kamba ya Mwenyezi Mungu iliyo madhubuti, na muombezi siku ya kiama, mwenye

[1]-Imesemwa kuwa: Al-anzau minash-shirki (alie vuliwa na kuepushwa na ushirikina), na Batwiin yaani: alie jawa na elimu na imani, (Angalia: Majmaul-bahraini, mada Naza'a).

kuswali swala khamsini na moja. Akataja sifa nyingi hadi akafikia kusema: Na mtumwa au ghulamu yule alipomaliza kutaja sifa au kumsifia na kwenda zake, Abdallah bin Alkaw akaingia kwa Imam na kumwambia: Assalaam alaika ewe Amiril-Muminiin. Amiril-Muuminiin (AS) akamwambia: Amani iwe juu ya mwenye kufuata uongofu, na akaogopa mwisho wa uovu maangamio na kufru. Akamwambia: Ewe Abal-Hassan! Hivi kweli umeukata mkono wa mtumwa mweusi, na nimemsikia akikusifu kwa kila sifa njema. Akasema: Umemsikia akisema nini? Akasema: Amesema hivi na hivi, na kumtajia yote aliyoyasema mtumwa yule. Imam akawambia watoto wake wawili Hassan an Hussein (AS): Nendeni mniletee mtumwa yule. Wakaenda kumtafuta katika kabila la Kindah. Wakamwambia: Itika wito wa Amiril-Muminiin, ewe ghulam! Akasema: Na alipofika na kusimama mbele ya Amiril-Muuminiin (AS) Akawambia: Nimeukata mkono wako wa kulia na wewe unanisifu kwa sifa zilizonifikia! Akasema: Ewe Amiril-Muuminiin! Hukuukata isipokuwa kwa haki iliyo wajibu, aliyoiwajibisha Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Imam (AS) akasema: Nipe kitanga chako cha mkono, Imam akakishika kitanga cha mkono na kukifunika kwa nguo akapiga takbira na kuswali rakaa mbili na kuzungumza au kusema maneno fulani na nilimsikia akisema mwishoni mwa dua yake: 'Aamin Rabbal-Aalamiin' na kuunganisha kwenye kiungio (Zand), na akawambia maswahibu wake: Itoeni nguo kwenye kitanga wakaifunua ile nguo kutoka kwenye kitanga cha mkono. Mara wakakiona kitanga kile kikiwa kwenye Zand au maungio yake kwa idhini ya Mwenyezi Mungu

Mtukufu.[1]

Tunasema: Hadithi hii inathibitisha na kuweka wazi imani kubwa ya Muafrika huyu kwa Amiril-Muuminiin (AS) na kutotatizika kwake kutokana na mafunzo ya Kiislamu hata kama yatasababisha kukatwa mkono wake, pindi atakapoyapituka na kutenda kinyume chake. Naye ni kielelezo na uthibitisho wa kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu isemayo: "Ninaapa kwa jina la Mola wako. Hawataamini mpaka wakufanye wewe kuwa hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao kuhusiana na yale uliyoyahukumu na wasalimu amri kikweli kweli.[2]

[1]-Mustadrakul-wasaail juzu 18 \ 33 min abwaab haddis-sirqah h 11 ukurasa 152.
[2]-Suratun-nisaai aya 65.

JOHN BIN HAWIYYU MTWANA WA ABI DHARRIL-GHIFARIY

Na miongoni mwa watu hawa walio huru na wema ni John bin Hawiyyu bin Qataadah Binil-Aawar bin Saaidah bin Awf bin Kaab bin Hawiyyu mtwana wa Abi Dharril-Ghifariy (Radhi za Allah ziwe juu yake) na ambaye alitokea Afrika.

Waandishi wa sira wanasema kwamba, alikuwa ni mtumwa mweusi wa Fadhli bin Abbas bin Abdul-Muttwalib. Alinunuliwa na Amiril-Muuminiin (AS) kwa dinari mia khamsini na akamtoa zawadi kwa Abi Dharril-Ghafariy ili amtumie kama mtumishi na alibakia kwake hadi alipotoka pamoja naye kuelekea Rabdha (Makimbilio ya Abudharri alipofukuzwa na Othumani bin Affan).

Abu dharri alipofariki dunia katika mwaka 32 Hijiria, mja huyu mwema alirudi na kujiunga na Amiril-Muuminiin (AS) kisha akahamia kwa mwanawe Imam Hassan (AS), kisha kwa Imam Hussein (AS). Alikuwa kwenye nyumba ya Sajjad Imam Zainul-Abidiin (AS)[1] akinywa maji yao safi (AS) hadi yalipokaribia mapigano na vita vya Karbalaa. Akatoka pamoja na Imam Hussein (AS) kutoka Madina hadi Makkah kisha kuelekea Karbalaa, malazi ya watu wenye kumpenda Mwenyezi Mungu mwenye rehma na mabwana wa peponi.

Bwana wa maurafaa na salikiin Ridhwiyud-Dini Abul-Qaasim Ali bin Musa bin Jaafar bin Twausu (Mungu autukuze utajo wake - aliyefariki dunia mwaka 664 Hijiria) ameashiria kuhusiana na kuanza kwa mapigano siku ya

[1]-Angalia:Tanqiihul-Maqaal fii Ilmir-Rijaal-jina John mtwana wa Abidharri, namba: 1992.

Ashura na kusimama kwa John akimuomba ruhusa Imam Hussein (AS). Alisema: Kisha akajitokeza John mtwana wa Abi Dharri, na alikuwa ni mtwana mweusi. Na (AS) akamwambia: Wewe ni mwenye idhini kutoka kwangu, kwa hakika umetufuata kwa ajili ya kutafuta afya yako, basi usiingie na kukumbwa na mitihani ya njia[1] yetu hii.

Akasema: Ewe mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Je, wataraji mimi wakati wa raha nikae na kula kwenye sahani zenu[2] na wakati wa shida nikuacheni? Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, hakika harufu yangu ni yenye kunuka na kwamba hadhi yangu ni mbaya na rangi yangu ni nyeusi, basi nifungulie milango ya pepo, ili harufu yangu iwe nzuri na hadhi yangu iwe tukufu na uso wangu uwe mweupe. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, haiwezekani kamwe kukutengeni na kukuacheni mpaka damu hii nyeusi (damu ya mtu mweusi) ichanganyike pamoja na damu yenu. Kisha akapigana hadi kuuliwa, radhi za mwenyezi Mungu iwe juu yake.[3]

Na imepokelewa kutoka kwa Muqaatil Abi Twalib kwamba, wakati alipojitokeza John kwa ajili ya mapigano alisema: Makafiri watayaona vipi mapigo ya mtu mweusi akiwakinga na kuwatetea watoto wa Muhammad kwa upanga! Ninawatetea kwa ulimi na mkono.* Ninataraji kwa kufanya hivyo kupata pepo siku ya marejeo.

Kisha akapigana hadi kuuwawa (baada ya kuua watu

[1]-Yaani usitihaniwe na mwendo wetu huu nayo ni jihadi na kupigana na adui hadi pumzi ya mwisho.
[2]-Qiswaa'akum: ni wingi wa Qas'ah nacho ni chombo cha chakula kitumikacho kulia chakula.
[3]-Almalhuuf ala Qatlaat-Tufuuf ukurasa 163.

ishirini na tano).[1] Imam (AS) akamsimamia na kusema: Ewe Mwenyezi Mungu! Ufanye mweupe uso wake, ifanye nzuri harufu yake, mfufue pamoja na watu wema na mtambulishe kwa Muhammad na Aali zake.

Na imepokelewa kutoka kwa Imam Baaqir (AS) kutoka kwa baba yake ya kwamba: Watu walikuwa wakihudhuria mapigano na kuwazika watu waliouwawa, mara wakamkuta John baada ya kupita siku kumi akitokwa na harufu ya miski.[2]

Ukiachia haya mbali, kwa hakika Mwenyezi Mungu alimzidishia utukufu juu ya utukufu wa kufa shahidi na kupendeza kwa harufu yake, kwa kumuhusisha na Imam al-Hujjah mwenye kungojewa, Mwenyezi Mungu aharakishe kudhihiri kwake, kwa salamu maalu katika Ziyaratun-Naahiyah al-Quqaddasah. Kwani imekuja kwenye ziyara hiyo: Amani iwe juu ya John bin Hariyyi, mtwana wa Abi Dharril-Ghifariy.[3]

[1]-Alaa maa fi Nafsil-Mahmuum ukurasa 291 akinukuu kutoka kwenye kitabul-Manaaqib cha Ibnu Shahri Aashuub juzuu 4 \ 103 chapa ya Qum.
[2]-Qaamusir-Rijaali, juzuu 2, jina John mtwana wa Abi Dharri-namba: 1615, ukurasa 756.
[3]-Al-Iqbaal cha Sayyid Ibnu Twawuus juzuu 3 \ al-Babul-Awwal: fiima yataallaku bi shahri-Muharram-ukurasa 78.

UKWE WA MAIMAMU MAASUMU WA AHLUL-BAIT (AS) KWA WATU WA AFRIKA

HAMIDAH MBARBARI

MAMA WA IMAM MUSAL-KAADHIM (AS)

Ni jambo lililo maarufu kwamba, idadi kadhaa ya Maimamu Maasumu wa Ahlul-Bait wa Mtume Mtukufu (SAW) walikuwa ni wakwe wa watu wa Afrika. Hilo ni kutokana na sifa nzuri walizozibeba na walizonazo za utwaharifu na ucha-Mungu (kuhifadhika na mambo ya kijinsia) na kusafika kwao kutokana na uchafu na najisi. Kwa mfano, huyu hapa Imam Jaafar bin Muhammad Swadiiq (AS) anamuoa mwanamke aitwae Hamidah binti Swaaid al-Barbariy[1] na ambaye alimzalia Imam Musal-Kaadhim (AS). Ni jambo lisilofichika kwamba Barbari ni

[1]-Ad-durrun-nadhwiim: ukurasa 649.

jina litumikalo kuwaitia wakazi wa Afrika ya Kaskazini, na kabla ya Uislamu hawakufurahia kuwa chini ya utawala wa Roma wala kujiunga na dini ya Ukristo. Kwa hivyo kwa kuja Uislamu ukiletwa na Aqabah bin Naafiu (katika karne ya kwanza Hijiria), kikundi miongoni mwao kiliingia katika dini ya Kiislamu na kikashiriki katika ukombozi wa Andalusi (Hispania) kwa uongozi wa Twariq bin Ziyad.

Na liliposimama dola la Adaarisa (Maidrisa) mwaka 172 Hijiria, yaliingia kwenye dini ya Kiislamu makundi kwa makundi na Uislamu wao kuwa mzuri zaidi kama tutakavyoelezea baadaye inshallah tala.

Ala kulli hal, amepokea Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (aliyefariki dunia mwaka 328 Hijiria) kutoka kwa Bin Muhammad al-Ash'ariy, kutoka kwa Mualla bin Muhammad, kutoka kwa Ali bin as-Sanadiy al-Qumiy, kwamba: Tumesimuliwa na Isa bin Abdur-Rahmaan, kutoka kwa baba yake, amesema: Ibnu Ukashah bin Muhswin al-Asadiy aliingia kwa Abi Jaafar (Imam al-Baaqir AS) na Abu Abdillah (yaani Imam Swaadiq AS) alikuwa amesimama kwake na akampatia zabibu, na akasema: Tembe moja moja anaila shekhe mkubwa (mtu mzima) na mtoto mdogo, na tatu na nne anazila anayedhania ya kwamba yeye hashibi, na kula tembe mbili mbili, hakika ni sunna kufanya hivyo.

Akasema kumwambia Abi Jaafar (AS): Ni kwa sababu gani humuozi Aba Abdillah hakika amefikia wakati wa kuoa? Akasema mbele yake kukiwa na kifuko kimefungwa: Ama kwa hakika atakuja kuuza watumwa kati ya watu wa Barbar na atafikia kwenye nyumba ya Maimauun, na tutamnunulia kwa kifuko hiki cha pesa mjakazi. Akasema: Ikafika siku hiyo na kutokea yale yaliyotokea. Siku moja

tuliingia kwa Abi Jaafar (AS) na kusema: Je, nikukupeni habari kuhusiana na muuza-watumwa ambaye nilikutajieni, kwa hakika amekwisha wasili. Basi nendeni na nunueni kwa kifuko hiki cha pesa mjakazi kutoka kwake. Akaksema: Tukamwendea yule muuza-watumwa na akasema: Tayari nimekwishauza niliokuwa nao isipokuwa wajakazi wawili ambao ni wagonjwa. Mmojawapo ni bora na mwenye hadhi kuliko mwingine. Tukasema: Basi watoe ili tuwaangalie naye akawatoa, tukasema: Huyu aliye bora na mwenye hadhi kuliko mwingine utatuuzia kwa kiasi gani? Akasema: Dinari sabini, tukasema: Fanya ihsani. Akasema: Sipunguzi chini ya dinari sabini. Tukamwambia: Tutamnunua kwa kijifuko hiki kwa kiwango chochote kitakacho kuwemo cha pesa na hatujui kiwango kilichomo na kulikuwa na mtu mwenye kichwa cheupe na ndevu nyepe (yaani mtu mwenye busara). Akasema: Fungueni na mpime. Akasema yule muuza-watumwa: Msifungue hakika ikiwa itapungua sarafu moja kati ya dinari sabini sitakuuzieni. Yule shekh akasema: Sogea, tukasogea na kufungua kile kizibo na kuzipima dinari zile mara tukakuta zikiwa ni danari sabini hazipungui wala kuzidi, na hapo tukamchukua yule mjakazi na kumpelekea Abi Jaafar (AS) na Jaafar akiwa amesimama mbele yake.

Na tukamfahamisha Aba Jaafar yaliyotokea, akamhimidi Mwenyezi Mungu na kumsifu kisha akamuuliza mjakazi yule: Jina lako nani? Akasema: Hamidah. Akasema: Ni Hamida duniani na mwenye kuhimidiwa (mahmuudah) katika akhera, hebu nifahamishe kuhusu hali yako mwenyewe, je, wewe ni bikra au ni thayyib (asiye bikra)? Akasema ni bikra, akasema: Itakuwaje uwe bikra wakati ambapo kila atumbukiaye kwenye mikono ya wauza

watumwa hatoki isipokuwa humharibu? Akasema: Kwa hakika alikuwa akinijia na kukaa pembezoni mwangu kama akaovyo mwanamume kwa mwanamke na Mwenyezi Mungu kumghilibu kwa mtu mmoja mwenye kichwa cheupe na ndevu nyeupe na hakuacha kumpiga makonde mpaka anaposimama na kutoka mahali nilipo, na alinifanyia hivyo mara kadhaa na yule shekh akamfanya vilev kwa mara kadhaa. Akasema: Ewe Jaafar! Mchukue, naye akamzaa mbora wa watu wa ardhini Musa bin Jaafar (AS)[1]

Na Kulainiy (Mungu autukuze utajo wake) amepokea pia kutoka kwa Muhammad bin Yahya, kutoka kwa Muhammad bin Ahmad, kutoka kwa Abdallah bin Ahmad, kutoka kwa Ali bin al-Hussein, kutoka kwa Ibni Sinan, kutoka kwa Saabiq bin al-Waliid, kutoka kwa al-Muallaa bin Khaniis ya kwamba, Aba Abdillah (AS) amesema: Hamidah ni mwenye kutakaswa kutokana na makosa na uchafu kama tofali la dhahabu lililo safishwa, na malaika hawakuacha kuendelea kumlinda mpaka akafikishwa na kukabidhiwa kwangu ikiwa ni takrima kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili yangu na kwa ajili ya Hujja atakayekuja baada yangu.[2]

Pamoja na haya, kwa hakika msimuliaji mkubwa na mfuatiliaji wa habari mwenye uzoefu Shekh Abbas al-Qumiy (alieyfariki dunia mwaka 1359 hijria) amesema kwamba: Kilicho dhahiri kwangu kutokana na baadhi ya riwaya ni kwamba, mjakazi yule (yaani Hamidah al-Barbariyyah) alikuwa ni mwenye elimu sana na mwenye

[1]-al-Kafiy juzuu 1 \ mlango: Maulid Abil-Hassan Musa bin Jaafar (a.s) h 1 ukurasa 476, 477.
[2]-al-Kafiy juzuu 1 \h, 2 477.

kufahamu sheria (fiqhi) na aliyezama katika hukumu za dini hadi ilifikia kwamba, Imam Swaadiq (AS) alikuwa akiwaamuru wanawake kurejea kwake katika kujifunza na kuchukua hukumu za kisheria.[1]

[1]-Muntahal-Amaal juzu 2 \ 289.

NAJMAH WA MOROKO
MAMA WA IMAM RIDHAA (AS)

Shekh Swaduuq (Mungu autukuze utajo wake) anasimulia kutoka kwa baba yake (Mungu amrehemu) kwamba: Tulisimuliwa na Saad bin Abdallah kutoka kwa Ahmad bin Muhammad bin Isa kutoka kwa Hassan bin Mahboub kutoka kwa Yaakub bin Is'haq kutoka kwa Abi Zakariya al-Waasitwiy kutoka kwa Hisham bin Ahmad kwamba: Abul-Hassanil-Awwal (AS) amesema: Je, unamfahamu yeyote kati ya watu wa Moroko aliyekuja? Nikasema: Hapana. Akasema (AS): Ndio, kwa hakika amekuja mtu mmoja mwekundu basi twende pamoja. Akapanda na sisi tukapanda pamoja naye hadi tukafika kwa mtu yule, ghafla tukamuona mtu yule kutoka Moroko akiwa na watumwa, akamwambia: Tuonyeshe watumwa ulio nao, naye akatuonyesha wajakazi tisa na kila aliyekuwa akimtazama Abul-Hassan alikuwa akisema, sina haja naye. Kisha akamwambia: Tuonyeshe wengine, akasema: Sina kitu tena. Akamwambia: Ni kipi kinachokuzuia kutuonyesha? Yule bwana akamkatalia. Kisha Imam (AS) akaenda zake. Kisha alinituma kesho yake kwa bwana yule. Akaniambia: Mwambie: Ni kiwango gani ukitakacho kwa mjakazi huyo? Ikiwa atasema: Kadhaa wa kadhaa mwambie: Nimemchukua (au nimemnunua). Nikamwendea bwana yule, akasema: Sitaki kumpunguza kwa kiwango kadhaa, nami nikasema: Basi nimemchukua na pesa hii ni yako. Akasema: Basi mchukue ni wako, lakini ni mtu gani uliyekuwa naye jana? Nikasema: Ni mtu mmoja wa kabila la Bani Haashim. Akauliza: Katika Bani Haashim

gani? Nikamwambia[1]: Kati ya wateule wao. Akasema: Ninataka maelezo zaidi ya haya. Nikasema: Sina maelezo zaidi ya haya. Akasema: Ninakufahamisha kuhusu mjakazi huyu.[2] Hakika nimemnunua kutoka sehemu za mbali za nchi ya Moroko (Maghribi) mara nikakutana na mwanamke mmoja kati ya watu waliopewa kitabu, akasema: Ni mjakazi gani huyu uliyenae? Nikasema: Nimemnunua kwa ajili yangu, Akasema: Mjakazi huyu hafai kuwa kwa mtu kama wewe, hakika mjakazi huyu anapaswa kuwa kwa mtu mbora kabisa kati ya watu wa ardhini, na hatakaa na kubakia kwao isipokuwa muda mchache tu na kuwazalia mtoto ambaye watu wa Mashariki na Magharibi watafuata dini yake na kumtii. Akasema: nikaja naye, na hakukaa kwake isipokuwa muda mchache tu akamzalia Ali (AS).[3]

Tunasema: Huenda mwanamke huyu wa Ahlul-Kitab alikuwa na mahusiano na mjakazi huyu na alimfahamisha yatakayomtokea.

Kwa vyovyote itakavyokuwa, mjakazi huyu alikuwa na majina mengi kati ya hayo ni: Najmah, Ar'waa, Sakinah, Samaanah na Tuktam. Alipomzaa Imam Ridhaa (AS), Imam Kaadhim (AS) akamuita (Twaahirah).[4]

Kwa hakika Najmah al-Maghribiyyah (Mmoroko) alikuwa miongoni mwa wanawake bora kabisa katika akili na dini yake na katika kumtukuza kwake mawlati (bibi mkuu) wake Hamidah al-Barbariyyah aliyesafishwa na kutakaswa ambaye alikuwa ni mama wa Imam Musal-Kaadhim (AS). Kwa hakika Imam Kaadhim Alimnunua Najmah kwa ajili ya

[1]-Katika Ikhtisaas: (Nikamwabia)- bila kutaja dhamiri-ukurasa 197.
[2]-Yaani mhudumu na mjakazi.
[3]-Uyuunul-Akhbaari-Ridhaa (AS) juzuu 1 \ 17-18- na mfano wa hadithi hiyo iko kwenye kitabu Al-Ikhtisaas ukurasa 197.
[4]-Kitabu hicho hicho kilicho tangulia.

mama yake Hamidah Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake ambaye alimtaja mjakazi wake kwa kusema:

Hakika alimuona ndotoni Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) akimwambia: Ewe Hamidah mtoe zawadi Najmah, kwa mwanao Musa hakika atamzalia kutoka kwa mjakazi huyu mtu bora kabisa ardhini, naye akamtoa zawadi kwa Musa , na alipomzalia Imam Ridhaa (AS) akamuita (Twahirah).

Kwa hakika Najmah alikuwa akimheshimu mawlati (Bi mkubwa) wake kwa kiwango kikubwa hadi ilifikia kwamba alikuwa hakai mblele yake tangu alipommiliki kwa ajili ya kumuheshimu na kumtukuza. Alimwambia mwanawe Musa (AS): Ewe mwanangu! Hakika Tuktam (yaani Najmah) ni mjakazi ambaye sijawahi kuona mjakazi aliye bora kumliko yeye na sina shaka yoyote ya kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu atakidhihirisha kizazi chake ikiwa atakuwa na kizazi, na kwa hakika nimekupatia wewe kama zawadi basi jiusie kheri kwa mjakazi huyo.

Kwa hakika alikuwa ni mwingi wa kuswali na mwingi wa kumsabbihi Mwenyezi Mwenyezi Mungu hadi ilifikia kwamba yeye alimtafutia mwanawe mnyonyeshaji ili apate faragha na muda wa kussali na kufanya ibada.[1]

Na baada ya haya watu fulani wamepokea hadithi na kusimulia kwamba, mama wa Imam Ridhaa (AS) alikuwa akiitwa Sakan an-Nuubiyyah (Mnubi)[2], na hii haidhuru bahthi yetu kutokana na mkusudiwa na mlengwa kuwa mmoja.

[1]-Angalia Uyuunu Akhbaarir-Ridhwaa ukurasa 14-15.
[2]-Chanzo hicho hicho.

SABIIKAH MNUBI
MAMA WA IMAM JAWAAD (AS)

Sabiikah Mnubi ni mke wa Imam Ali Ridhaa (AS) na mama wa Imam Muhammad al-Jawaad. imepokelewa kwamba, alikuwa ni miongoni mwa watu wa familia na nyumba ya Mariyah mama yake Ibrahim mtoto wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW).[1]

Hakika utukufu wa Sabiikah Mnubi mke wa Imam Ridhaa (AS) ulifikia kiwango ambacho kilimfanya Mtume Mtukufu (SAW) akawa akimsifia kabla ya kuzaliwa.

Thiqatul-Islaam Al-Kulainiy amepoa kutoka kwa Ali bin Ibraahim kutoka kwa baba yake, na kutoka kwa Ali bin Muhammad al-Qaasaniy wote, kutoka kwa Zakaria bin Yahya bin an-Nuuman As-Swairafiy kwamba: Nimemsikia Ali bin Jaafar akimsimulia Hassan bin Ali bin Hussein akisema: Wallahi! Mwenyezi Mungu alimnusuru Abal-Hassan ar-Ridhaa (AS), na Hassan akamwambia: Wallahi! Ndio nifanywe kuwa fidia yako, kwa hakika ndugu zake walimfanyia uovu. Ali bin Jaafar akasema: Wallahi! Ndio, na sisi ni baba zake wadogo (ami zake) tumemfanyia makosa au tumemkosea. Hassan akamwambia: Nifanywe kuwa fidia yako mmefanyaje hakika mimi sikuwa pamoja nanyi? Akasema: Ndugu zake walimwambia na sisi pia: Kamwe hakuna kati yetu Imam mwenye rangi iliyobadilika aliye mweusi. Ridhaa (AS) akawambia: Yeye ni mwanangu.

Wakasema: Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu alihukumu kwa kutumia uchunguzi wa nasaba (al-

[1]-Al-Kafiy juzuu 1 \- mlango: Maulid Abi Jaafar Muhammad bin Ali ath-Thaniy (AS)-ukurasa 492.

Qaafiah)[1], basi tumuweke kati yetu sisi na kati yako mchunguzi wa nasaba. Akasema: Tumeni nyinyi wenyewe kwao ama mimi sitafanya hivyo, na wala msiwafahamishe jambo lililowafanya kuwaita na kaeni majumbani mwenu.

Pindi walipokuja wakatukalisha kwenye bustani (au shambani) na ami zake kujipanga msitari na ndugu zake wa kike na kiume na wakamchukua Ridhaa (AS) na kumvisha juba na kofia ya sufi na wakamuwekea shingoni mwake (guduria la kumwagilia maji), na wakamwambia: Ingia Bustanini na ujifanye kana kwamba unafanya kazi humo. Kisha wakamleta Abi Jaafar (AS) wakasema: Kijana huyu Mnasibisheni (muunganisheni) na nasaba ya baba yake. Wakasema: Hana baba hapa lakini huyu ni ami (baba mdogo) wa baba yake, na huyu ni ami wa baba yake, na huyu ni ami yake, na huyu ni shangazi yake, na kama atakuwa na baba hapa basi yeye ni mwenye bustani (yuko kwenye bustni). Nyayo zake na nyayo za huyo ni moja. Abul-Hassan (AS) (ar-Ridhwaa) aliporejea wakasema: Huyu ndiye baba yake. Ali bin Jaafar Akasema: Nikasimama na kunyonya jasho la Abi Jaafar (AS) kisha nikamwambia: Ninashuhudia ya kwamba wewe ni Imam wangu kwa Mwenyezi Mungu, na Ridhwa (AS) akalia kisha akasema: Ewe ami yangu! Je, hukumsikia baba yangu akisema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW): 'Naapa kwa jina la baba yangu, mtoto wa mjakazi aliye bora mtoto wa Mnubi mwenye mdomo mzuri aliyechaguliwa kizazi chake'.[2]

Tunasema: Hadithi hii inathbitisha ya kwamba, Imam al-

[1]-al-Qaafah: ni wingi wa Qaaif naye ni yule ambaye hufuatilia athari za nasaba na kuzifahamu na kufahamu kufanana kwa mtu fulani na ndugu yake na baba yake na kuhukumu juu ya nasaba yake.

[2]-al-Kafiy: juzu 1 \ -mlango Ishaarah wan-nas Ala Abi Jaafar ath-Thaniy (AS) –h14 ukurasa 322.

Jawaad (AS) takriban alikuwa akifanana na Waafrika kwa upande wa rangi, na hiyo ni kutokana na ukweli kwamba mama yake kama ilivyotangulia na kuelezwa katika hadithi pia, alikuwa ni miongoni mwa wajakazi walio bora na alikuwa anatokea katika miji ya Unubi barani Afrika.

Na Kulainiy (Mungu autukuze utajo wake) amepokea pia kutoka kwa Ahmad bin Mahran, kutoka kwa Muhammad bin Ali, kutoka kwa Abil-Hakam al-Armaniy kwamba: Nimehadithiwa na Abdallah bin Ibrahim bin Ali bin Abdallah bin Jaafar bin Abi Twalib, kutoka kwa Yazid bin Saliit az-Zaidiy[1], Abul-Hakam amesema: Na nimepewa habari na Abdallah bin Muhammad bin Ammarah al-Jurmiy, kutoka kwa Yazid bin Saliit amesema: Nilikutana na Aba Ibrahiim (AS) (yaani Kaadhim) -na sisi tukikusudia kwenda safari ya Umrah - tukiwa njiani, nikasema: Nifanywe kuwa fidia yako, je, unaifahamu vyema sehemu hii ambayo tuko hivi sasa? Akasema: Ndio je, wewe unaifahamu vyema? Nikasema: Ndio hakika mimi na baba yangu ndio tulikutana na wewe hapa na wewe ukiwa pamoja na Abi Abdillah (AS) na akiwa na ndugu zako. Yazid akasema: Kisha baba wa Ibrahiim (AS) akasema: Hakika mimi nitachukuliwa katika mwaka huu na jambo la (Uimamu) litakuwa kwa mwanangu Ali, ameitwa Ali na Ali: Ama Ali wa kwanza ni Ali bin Abi Twalib, ama Ali mwingine ni Ali bin Hussein (AS). Amepewa ufahamu, upole, nusra, mapenzi, dini na mitihani ya Ali wa kwanza, na vilevile mitihani ya mwingine na subira yake juu ya mambo yachukizayo na si juu yake kuzungumza isipokuwa baada ya kifo cha Haroun kwa muda wa miaka minne.

[1]-az-Zaidiy ni kujinasibisha kwa Zaidi Shahidi kwa upande wa nasaba si upande wa Madhehebu.

Kisha Akaniambia: Ewe Yazid! Pindi utakapopita sehemu hii na kukutana naye na utakutana naye hapo baadaye, basi mpe bishara ya kuwa atapata mtoto, muaminifu, mwenye kubarikiwa, na mwenye baraka, na atakufahamisha ya kuwa wewe umekutana na mimi. Basi mpe habari wakati utakapokutana naye ya kwamba mjakazi ambaye atamzaa mtoto huyu ni mjakazi atokanaye na familia ya Mariyah mjakazi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) na mama wa Ibrahim, na ikiwa utaweza kumfikishai salamu kutoka kwangu mjakazi huyu basi fanya hivyo.[1]

Tinasema: Inatosha katika kufahamu utukufu na ukubwa wa Sabiikah Mnubi wa Afrika kwamba, Imam Musa al-Kaadhim (AS) anamuamuru Yazidi bin Saliit amfikishie salamu zake, kama alivyofanya Mtume wetu (SAW) wakati alipomuamuru Jaabir bin Abdallah al-Answariy radhi za Allah ziwe juu yake amfikishia salamu zake Imam Baaqir (AS).

[1]-al-Kafiy, juzuu 1 \ babu al-Isharatu wan-Nassu alaa Abil-Hassan Ar-ridhaa (AS) h 14 ukurasa 313-315.

SUMAANAH MMOROKO
MAMA WA IMAM ALI AL-HADIY (AS)

Sumanah Mmoroko na inasemekana jina lake lilikuwa ni Jumanah, mama yake Imamu wa kumi Ali al-Hadiy (AS), alikuwa akijulikana kwa jina la Sayyidah na alikuwa wakati wote amefunga na hana mfano katika ucha Mungu[1] na alikuwa akijulikana kwa kuniya ya: Umul-Fadhli.

Imepokelewa kutoka kwa Muhammad bin al-Faraj na wengineo kwamba: Abu Jaafar (AS) (yaani Imam al-Jawad) aliniita na kunijulisha ya kwamba msafara umekuja na kwenye msafara huo kuna muuza watumwa na kwamba ana mjakazi (mahsusi). Akanipatia kifuko cha pesa kukiwa na dinari sitini ndani yake na akinipatia sifa za mjakazi aliyekuja naye mapambo yake na sura yake na nguo zake alizoziva. Akaniamuru kumnunua mjakazi huyo, nikenda na kumnunua kwa fedha alizo zipokea na thamani ya kumnunua mjakazi huyo ni kiwango kile alichonipatia. Na alinunuliwa na yule muuza watumwa na hakufanya uamuzi wa kumkaribia kijinsia hadi akamuuza.[2]

Na Muhammad Binil-Faraj na Ali bin Mahziyaar wamepokea kutoka kwa Abil-Hassan (AS) (yaani Imam al-Hadiy) ya kuwa amesema: Mama yangu ni mwenye kufahamu haki yangu naye ni miongoni mwa watu wa peponi, shetani hamkaribii kwa utashi wake wala havimfikii vitimbi vya mwenye kiburi na mpingaji. Naye ni mwenye kuhifadhiwa na kulindwa na jicho la Mwenyezi Mungu Mtukufu lisilo lala, na haendi kinyume wala kukengeuka maadili ya akinamama wa watu wakweli na watu wema.

[1]-Angalia kitabu Muntahal-Amaal, juzuu 2 \ 591.
[2]-Ithbatul-Waswiyyah –ukurasa 228.

Tunasema: Hakika weusi wa ngozi ya Imamu wetu al-Hadiy (AS) kama tutakavyo eleza hapo baadaye, ima ilikuwa ni kutokana na upande wa mama yake au kutokana na upande wa baba yake Imam Jawad kwani. Inasemekana kwamba alikuwa ni mwenye rangi iliyobadilika (yaani mweusi) kutokana na ukweli kwamba mama yake Sabiikah alikuwa akitoka kwenye miji ya Unubi.

Kwa hakika Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mungu autukuze utajo wake) amepokea na kusimulia kutoka kwa Ali bin Ibrahiim, kutoka kwa baba yake, kutoka kwa baadhi ya maswahibu zake kwamba: Pindi Mutawakkil alipopewa sumu (yaani Khalifa wa bani Abbas) aliweka nadhiri kwamba kama angepona, angetoa sadaka ya mali nyingi. Alipopona, aliwauliza wanazuoni wa fiqhi kuhusiana na kiwango cha mali nyingi wakatofautiana juu ya hilo. Baadhi yao wakasema: Laki moja na wengine wakasema: Ni elfu kumi, na wakamwambia kauli tofauti kuhusiana na suala hilo. Basi jambo hilo likamtatiza na mtu mmoja kati ya wake wa karibu aliyekuwa akitwa Swafwaan akasema: Je, hutumi ujumbe kwa huyu mtu mweusi na kumuuliza kuhusiana na jambo hili? Mutawakkil akamwambia: Ole wako! Unamkusudia nani? Akamwambia: Mtoto wa Ridhwa.[1] Akamwambia: Je, yeye ana chochote au kauli nzuri zaidi kuliko kauli hizi? Akasema: Ikiwa atakutoa kwenye utata huu basi nina haki kutoka kwako ya kitu fulani na fulani (kadha wa kadhaa), la sivyo nipige fimbo au bakora mia moja. Mutawakkil akasema: Nimeridhia. Ewe Jaafar bin Mahmoud! Nenda kwake na muulize kuhusu kiwango cha mali nyingi. Jaafar bin Mahmoud akenda hadi

[1]-Akimuashiria Imam Ali al-Hadiy (AS) mtoto wa Imam Muhammad al-Jawad (AS) mtoto wa Imam Ali Ridhwaa (AS).

kwa Abil-Hassan Ali bin Muhammad (AS) na kumuuliza kuhusiana na kiwango cha mali nyingi naye akasema: Mali nyingi ni thamanini. Jafar akamwambia: Ewe sayyid na bwana wangu! Hakika yeye anauliza kuhusu sababu ya mali nyingi. Abul-Hassan (AS) akamwambia: Hakika Mwenyezi Mungu Aliyetakasika anasema:

ﮋ ﮊ ﮉ ﮈ ﮇ ﮆ ﮅ

"Kwa hakika Mwenyezi Mungu alikuokoeni katika sehemu nyingi"[1] na tukahesabu idadi ya sehemu zile na zilikuwa ni thamanini.[2]

Tunasema: Riwaya hii imetumiwa na wanazuoni kadhaa wa fiqhi kama ilivyoelezewa katika kitabu ad-Duruus,[3] lakini nukta muhimu ni kwamba, hakika Mwenyezi Mungu alitaka rangi ya ngozi ya Imamu wetu (AS) iwe nyeusi kwa mujibu wa yaliyoelezwa katika riwaya hii, ili iwe ni kigezo kwetu kwa kila mwenye kutaka kutufanyia istihzaa na kutuchezea shere na kuliweka mbele ya Mwenyezi Mungu aliyetukuka utajo wake.

[1]-Suuratut-Tawbah aya 25.
[2]-al-Kafiy-kitabul-Iiman wan-Nadhri wal-kaffarat-babu an-Nawaadir-h 21.
[3]-ad-Duruus juzuu 2 \ 155.

HUDAITHU MAMA WA IMAM HASSAN ASKARI (AS)

Kilicho maarufu kutoka kwa mkewe Imam Ali al-Hadiy (AS) na mama wa Imam Hassan al-Askariy (AS) ni kwamba, alikuwa ni mjakazi aliyekuwa akiitwa Hudaith au Hudaithatu, na inasemekana alikuwa akiitwa kwa jina la Saliil. Pia inasemekana ya kwamba jina lake lilikuwa ni Shaklu an-Nuubiyyah yaani kutoka katika miji ya Unubi iliyoko Afrika, na inasemekana ya kwamba jina lake lilikuwa ni Susan kutoka Moroko.[1]

Kwa itakavyokuwa, lililo dhahiri ni kwamba, mjakazi huyu alikuwa akitokea kwenye bara la Afrika na alikuwa amefikia katika kilele cha ucha Mungu na kujihifadhi. Katika mji wake alikuwa ni miongoni mwa watu watukufu zaidi na yatutosha katika fadhila zake ya kwamba, yeye alikuwa ni kimbilio na marejeo ya mashia baada ya kufariki dunia Imam Hassan al-Askariy (AS).[2]

Na imepokelewa kutoka kwa Masoudiy (Mwenyezi Mungu autukuze utajo wake aliyefariki dunia mwaka 346 Hijiria) amesema: Imepokelewa kutoka kwa al-Aalim (AS) (yaana Imam Jawaad (AS)) ya kwamba amesema: Pindi (Saliil) mama wa baba yangu Muhammad (AS), Ali Abil-Hassan (AS) akasema: (Saliil) ni mwenye kuvuliwa na kukombolewa kutokana na mitihani na mabalaa ya kimaumbile na uchafu na najisi mbali mbali.

Kisha akamwambia: Mwenyezi Mungu atampatia Hujja wake juu ya viumbe wake atakaeijaza ardhi kwa uadilifu kama ulivyojawa ujeuri na uovu.[3]

[1]-Angallia:ad-Durrun-Nadhiim:ukurasa 738 - na yawezekana kukusanya kati ya majina haya kwa upande wa zama na mahala na Uislamu na kabla yake kama ilivyokuwa ikijulikana katika zama zile.
[2]-Angalia kitabu Muntahal-Amaal, juzuu 2 \ 650.
[3]-Ithbatul-Waswiyyah-ukurasa 244.

NARJIS MAMA WA MTAWALA WA ZAMA HIZI
IMAM WA KUMI NA MBILI

(Mwenyezi Mungu Aharakishe Kudhihiri Kwake)

Ilivyo maarufu ni kwamba, mama wa Imam al-Hujjah al-Mahdiy mwenye kusubiriwa (al-Muntadhar)m Mwenyezi Mungu Mtukufu aharakishe kudhihiri kwake, alikuwa ni mjakazi aliyenunuliwa na Imam Ali al-Hadiy (AS) kwa ajili ya mwanawe Hassan al-Askariy (AS) na jina lake lilikuwa ni Narjis. Pia inasemekana kuwa alikuwa akiitwa Susan au Souzan.[1] Inadhihiri kutokana na baadhi ya habari ya kwamba, yeye alitokea katika miji ya Afrika. Kwa mfano, Shekh mtukufu Muhammad bin Ibrahiim an-Nuumaniy (mmoja kati ya wanazuoni wa karne ya nne Hijiria) amepokea hadithi na kusema: Tumefahamishwa na Ahmad bin Muhammad bin Saidi bin Uqdah amesema: Tumehadithiwa na Muhammad bin Mufadhal bin Qaisi bin Rumanah al-Ash'ariy, na Suadan bin Is'haaq bin Saidi, na Ahmad bin al-Hussein bin Abdul-Malik, na Muhammad bin Hassan al-Qut'waaniy wote wamesema: Tumesimuliwa na Hassan bin Mahboub az-Zarraad kutoka kwa Hisham bin Saalim kutoka kwa Yazid al-Kannaasiy amesema: Nilimsikia Aba Jaafar Muhammad bin Ali al-Baaqir (AS) akisema: Hakika mwenye jambo hili (Utawala na Uimamu) ana mshabaha na kufanana na Yusuf. Ni mtoto wa mama mweusi, Mwenyezi Mungu Aliyetakasika atamsuluhishia na kumtengenezea mambo yake katika usiku mmoja. Kisha akasema: an-Nuumaniy: Anakusudia kufanana na Yusuf

[1]-Angalia: Ad-durrun-nadhiim-ukurasa 753.

katika ghaibah (kuwa ughaibuni).[1]

Tunasema: Kauli yake (SAW): Mtoto wa mjakazi au mtumwa wa kike aliye mweusi ndio mahala pa ushahidi, na Mwenyezi Mungu ndiye ajuae ukweli na uhakika wa mambo.

Pamoja na hayo, kwa hakika Narjisi alifahamika kwa usafi na ukweli, kwani alikuwa akikataa kuanikwa kwa ajili ya maonyesho na kuguswa na mnunuzi na kukataa kumtii aliyekuwa akijaribu kufanya hivyo. Alikuwa akisema kuwambia baadhi ya wanunuzi kwa Kiarabu: Lau kama ungejitokeza ukiwa katika vazi la Suleiman bin Daudi (AS) akiwa juu ya ufalme wake, kamwe kusingejitokeza na kuonekana mapenzi yangu kwako (yaani nisinge kupenda).[2] Hadi aliponunuliwa na Imam Ali al-Hadiy (AS) kwa ajili ya mwanawe Hassan al-Askariy (AS) na kumzalia mtoto anayeunganisha ardhi na mbingu, mwenye kuwatukuza mawalii na mdhalilishaji wa maadui, ambaye atadhihir na kuijaza dunia kwa uadilifu na usawa baada ya kujawa na dhulma na ujeuri (kiburi).

[1]-al-Ghaibah cha Nuumaniy ukurasa 228.
[2]-Angalia: al-Iiqaad ukurasa 251.

KUTOKEA KWA KUNDI LA WATU WEMA MIONGONI MWA WAAFRIKA PAMOJA NA IMAM Al-QAAIM (AS)

Kwa hakika kuna riwaya nyingi kutoka kwa Maimu wa Ahlul-Bait walio maasumu na watwaharifu (AS) zinazothibitisha na kujulisha kwamba, idadi ya maswahaba wa Imam Mahdi Mwenyezi Mungu aharakishe kudhihiri kwake (AF) ni mia tatu kumi na tatu, idadi ya wapiganaji wa Badri, na kwamba wao watatoka katika sehemu tofauti ulimwenguni.[1] Imeelezwa katika baadhi ya riwaya hizo ya kwamba, baadhi yao wanatokana na kabila la Wanubi lililoko Afrika.

Na Thiqatul-Islaam al-Kulainiy (Mungu autukuze utajo wake aliyefariki dunia mwaka 328 Hijiria) amepokea hadithi na kusimulia kutoka kwa Ali bin Ibrahiim kutoka kwa Ismaili bin Muhammad al-Makkiy kutoka kwa Ali bin al-Hussein kutoka kwa Amru bin Othuman kutoka kwa al-Hussein bin Khalid, kutoka kwa aliyemtaja, kutoka kwa Abi Rabii'i ash-Shamiy amesema: Abu Abdillahi (AS) aliniambia: Litatoka pamoja na al-Qaaim atokanaye na sisi kundi la watu miongoni mwao (yaani miongoni mwa watu wa kabila la Nuubah (Wanubi).[2]

Pamoja na hayo, Sayyid Radhwiyud-Dini Abul-Qassim Ali bin Musa bin Jaafar bin Muhammad bin Twawuus (Mwenyezi Mungu autukuze utajo wake, aliyefariki dunia mwaka 660 Hijiria) amesema: Kitengo kuhusiana na

[1]-Angalia kitabu Nawaadirul-Akhbar ukurasa 269.

[2]-al-Waafi juzuu21 mlango wa 18 h 5 ukurasa 114-Wasaailush-Shiah, juzuu 14, babu 32 min abwaab muqaddimaatin-nikaah wa adaabuhu-h 1 ukurasa 56.

tuliyoyaona kati ya riwaya zielezeazo idadi ya maswahibu wa al-Qaaim (AS), na kubainisha sehemu zao kutoka kwenye barua au kitabu cha Yaaqub bin Nuaim bin Qurqaarah mwandishi Abi Yuusuf.

Najashi amesema: Ambaye alisifiwa kwa sifa njema na Muhammad bin Najjar-: Hakika Yaaqub bin Nuaim – aliyetajwa - amepokea kutoka kwa Ridha (AS), na alikuwa ni mtukufu kati ya maswahibu zetu na mkweli (Thiqah).

Kisha Ibnu Twawus Mungu autukuze utajo wake akasema: Na tuliona kati ya riwaya tulizozinukuu katika kopi ya zamani huenda iliandikwa katika uhai wake, na juu yake kukiwa na hati ya Said Fadhlullah ar-Rawandiy Mwenyezi Mungu azitukuze roho zao, na akasema maneno yenye lafdhi zifuatazo: Nimesimuliwa na Ahmad bin Muhammad al-Asadiy kutoka kwa Said bin Janah kutoka kwa Mas'adah, ya kwamba, Aba Baswiir amesema kumwambia Jaafar bin Muhammad (AS): Je, Amirul-Muuminiin alikuwa akifahamu sehemu na mahali watakapotokea sahaba wa al-Qaaim kama alivyokuwa akifahamu idadi yao?

Jaafar bin Muhammad (AS) akajibu: Ndio, Wallahi, anawafahamu kwa majina yao na majina ya baba zao mmoja mmoja, na sehemu za nyumba zao.

Akasema: Nifanywe kuwa fidia yako, yote aliyoyafahamu Amirul-Muuminin, Hassan pia aliyafahamu, na yote aliyoyafahamu Hassan yalihamia kwa al-Hussein naye kuyafahamu, na yote aliyoyafahamu yalihamia kwenu nanyi kuyafahamu? Nifanywe kuwa fidia yako, nifahamishe sifa zao kwani twahitaji kuzifahamu. Jaafar (AS) Akasema: Itakapofika siku ya Ijumaa baada ya swala njoo kwangu (nijie). Nikamwendea, na akasema: Yuko wapi sahibu wako

ambaye hukuandikia? Nikasema: Amepatwa na shughuli, na nilichukia kuchelewa kunako wakati wa haja yangu. Akasema (AS) kumwambia mtu mmoja: Muandikie: Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehma Mwenye kurehemu: Haya ndiyo mambo aliyomwambia Mutme wa Mwenyezi Mungu Ali Amiril-Muuminiin na kuyaweka kwake kama dhamana au akiba. Yanahusiana na kutaja majina ya As'habi wa Al-qaaim na idadi ya watu ambao watamlinda kati ya watu waliohama na kukosekana kwenye matandiko yao (wasiolala), na watakao tembea kwenda Makkah usiku, na watafanya hivyo pindi watakaposikia sauti katika mwaka ambao atadhihiri na kuonekana ndani yake amri ya Mwenyezi Mungu Aliyetakasika. Nao ni wateule, mafaqihi na watawala wa watu. .....Na kutakuwa na mtu mmoja atakayetokea kwenye mji wa Balbaliis,[1] mwingine kutoka katika mji wa Dimiyaat,[2] mwingine kutoka Us'waan,[3] wanne kutoka Fustwaat,[4] wawili kutoka mji wa Qulzuum,[5]...mmoja kutoka katika mji wa Tarablos (Tripoli),[6] na wawili kutoka Qairawaan. Basi hawa ndio watu mia tatu na kumi na tatu, wote kwa pamoja Mwenyezi Mungu atawakusanya katika mji wa Makka katika usiku mmoja, na usiku huo ni usiku wa Ijumaa. Wataamka

[1]-Bal-biis kati ya mji huo na mji wa Fustwaat wa Misri kuna takriban kilomita 60.
[2]-Dimyaat ni mji wa zamani ulioko kati ya Tuniyyis na Misri upande wa kati ya bahari ya Rum na Mto Nile.
[3]-Us'waan ni mji mkubwa ulioko mwishoni mwa mipaka ya Misri na mwanzoni mwa ardhi ya Unubi.
[4]-al-Fistwaat: ni mji wa kwanza ulioanzishwa na Waislamu katika nchi ya Misri katika ukingo wa Mashariki wa Mto Nile.
[5]-al-Qulzuum: ni mji ulioko katika ukingo wa bahari ya Yemen karibu na Ailah na Tuur na Madyan kati ya miji ya Misri.
[6]-Twaraablos: ni jina la miji mingi mmoja wapo ni ule ulioko Libya.

wakiwa Makka katika Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu. Hakuna yeyote miongoni mwao atakayekwenda kinyume na kutofika... Abu Baswiir akasema: Nifanywe kuwa fidia yako, je, hakuna juu ya ardhi muumini tofauti na hawa? Akasema (7): Ndio lakini hili ndiyo idadi na kundi ambalo ndani yake atakuwepo al-Qaaim, nao ni wateule, mafaqihi, na mahukama (watu wenye busara), na ni mahakimu ambao yatapanguswa matumbo yao na migongo yao na hakuna utawala wowote utakaowatatiza.[1]

Tunasema: Riwaya hii imesimuliwa na kupokelewa pia naTwabariy Abu Jaafar Muhammad bin Jariir bin Rastam lakini ikiwa tofauti kidogo. Imeelezwa kwenye riwaya hiyo:...Na kutokea kwenye mji wa Balbiis mtu mmoja, Dimyaat mtu mmoja, kutokea As'waan mtu mmoja, kutokea Fistwaat watu wanne, kutokea Qairawaan watu wawili, ...na kutokea Qaabis mtu mmoja[2]... na kutokea Twarablos watu wawili, kutokea Qulzuum watu wawili, kutokea al-Qubbah mtu mmoja[3]... Na kutokea Twihnah mtu mmoja...hao ndio watu mia tatu kumi na tatu, idadi ya wapiganaji wa Badri Mwenyezi Mungu atawakusanye katika mji wa Makkah katika usiku mmoja, nao ni usiku wa Ijumaa... nk.[4]

Na Alfadhlu bin Shaadhaan amepokea kutoka kwa Muammar bin Khallad, kutoka kwa Abil-Hassan (Ar-

[1]-at-Tashriifu Bilminan fit-Taarifi bil-Fitan, kilicho maarufu kwa jina la: al-Malaahim wal-Fitan cha Sayyid ibn Twawus ukurasa 375 hadi ukurasa 380 - chapa ya Muassasatu Swaahibul-Amri (Mwenyezi Mungu aharakishe faraja yake)- Iran-Isfahan.
[2]-Qaabis: Ni mji ulioko kati ya Twarablos na Safaaqis ulioko ukingoni mwa Bahari.
[3]-al-Qubbah: Ni sehemu kati ya Bahraini na Misri na Iskandariyyah.
[4]-Makaatibur-Rasuul (SAW) juzuu 2 \ 302 kutoka kwenye kitabu Dalaailul-Imaamah cha Twabariy ukurasa 554.

Ridhwa) (AS) amesema: Kana kwamba mimi ninaona bendera kutokea Misri zikija zikiwa zimepakwa rangi ya kijani, hadi kuja na kufika kwenye miji ya Sham na kutolewa zawadi kwa mtoto wa Swashibul-Waswiyyaat.[1]

Tunasema: Huenda bendera hizi ndizo bendera zile za Mmoroko ambaye atadhihiri katika Misri na kuja katika miji ya Sham na kuitawala. Shekh Mufiid amesema kwamba: Hakika zimepokelewa na kuja habari na riwaya zikitaja alama za zama za kusimama kwa al-Qaaim al-Mahdiy (AS), dalili na matukio mbali mbali ambayo yatatokea kabla ya kusimama (kudhihiri) kwake. Na kati ya alama na dalili hizo ni:... Kudhihiri kwa Mmoroko (Mmaghribiy) katika nchi ya Misri na kudhibiti kwake miji yote ya Sham.[2]

Basi ni uzuri na furaha ilioje kwa mtu ambaye atafikia cheo hiki na kupata utukufu na heshima ya kufuatana na kuwa sahaba wa Imam (AS) kwa ajili ya kupigania na kuuhami Uislamu na kueneza uadilifu na amani katika nchi zote ulimwenguni?!

[1]-al-Irshaad- juzuu 2 \ 376.
[2]-Chanzo kilichotangulia.

ADAARISAH NA UENEZAJI WA UISLAMU ASILIA WA MUHAMMADIY KATIKA NCHI ZA AFRIKA

Huzingatiwa Idrisa bin Abdallah bin Hassan al-Muthanna bin Hassan bin Ali bin Abi Twalib (AS) na ndugu wa mashahidi watatu, Muhammad na Ibrahim na Yahya watoto wa Abdallah bin Hassan, ya kuwa ni mtu wa kwanza aliyeingia katika nchi ya Moroko kati ya watoto wa Abi Twalib na Watu wa familia ya Bani Haashim, na kuanzisha kwenye nchi hiyo dola au serikali ya kwanza iliyokuwa ikihukumu kwa mujibu wa sunna ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Na ni jambo lisilofichika kwamba, Idrisa bin Abdallah al-Haashimiy al-Madaniy alikuwa miongoni mwa maswahaba wa Imam Swaadiq (AS),[1] na kati ya watu waliopokea hadithi kutoka kwake. Hakika Sayyid mtukufu Abul-Qassim Ali bin Musa bin Twawuus al-Hassaniy al-Hilliy (Mungu autukuze utajo wake – aliyeishi kati ya miaka 460-589 Hijiria) alipokea na kusimulia kwa sanadi yake hadi kwa babu yake Abi Jaafar at-Tuusiy Mungu autukuze utajo wake (aliyefariki mwaka 460 hijria) kwa kuitegemeza hadi kwa Idrisa bin Abdallah bin Hassan kutoka kwa Jaafar bin Muhammad (as-Swaadiq) kutoka kwa baba yake (AS) amesema: Tulikuwa tukijifunza Istikharah kama tulivyokuwa tukijifunza sura moja ya Qur'an).[2]

Ala kulli haal, katika zama za Banil-Abbas, alikuwa akiishi

[1]-Muujam rijaalil-hadiith juzu 3 \ 173.
[2]-Fat'hul-abwaab ukurasa 159, kutoka kwake Wasaailush-shiah juzu 5 \ 206. h 9.

katika mji wa babu yake Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW). Isipokuwa ni kwamba bin Ali bin Hussein bin Hassan bin Ali bin Abi Twalib (AS), pindi alipoona utawala wa bani Abbas ukikengeuka, kwenda kinyume na mafundisho ya Uislamu na kufuata upotovu, alitoka pamoja na kikundi cha watu wa nyumbani kwake miongoni mwao wakiwemo (Idrisa na Yahyaa), na kuudhibiti mji wa Madinah na kumfukuza mtumishi wa (al-Hadi al-Abbas) kutoka kwenye mji huo. Ulikuwa ni msimu wa haji, akatoka yeye na maswahaba zake kwenda hija, hadi walipofika mahali fulani karibu na Makkatul-Mukarramah paitwapo 'Fakh.' Mtawala wa Kibani Abbas akawatumia jeshi akaweka kati yao majambia au mapanga kupigana nao na kuuwa watu wengi au na kati yao kukiwa na kiongozi wao. Siku hiyo ilikuwa ni siku ya tarwiya (mapumziko) mwaka 170 Hijiria na akaokoka miongoni mwao Idrisa bin Abdallah na Yahyaa bin Abdallah.

Na pindi Idrisa alipookoka kutokana na mauaji ya halaiki ya Fakh akauelekeza uso wake upande wa Afrika na akafika Moroko na akaingia mjini Lailaa na akafikia kwa mkuu wa mji huo aliyekuwa akiitwa Abdul-Hamiid bin Is'haaq al-Uruubiy. Hiyo ilikuwa ni mwishoni mwa mwezi wa Rabiul-Awwal mwaka 172 Hijiria (sawa na mwaka 788 Milaadia), Abdul-Hamiid akaita jamaa wa kabila lake au walezi wa nyumba yake kwa ajili ya kumpatia kiapo cha utii na hao walikuwa ndio watu wa mwanzo kumpa baia siku ya Ijumaa tarehe nne ya mwezi mtukufu wa Ramadhani mwaka 172 Hijiria. Na safari ya Idrisa iliyoanzia Hijazi hadi Moroko ilikuwa imejawa na matatizo na mabalaa hatari kiasi kwamba kulikuwa na ihtimali ya kuangukia kutumbukia

katika mikono ya watu waliokuwa wakimfuatilia na kumtafuta wakati wowote ule.

Pamoja na haya, alifuatana katika msafara huu wa mbali na mtwana wake Raashid (muongozaji) ambaye alikuwa na fadhila kubwa katika kufanikiwa kwa safari kisha baadaye katika kufaulu kwa dola na utawala wake.

Walitoka pamoja kwa kujificha na kujisitiri wasionekane katika kundi la mahujaji wa Misri na Afrika. Wakiwa Misri, hali yao ilifichuka na kubainika kwa baadhi ya watumishi wa dola na wakawahami na kuwahifadhi na hapo safari yao kuwa nyepesi hadi walipofika kwenye miji ya Moroko.[1]

Kwa hakika Idrisa na muongozaji wake (Raashid) walifika Moroko ya mbali wakivuka bonde la Taazah hadi wakafika mahala paitwapo Twanjah.[2] Wakakaa kwenye mji huo kisha akahamia kwenye mji wa Walaila huko Moroko na yalikuwa yakiishi kwenye mji huo makabila ya Barbariyyah yaliyokuwa na nguvu kubwa, yakitanguliwa na kuongozwa makabila yote hayo na kabila la Yurobah (Orubah) likiongozwa na Abdul-Hamiid bin Is'haqa tuliyemuelezea hapo kabla. Idrisa akenda kwake na kufikia kwake kama mgeni, na akakuta kuwa ni mtu mwenye wasaa aliyemkaribisha na kupokea fikra zake - hivyo ndivyo afanyavyo kila mtu mwenye fikra huru - basi yeye akampa baia na kabila lote kumpa baiah. Kisha makabila yaliyokuwa jirani pia yakampa baiah, yakiwemo makabila ya Zanaatah, Zawaaghah, Zawaawah, Lamaayah, Sadraateh, Masraateh, Nafrah, Maskanah na Ghamarah.[3]

---

[1]-Angali kisa chote katika kitabu: Maqaatilut-Twaalibiin ukurasa 324-chapa ya Darul-Kitaab-Qumil-Muqaddasah.

[2]-Ni mji ulioko Moroko katika mkondo wa mlima wa Twaariq.

[3]-Angalia:Dairatul-Maarifil-Islaamiyyah ash-Shi'iyyah-juzuu 1 \ -madda al-Adaarisah.

Na baada tu ya kupewa baiah na makabila yale yaliyokuwa huru, akatangaza wito wake kwa kutoa khutba nzuri na ya kuvutia ambayo haikuwahi kusikiwa mfano wake kati ya khutba zilizowahi kutoklewa kabla yake na akasema, (Mungu amrehemu) kwenye khutba hiyo: 'Bismillahir-Rahmaan Rahiim. Sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu ambaye ameufanya ushindi kwa mwenye kumtii na mwisho mbaya kwa mwenye kumpinga. Hapana Mungu wa haki illa Mwenyezi Mungu wa pekee na mmoja mwenye kuthibitisha hilo kwa yale mambo ya ajabu aliyoyadhihirisha kati ya hekima zake na uzuri wa upangiliaji wake ambaye hafahamiki isipokuwa kwa alama zake. Rehma za Mwenyezi Mungu na amani ziwe juu ya Muhammad mja na Mtume wake na mbora wake katika viumbe wake aliyempenda na kumchagua na kumteua na kumridhia. Rehema za alla ziwe juu yake na ziwe juu ya jamaa zake walio wema.

Ama baad: Hakika mimi ninakuiteni kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Sunna ya Mtume wake juu yake rehama na amani na jamaa zake, na ninakuitieni kuwafanyia uadilifu wananchi na kugawa mali kwa usawa, na kuondoa dhulma na kumshika mkono pia kumsaidia aliyedhulumiwa, kuhuisha Sunna na kuitokomeza bidaah na kutekeleza hukumu za Kitabu kwa mtu wa karibu na wa mbali. Mkumbukeni Mwenyezi Mungu katika wafalme waliobadilisha na walioifanyia khiyana amani na ahadi za Mwenyezi Mungu na wakazikhalifu ahadi zake na wakakiua kizazi cha Mtume wake. Ninakukumbusheni Mwenyezi Mungu katika wajane waliodharauliwa. Na hukumu za sheria walizozisimamisha na kuziatwilisha na katika damu zilizomwagwa bila ya haki. Kwa hakika walikiacha na kukitupa Kitabu na Uislamu na hakukubakia katika

Uislamu isipokuwa jina lake, wala hakikubakia katika Qur'ani aisipokuwa maandishi yake.

Na fahamuni enyi waja wa Mwenyezi Mungu ya kwamba, hakika miongoni mwa mambo aliyoyawajibishia Mwenyezi Mungu kwa watu wenye kumtii ni kuwapiga jihadi watu wenye kumfanyia uadui na kumuasi kwa mkono na ulimi. Kwa ulimi ni kuwalingania kwenye njia ya Mwenyezi Mungu kwa mawaidha mazuri na kuwanasihi na kuwahimiza kumtii Mwenyezi Mungu, na kutubia kutokana na madhambi na huko ndiko kurejea na kujivua na kujitoa kwenye mambo ayachukiayo Mwenyezi Mungu Aliyetakakasika, kuusiana kwenye mambo ya haki na ukweli na subira na reham au kuhurumiana na upole na kuzuiana au kukatazana kufanya maasi yanayomuudhi Mwenyezi Mungu. Vilevile kujifunza na kumtanguliza aliyemuitikia Mwenyezi Mungu na Mtume wake hadi macho yao yaweze kuona vema na kukamilika na kuungana kwa neno lao, yaani kuwa na mashikamano na umoja wao kuundika. Ikiwa wataungana miongoni mwao wenye kuupinga ufisadi, mwenye kupambana na madhalimu, mwenye kuushinda uovu na uadui hapo watadhihirisha wito wao na kuwaita au kuwalingania waja kwenye twaa'ah ya Mola wao, kuwapinga madhalimu kutokana na kufanya kwao mambo yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu na kusimama dhidi ya watu wafanyao maasi. Hakika katika kumuasi Mwenyezi Mungu kuna uharibifu kwa mwenye kuufanya na maangamio kwa mwenye kuutenda. Msikatishwe tamaa kuhusiana na kushinda kwa haki na kudhihirishwa kwake na na walio wachache. Hakika kati ya mambo aliyoanza nayo Mtume (SAW) akiwa peke yake na mitume wengine pia waliofuata njia ya Mwenyezi Mungu kabla yake na wingi

wa wasaidizi kwao baada ya udhalili, ni dalili na uthibitisho wa wazi kabisa kuhusiana na suala hilo.

Amesema Mwenyezi Mungu Aliyetakasika:

ٺ ڏ ڏ ٽ ٽ ٽ

"Na kwa hakika Mwenyezi Mungu alikunusuruni katika (vita vya) Badri hali ya kuwa nyinyi ni dhaifu."[1] Na amesema:

ڇ ڇ ڇ ڇڇ ڇ ڇ ڍ ڍ

"Na Kwa hakika Mwenyezi Mungu atamnusuru mwenye kumnusuru (anayesaidia dini yake). Hakika Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na Mwenye kushinda).[2]

Na hapo Mwenyezi Mungu akamnusuru Mtume wake na jeshi lake kulifanya kubwa (kuwafanya wengi majeshi yake) na kulidhihirisha kundi lake na kutekeleza ahadi yake, yakiwa ni malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Aliyetakasika na thawabu kwa ajili ya fadhila yake, subira yake, kujitolea na kuitanguliza twaa ya mola wake, upole wake kwa waja wake na rehma yake au upole wake kwake, uzuri wa kisimamo chake kutekeleza uadilifu, usawa katika malezi na kuwapiga jihadi maadui zake, ucha Mungu wake katika mambo yale aliyomtaka ayafanyie zuhdi, mapenzi yake kwenye mambo aliyompendelea na kuyatekeleza, kuwaliwaza kwake maswahaba wake, upana wa tabia yake, kama alivyoadabishwa na Mwenyezi Mungu na kuwaamuru waja kumfuata, kufuata njia na muongozo wake na kufuatilia athari zake. Ikiwa watafanya hivyo atayatekeleza kwa ajili yao aliyowaahidi kama alivyosema Mwenyezi Mungu mwenyewe:

[1]-Aali-Imraan: aya 123.
[2]-Suratul-Hajji: aya 40.

ۋ ۋ ۋ ۇ ۇ ۇ

"Ikiwa mtamnusuru Mwenyezi Mungu (mtainusuru dini yake naye) atakunusuruni na kuiimarisha miguu yenu."[1] Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

"Na saidianeni katika mambo mema na ya ucha Mungu na wala msisaidiane katika madhambi na mambo ya uadui",[2] na amesema:

ڇ ڇ ڇ ڇ ڇ ڇ ڍ ڍ ڏ ڏ ڏ

"Hakika Mwenyezi Mungu anaamuru kufanya uadilifu na hisani na kuwapa watu wa karibu (jamaa) haki zao na anakataza kufanya maovu na mabaya".[3] Pia anasema Mwenyezi Mungu:

ٺ ٺ ڏ ڏ ٽ ٽ ٽ ٽ ٽ ٽ ٽ

"Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishiwa watu (ulimwenguni) - mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu",[4] na amesema Mwenyezi Mungu Aliyetakasika:

ڪ ڪ ڪ ڪ ڪ

"Na waumini wa kiume na waumini wa kike ni marafiki wao kwa wao",[5] na akaamrisha mema na kukataza mabaya, ukiongezea kuamrisha kushikamana na imani na kukiri maarifa yake, kuamrisha jihadi kwa ajili yake na kuwalingania watu kwake. Mwenyezi Mungu Mtukufu

[1]-Suurat-Muhammad: aya 7.
[2]-Suuratul-Maaidah:aya 2.
[3]-Suuratun-Nahli aya 90.
[4]-Suurat-Aali-Imraan aya 110.
[5]-Suratu-Tawbah aya 71.

amesema:

ک ڑ ڑ ژ ژ ڈ ڈ ڈ

wa Mwenyezi Mungu (SAW) ni baba zangu, na Muhammad na Ibrahim watoto wa Abdallah al-Mahdiy na Zakiy ni ndugu zangu. Huu ndio wito wangu wa kiuadilifu sio wa kidhalimu. Basi mwenye kuniitikia, anayo yale yaliyo juu yangu na ni juu yake yaliyo juu yangu, na mwenye kukataa basi hadhi yake ni kuwa amekosea na atayaona hayo katika ulimwengu wa ghaiba na shahada. Hakika mimi sikumwaga damu yake na wala sikuhalalisha la haramu wala mali yoyote, na ninakushuhudisha ewe mkuu wa washuhudiao na ninamshuhudisha Jibril na Miikail ya kwamba, hakika ni mtu wa kwanza kuitika na kurejea. Ninakuitikia ewe Mwenyezi Mungu! Ewe mwenye kuigeuza milima na kuifanya kuwa mazigaziga baada ya kuwa ni madhubuti na migumu na isiyotikisika! Ninakuomba ushindi kwa ajili ya mtoto wa Nabii wako, hakika wewe ni muweza juu ya kila kitu na swala na salamu ziwe juu ya Muhammad na Aali zake. (Mwisho wa hotuba)[1]

Na baada ya khutba hii, akaanza kupangilia jeshi la utawala na dola lake lililoundwa na watu wa kabila la Barbar walio mashujaa na majemedari katika vita, na likaundika jeshi kubwa lililoilazimisha miji mingine iliyokuwa pembezoni mwake kati ya miji ya Moroko ya mbali kuwa chini yake, na hasa miji ambayo ilikuwa bado haijaingia kwenye Uislamu kama vile miji ya Taadlaa, Bahluulah, Hasuun (Fandlaandah), Madyuuqah, Qilaaa'a (Ghiyaathah) na mji wa Faazaar. Kisha likasonga mbele na kuuteka pia mji wa Tilmasaan uliko Moroko ya Kati.

Na kwa hakika Idrisa (Mungu amrehemu) katika kipindi cha miaka mitano, nao ni muda na kipindi cha utawala

[1]-Daairatul-maarifil-islaamiyyah Ash-shii'iyyah juzu 1 \ 3-4 baabul-adaarisah.

wake, aliweza kuufikisha Uislamu wa asili wa Muhammad kwa wananchi wengine wa miji hiyo hata kwenye sehemu ambazo Uislamu haukuwa umefika huko hata chembe. Aliweza kusimamisha dola la Kiislamu lililosimama kwenye nguzo za uadilifu na usawa kati ya watu wote.

Lakini kifo chake hakikumruhusu abakiye zaidi ya muda huo, kwani alifariki kwa sumu kutokana na vitimbi vya Haroun Rashiid khalifa wa utawala wa Bani Abbas,[1] na kuzikwa kwenye makaburi ya Walailaa, eneo ambalo mji wake mkuuu ulibakia ukiwa chini ya mlima Zahrouun ulio karibu yake.

Idrisa (Mungu amrehemu) alioa mwanamke mwema wa kabila la Barbari aliyekuwa akitwa Kanzah na alikuwa ni mja mzito wakati mumewe alipoaga dunia. Raashid ambaye tumemtaja hapo kabla kati ya wazee na washauri (halli wal akdi) akatoa pendekezo la kuwa wamsubiri mtoto atakayezaliwa. Ikiwa atakuwa ni wa kiume watampa utawala na ikiwa ni msichana hapo watafanya maamuzi kama watakavyoona, na wakakubali pendekezo hilo.[2]

Imesemekana ya kwamba watu wa Moroko waliweka taji na (kofia ya kifalme) juu ya tumbo la mwanamke yule na kuzaa baada ya miezi minne mtoto wa kiume na kumuita kwa jina la Idrisa bin Idrisa bin Abdallah. Zilifichika habari na mazungumzo kuhusiana na idrisa mtoto wa Idrisa kwa baadhi ya watu kutokana na kuwa mbali nao, na wakamnasibisha kwa bwana wake Raashid na kwamba alifanya hila katika hilo ili ufalme ubakie kwake, na kwamba Idrisa bin Abdalla hakuwa na mtoto.

[1]-Angalia: AL-kaamilu fiit-tariikh cha ibni Athiir juzu 6 \ 93.

[2]-Dairatul-maarifil-islaamiyyah Ash-shii'iyyah-juzu 1 \ mada: Al-adarisah.

Hii ni katika hali ambayo Daud bin Qaasim Al-Jaafariy - huyu ni mmoja wa wanazuoni wakubwa na ambaye alikuwa na elimu na maarifa ya nasabu - alisimulia ya kuwa alikuwepo kwenye kisa hiki na kuzaliwa mtoto Idrisa bin Idrisa katika tandiko la baba yake. Na akasema: Nilikuwa pamoja naye Moroko na sikuona mtu aliyekuwa shujaa zaidi yake wala mwenye uso mzuri wala mwenye nafsi ya ukarimu zaidi yake.[1]

Kuhusiana na haya imepokelewa kutoka kwa Imam Ali bin Musa Ar-Ridha (AS) ya kwamba amesema: Mwenyezi Mungu amrehemu Idrisa bin Idrisa bin Abdallah, hakika yeye alikuwa ni mteule wa Ahlul-Bait na shujaa wao. Wallahi! Hakuachwa yeyote kati yetu mfano wake.[2]

Ala kulli hali, hakika Raashid alisimamia usia wake hadi alipofariki mwaka 186 hijria (sawa na 802 Milaadia) na utawala wake ukahamia kwa Abi Khaalid al-Abdiy.

Na pindi Idris wa pili alipofikia umri wa miaka kumi na tatu (13) watu wakampa baiaa. Kisha akapewa baia tena katika mji wake mkuu mpya Fas mwka 192 Hijiria (sawa na 808 Milaadia), nao ni mji alioujengwa baada ya mji mkuu wa kwanza Lailaa kuwa finyu na mdogo.

Kisha utawala wake ukapanuka na kuingia kwenye mji wa Nafiisna mji wa Ughmaat na sehemu zingine.

Kwa hakika Dola na utawala wa Adaaridah uliendelea kuanzia mwaka 172 hadi 375 Hijiria, na amesema Siidyu katika kitabu Taarikhul-Arab: Utawala wa Adaarisa uliendelea kutawala sehemu zake ulizozitawala na kukaa kwenye miji hiyo na kuanzisha mji wa Faas, ambao msikiti wake baadaye ulikuwa msikiti wenye kutukuzwa na

[1]-Angalia: Sirrus-Silsilatil-Alawiyya ukurasa 13.
[2]-Chanzo kilichotangulia.

kuheshimiwa na watu wote wa karibu na misikiti huo, na kupata umashuhuri mkubwa katika muda mfupi tu. Mji wa Faas ukajengwa ndani yake Mashule na maktaba mbali mbali, vitu ambavyo vilikuwa sambamba na harakati ya kukua kwa elimu ambayo bendera yake ilibebwa na Banil-Abbas katika upande wa Mashariki, na ikawa ni hazina kubwa na pana kati ya Waarabu wa Hispania na Waarabu wa Afrika.[1]

Hakika kusimama kwa Dola la Adaarisah huko Moroko kulipelekea kupatikana kwa natija na au faida nyingi nzuri. Hii ni kwa sababu mambo yaliyotokea kwenye kipande kile cha ardhi kabla ya dola la Adaarisa hayakuweza kuuthibitisha na kuuzatiti Uislamu kwenye sehemu hiyo na yalizuia kuenea kwa Uislamu ueneaji ulio mpana zaidi.

Na kwa fadhila za Adaarisa Uislamu uliweza kuenea hadi kufika kila sehemu. Kwa fadhila zao watu wengi wa kabila la Barbar ambao hawakuwa Waislamu mwanzoni wakaingia kwenye Uislamu hata katika zama za Idrisa wa Kwanza. Harakati kubwa ya kielimu ilianzishwa na shule na maktaba kujengwa. Kama ambavyo ujenzi wa majumba ulienea, jambo ambalo lilipelekea kupanuliwa na kupendeza.

Na lau kama wasingekabliwa mazingira magumu ambayo yaliwazunguka na kuzibana juhudi na hima yao madhubuti basi wangekuwa na hadhi kubwa katika utekelezaji wa mambo hayo ya ujenzi.

Kazi kubwa ambayo waliifanya hao Maidrisa na ambayo wanapaswa kusifiwa kutokana nayo ni kueneza kwao Uislamu kati ya makabila ya Barbari na kuiimarisha nguzo za Uislamu kwenye makabila hayo, hadi yakawa ni makabila yenye nguvu na hadhi na yenye kuutetea Uislamu

[1]- Daairatul-maarifil-islaamiyyah Ash-shiiyyah juzu 1 \ mada Adaaisa

nchini Moroko. Mengi ya makabila hayo mwanzoni na kabla ya kuja Adaarisa hayakuukubali Uisilamu, kwa sababu watawala walioikomboa Moroko kabla ya Adaarisa walikuwa na muamala mbaya na watu wa kabila la Barbar. Lakini pindi tu Idrisa wa Kwanza, rehma za Allah ziwe juu yake, alipofika Moroko haukupita muda, akasimamisha uadilifu kati yao, akaoa kwao na baada yake, kizazi chake, hadi wakachanganyika moja kwa moja na Wabarbar..

Ilikuwa ni sababu kubwa kabisa ambayo ilisaidia kufaulu kwa wito wa Adaarisah na kabila la Barbar kujiunga na Uislamu kwa wingi kupitia kwao. Hali hii ni tofauti kabisa na muamala waliokuwa wakiupata kutoka kwa watumishi wa utawala wa Bani Umayyah na Bani Abbas kama vile dhulma kubwa na kuwatumia vibaya. Yote hayo ni mambo yaliyokuwa yakipingana na Uislamu na kuudhihirisha katika sura na picha mbaya sana na ya kutisha.

Na kwa sababu hiyo Moroko yote ya Mbali (nayo ni ile ifahamikayo hivi leo kama Jamhuri ya Moroko) na Moroko ya Kati (ambayo ni al-Jeria) na Moroko ya Chini (Ambayo ni Tunisia) zikaingia katika mkondo wa mapinduzi yasiyokoma dhidi ya watawala wale, na watu wake walio huru wakitafuta wakati wote sehemu ya kupumulia na uokovu kutokana na tawala hizo.

Kama mfano wa ufisadi uliofanywa utawala wa Bani Umayyah na muamala wao mbaya dhidi ya watu waliokuwa wakiwatawala wakiwemo watu wa kabila la Barbar, na mambo wanayoyaashiria wanahistoria kutoka kwa Yazidi bin Abi Muslim Diinar (mtwana wa al-Hajjaj bin Yusuf ath-Thaqafiy) ambaye alimfanya kuwa muandishi wake na msimamizi wa jeshi lake la polisi. Katika zama za Yazidi bin Abdul-Maliki, khalifa wa utawala wa bani Umayyah,

alimtawalisha kwenye nchi ya Moroko, na alitekeleza huko siasa za Hajjaj. Miongoni mwa matendo yake ni kwamba Hajjaj alikuwa ameweka Jizya (kodi) kwa ajili ya watu ambao walisilimu kati ya watu weusi na akaamuru warudishwe kwenye vijiji vyao katika hali ile ile waliyokuwa nayo kabla ya Uislamu (yaani waendelee kutoka Jizya na mfano wa hayo). Yazidi bin Abi Muslim akataka kufanya yale yale aliyoyafanya Hajjaj na kuyatekeleza katika kabila la Barbar kwa kulazimisha watoe jizya hata baada ya kusilimu kwao. Kiabila la Barbar likafedheheshwa na kuchukizwa na jambo hilo na wala halikulivumilia. Kwa hiyo wakampangia mipango na kukubaliana kumuua, na mwishowe wakamuua.[1]

Lakini pindi Idrisa mkubwa (Mungu amrehemu) alipofika na kusimamisha dola la Adaarisa, watu wa kabila la Barbar wakafahamu ya kuwa Uislamu ulio sahihi sio ule uliokuwa ukiwakilishwa na watawala wale waovu, na kwamba Uislamu si kitu kingine isipokuwa ni uadilifu, ukunjufu na rehma. Kwa hivyo wakawa wanaingia kwenye Uislamu makundi kwa makundi kupitia kwenye mikono ya Adaarisah, wajukuu wa Mtume Mtukufu na Amiril-Muuminiin, Imam wa uadilifu na uhuru.

Ukiyaachilia mbali haya, kwa hakika makabila ya Barbar yalirithishana hadi hivi leo imani na wilaya yao kwa Ahlul-Bait na kuwatakasia nia. Watu na kizazi cha Ali pamoja na kutofautiana vizazi vyao lakini bado ni wengi mno nchini Moroko, na bado wanaheshimiwa sana nchini humo.

Kwa hakika kilibakia kizazi cha Idrisa wa Kwanza (Mungu amrehemu) katika nchi ya Moroko hadi leo, wakiwa ni

[1]-Daairatul-Maarifil-Islaamiyyah ash-Shiiyyah juzuu 1 \ mada Adaaisa.

pamoja na Elimiyyun, al-Wazaniyyuun, Araisiyyuun, al-Shabiihiyyuun, at-Twahiriyuun, al-Juutwiyyuun, al-Umraaniyyuun, at-Tuunisiyyuun, (watu wa nyumba ya al-Qaitwuun), at-Twalibiyyuun, na al-Ghaalibiyyuun, ad-Dabaaghiyyuun, al-Kataaniyyuun, al-Shafshaawiyyuun, al-Widghiiriyyuun, ad-Dirqaawiyyuun, na az-Zakariyyuun.[1]

Na mwisho ninawausia Waislamu wote katika nchi ya Moroko, kuanzia Moroko ya Karibu hadi ya Mbali, waifanye Ijumaa ya kwanza ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, nayo ni Ijumaa ambayo ilitangazwa katika siku hiyo baia ya Idrisa wa Kwanza, kuwa ni 'Siku ya Nuru ya Mwenyezi Mungu,' kwa sababu siku hiyo, "Imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinachobainisha (kila jambo) ambacho Mwenyezi Mungu huwaongozea wenye kufuata radhi Yake katika njia za salama na kuwatoa kwenye kiza hadi kwenye nuru kwa idhini Yake, na kuwaongoza kwenye njia iliyonyooka).[2] Na msherehekee siku hiyo na msome na kutawanya kati ya watu khutba ya kwanza iliyo nzuri aliyoitoa Idrisa wa

Kwanza, Mungu amrehemu, ambapo alitangaza wito na azma yake ya kueneza Uislamu wa asili wa Mtume Muhammad (SAW) katika ardhi hizo nzuri.

[1]-Angalia: Al-aalaam cha Khairud-dini Az-zarkaliy juzu 1 \ 279.
[2]-Suuratul-maaidah aya 15-16.

KUULIWA KWA MASHIA HUKO AFRIKA

Hivi ndivyo alivyoitaja anwani hii Ibnu Athiir katika kitbu chake al-Kaamil akisema: Katika mwaka huu (yaani mwka 407 Hijiria) katika mwezi wa Muharram, waliuliwa Mashia katika nchi zote za Afrika.[1]

Kuhusiana na mauaji hayo ni kwamba, Muizzu bin Baadis[2] alitembelea mji wa Qairawaniy[3] na watu wakimsalimia na kumuombea. Mara watu fulani wakavuka na kupita, akauliza kuhusiana na watu hao. Akajibiwa: Hawa ni Marawaafidh (Mashia) wanamtukana Aba Bakri na Omar. Akasema: Mwenyezi Mungu awe radhi na Abu Bakr na Omar! Mara Masunni wote wakaondoka haraka na kwenda kwenye mlangoni wa al-Maqliy, kwenye mji wa Qairuwaani, na hiyo ni sehemu ambayo walikuwa wakikusanyika Mashia na kuwaua baadhi yao. Hilo lilifanyika kwa utashi na matakwa ya jeshi la wafuasi wao, kwa tama ya kupora mali. Na mikono ya masunni ikafunguka dhidi ya Mashia. Walifanya mauaji watakavyo, na wakadanganywa na mtumishi wa Qairawaniy aliyewachochea kufanya hivyo.

[1]-Afrika: Ni jina walilolitumia Waarabu kwa miji ya Barbar ya Mashariki, ama upande wa Magharibi ikiitwa kwa jina la Moroko (Maghribi). Jografia ya Waarabu ilitofautiana katika kuweka mipaka yake au kuelezea mipaka yake, na baadhi yao waliifikisha Moroko ya Mbali hadi Libiya. Na kwamba Afrika kwa kawaida mipaka yake inakomea katika uzio ulio mpana kidogo kutokea kwenye nchi ya Tunis ya leo.

[2]-al-Muizzu bin Badiis (398-454 Hijiria) ni mtawala atokanae na kabila la Bani Ziiriy. Alijitenga na Fatwimiyyiin na kuwaendesha watu kwa mujibu wa madhehebu ya Maaliki.

[3]- Ni mji ulioko katika nchi ya Tunisia.

Sababu yake ni kwamba alikuwa amerekebisha mambo ya mji, na akafikiwa na habari ya kuwa Muizzu bin Baadiis anataka kumuuzulu, naye akataka kumharibia na kufanya ufisadi wake. Kwa hivyo akawaua Mashia wengi, kuwachoma moto na kupora majumba yao. Wakauliwa katika sehemu zote za Afrika, na wakakusanywa miongoni mwao kwenye Ikulu ya Mansour karibu na Qairawaniy. Masunni wakawazingira huko na kuwazibia njia zote. Wakazidiwa na njaa, wakawa wanatoka na watu kuwaua hadi wakauliwa wote. Wengine walikimbilia kwenye mji wa Mahdiyyah[1] hadi kwenye msikiti mkuu na wote wakauawa kinyama huko.

Mashia walikuwa wakiitwa huko Moroko kwa jna la Mashariqah wakinasibishwa kwa Abi Abdillahi Mshia. Alikuwa akitokea maeneo ya Mashariki, na washairi wengi wameliashia tukio hili. Kuna waliokuwa na furaha ya kupindukia na wengine wakilia kwa huzuni.[2]

Tunasema: Kila mtu mwenye insafu anaposoma hadithi hii atarejea na kurudi nyuma na kuwa katika kundi la pili, yaani mwenye kulia kwa huzuni. Hiyo ni kutokana na aliyoyataja Ibnu Athir mwenyewe katika tukio hili ya kwamba: Suala si kwa sababu ya kumpenda Abubakar na Omar bali ni kutokana na tamaa ya kupora na kuiba mali.

Na pili ni kwamba mkuu wa mji wa Qairawaniy aliwachochea kufanya hivyo kwa kuogopa asiuzuliwe akataka kuharibu dini yake na dini za wengine.

Kisha hata kama tutajaalia ya kuwa uzushi huu ni wa kweli juu ya Mashia, je, walikuwa wanastahiki malipo haya

[1]-Ni mji ulioko katika nchi ya Tunisia ulioko karibu na Bahari Nyeupe. (Bhrul-Abyadhil-Mutawassit -Mediterranean).

[2]-al-Kaamil fit-Taarikh cha Ibnu Athiir juzuu 9 \ 294.

ya kuuliwa na kuchomwa moto kwa umati?! Kwa mfano, huyu hapa Muawiyah ambaye aliamuru kulaaniwa na kutukanwa kwa Amiril-Muuminiin Ali bin Abi Twalib (AS) juu ya mimbari, na bila shaka jambo hilo lilitekelezwa na kubakia Ali akitukanwa na kulaaniwa kwa muda unaokaribia miaka arubaini (40) mbele ya watu wote na juu ya mimbari au vinara vya misikiti na katika siku za ijumaa. Lakini pamoja na hayo, hatukumuona yeyote akimhukumu kama walivyohukumiwa kidhulma watu hawa walioteswa na kunyang'anywa haki zao. Naam, huenda Ali bin Abi Twalib mume wa Batuli na mkwe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (SAW) hakuwa miongoni mwa masahaba au tukayahalalisha matendo ya Muawiyah ya kwamba yeye alifanya ijtihadi na kukosea, kama alivyofanya katika vita vya Swaiffin, ambapo maelfu ya wahanga wa Kiislamu wasio na hatia walipoteza maisha yao katika vita hivyo kutokana na ijtihadi kama hiyo.

Lakini "karibuni hivi utaona na wao pia wataona. Basi subirini, hakika mimi niko pamoja nanyi miongoni mwa wenye kusubiri".

DOLA LA FAATIMIYYUN

Ni jambo lililo wazi kwamba Ushia ulipanuka na kuongezeka sana na kwa kiwango kikubwa katika miji au nchi za Afrika katika zama za Dola la Fatimiyyiin ambao nasaba yao inarudi na kurejea kwa Amiril-Muuminiin Ali bin Abi Twalib (AS) na mkewe Swiddiiqah Atwahirah Fatimah Zahra (AS), kwani utawala na dola lao ulitanda na kuendelea tokea mwaka 297 Hijiria sawa 909 Milaadia hadi mwaka 567 Hijiria sawa na 1171 Milaadia. Mwanzo wa utawala wao ulikuwa ni kwamba, Abdallah bin Muhammad al-Fatwimiy al-Alawiy,[1] mmoja kati ya wajukuu wa Imam wa Sita Jaafar bin Muhammad as-Swaadiq (AS) na aliyezaliwa mwaka 259 Hijiria sawa na 873 Milaadia na ambaye alikuwa akiishi katika mji wa as-Silmiyyah huko Syria alihamia kwa maswahibu zake ambao walikuwa wakiishi katika nchi ya Moroko. Wakakusanyika pembezoni mwake pamoja na jamaa wengine, na wakati Khalifa al-Abbasiy al-Muktafiy Billah alipomtafuta kumkamata akakimbilia kwenye mji wa Qairawaniy (huko Tunisia), na huko akapewa baia. Ilikuwa ni mwaka 297 Hijiria sawa na 909 Milaadia. Baada ya dola na utawala wake kujizatiti katika mji huo, akajenga mji wa Mahdiyyah kusini mashariki mwa mji wa Qairawaan na kuufanya kuwa mji mkuu wa dola lake.

Utawala wake uliendelea takriban kwa muda wa miaka 24, kwani alifariki dunia mwaka (322 Hijiria sawa na 934

[1]-Kilicho mashuhuri ni kwamba Jina lake lilikuwa ni Ubaidullah, lakini ilibainika kutokana na maandishi ya Dirham na Dananir zilizokuwa zikitumika wakati ule na chekeche za dufi na mizani iliyohifadhiwa katika jumba la makumbusho la al-Qairawan ya kuwa jina lake lilikuwa ni Abdallah si Ubaidullah.

Milaadia kisha mwanawe Muhammad akashika nafasi yake ya utawala na wakafuatia watawala wao ambao walifikia makhalifa kumi na nne.

Na Dola la Fatwimiyyuun likasambaa na kuenea kaskazini mwa Afrika kwani sehemu hiyo yote ilikuwa chini ya dola lao. Kisha nchi ya Misri ambayo alikombolewa katika zama za Muizzu Lidinillah ambaye alipanua mipaka ya dola la Faatwimiyyah kwenye ukingo wa bahari ya Mediterranea. Alimtuma jemedari na mkuu wa jeshi lake Jawhar bin Abdillah as-Swaqliy aliye maarufu kwa jina la al-Kaatibir-Ruumiy,[1] kwani alimuanda kwa ajili ya kuikomboa miji ya Misri.

Wakati huohuo, kiongozi huyo Jawhar alipokea uongozi wa nchi ya Misri siku ya Jumanne tarehe kumi na nane ya mwezi wa Shaaban mwaka 358 Hijiria sawa na mwaka 969 Milaadia. Akenda hadi kwenye msikiti mkongwe wa Jaamiatu Ibnu Tuuluun na akaamrisha kuadhiniwa kwenye msikiti huo kwa kuwekwa ibara isemayo 'hayya alaa khairil-amal' nayo ni sehemu ya kwanza iliyoadhiniwa kwenye adhana. Baada ya hapo ikaadhiniwa katika Jaamiul-Atiiq na kusoma kwa sauti ya juu katika swala, Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim. Na katika siku ya Ijumaa tarehe nane (8) ya mwezi wa Dhul-Qaadah, Jawhar aliamuru kuongezwa mwishoni mwa khutba ibara isemayo:

اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ الْمُصْطَفَى وَعَلَى عَلِيٍّ الْمُرْتَضَى وَعَلَى فَاطِمَةَ الْبَتُولِ وَعَلَى الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ سِبْطَيِ الرَّسُولِ الَّذِينَ أَذْهَبَ اللهُ عَنْهُمُ الرِّجْسَ وَطَهَّرَهُمْ تَطْهِيراً، اَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى الأَئِمَّةِ الطَّاهِرِينَ...

[1]-Na hilo lilikuwa ni kwa sababu yeye alizaliwa katika nchi ya Roma kisha akashikwa mateka hadi Qairuwani akiwa amemilikiwa kisha akapanda cheo hadi kufikia kuwa amiri jeshi.

Pamoja na haya alianza kukiimarisha na kukijenga chuo kikuuu cha al-Azhar[1] mwaka 359 Hijiria na kumaliza kukijenga tarehe 7 ya mwezi mtukufu wa Ramadhani mwaka 361 Hijiria.[2]

Na jambo tulitilialo umuhimu kutokana na maelezo haya ni kuwa, watawala wa Fatwimiyyiin walikuwa wakiwahamasisha maulama na mafuqaha kuweka halaqa zao za darsa katika msikiti huu wa (Jaamiul- Azhar) na kukifanya kuwa ni chuo kikuu cha elimu ambacho huzingatiwa hii leo kuwa chuo kikuu kikongwe kinachojulikana katika historia.

Ni jambo lisilofichika kwamba, tangu kuanzishwa chuo hicho, waliruhusu madhehbu mengine ukiachilia mbali madhehbu yao, kufundishwa kwenye chuo hicho na kutoa fatwa kwa mujibu wa itikadi zao. Ni kwa sababu hiyo ndio maana Doctor Mustafaa Musharrafah akasema ya kwamba: Madhehebu ya Maalikiy katika chuo cha Azhar katika dola la Fatwimiyyah yalikuwa na halaqa kumi na tano za darsa, Madhehebu ya Shaafii walikuwa na idadi hiyo hiyo na wafuasi wa Abu Hanifah walikuwa na halaqa tatu za darsa.[3]

Kwa vyovyote vile itakavyokuwa, kwa hakika barnamiji na silabasi ya chuo kikuu cha Azhar ilipanuka na kuzijumuisha elimu za nahau, lugha, bayaan, mantiki na fasihi. Mnamo mwaka 1936 Milaadia chuo kikuu hicho kikatambulika rasmi na kujumuisha vyuo vya elimu mbali mbali kama vile: sheria, usulud-din na lugha ya Kiarabu, na mnamo mwaka

[1]-Akinasibishwa kwa Sayyidah Faatwimah Zahra (AS).
[2]-Kwa ajili ya kupata maelezo zaidi na kupata matumaini rejea kitabu Wafayaatul-Aayaan cha Ibnu Khalaqaan, juzuu 1 \ 375.
[3]-Angalia:Daairatulmaarifil-Islaamiyyah Ash-shii'iyyah juzuu 3 \ 256.

1961 Milaadia, vikaongezwa vyuo vingine.

Ala kulli hal, mwenye kufuatilia kwa karibu maisha ya kifikra katika Dola la Faatwimiyyah ataona ya kwamba, utamaduni wa Kiislamu na thaqafa ya Kiislamu katika zama za Dola la Fatwimiyyiin ulifikia kwenye kilele chake, kwani walihamasisha elimu, fasihi na Falsafah na kuwaita maulamaa kwenye nchi ya Misri kutokea nchi za nje na kuwashughulisha tu na suala la elimu.

Kama ambavyo Dola la Fatwimiyuun lilijichukulia sifa ya pekee ya kuanzisha makataba mbali mbali katika Uislamu na maktaba hizo kufikia kiwango cha kustaajabisha na kukusanyika humo vitabu ambavyo hivi leo hutushangaza. Inatosha kufahamu ya kwamba maktaba ya Qasr pekee ilikuwa na vitabu laki sita na elfu moja (601000).

Hata ilifikia kwamba kwa ajili ya kuwarahisishia wasomaji katika usomaji utaliaji wao vitabu mama na vikubwa ambavyo watu wakivihitaji sana vilikuwa vikitolewa makumi kwa makumi ya nuskha. Kwa mfano, Taarikhu Tabari pekee ilitolewa nuskha (kopi) elfu moja na mia mbili (1200) ikiwemo kopi ya khatti ya Ibnu Jariir mwenyewe.

Lakini wakati alipokuja Swalahud-Din al-Ayyuubiy na kuliteketeza Dola la Faatwimiyyiin, hazina hiyo yenye thamani ikatoweka kutokana na taasub mbaya yenye kuchukiza. Alivichoma moto vitabu na hazina hiyo muhimu na kuigeuza kuwa milima, ambayo ilijulikana baadaye kama milima ya vitabu. Historia inatuarifu namna ambavyo ngozi na majalada ya vitabu hivyo yalivyokuwa yakichukuliwa na watumwa na wajakazi kwa ajili ya kutengenezea vitu kama vile viatu na kuvivaa miguuni mwao.[1]

[1]-Daaratul-maarifil-islaamiyyah ash-Shii'iyyah juzuu3 \ 256.

Naam, taasubi katika kipindi hicho ilifikia kiwango kikubwa kiasi kwamba historia inatunukulia kauli ya Faqihi al-Haafidh Muhammad bin Ahmad bin Sahl ar-Ramliy al-Falastwiniy, mmoja wa wanazuoni wa kisunni ya kwamba, alisema: Lau kama ningekuwa na mishale kumi, basi ningempiga Mrumi kwa mshale mmoja na Wamoroko[1] kwa mishale tisa.[2]

Na hii ni dhambi ya mtu aliyepatiwa fadhila kutoka kwa Mawenyezi Mungu Mtukufu. Mwenyezi Mungu anasema katika Kitabu chake chenye hekima:

"Au wanawahusudu watu kwa yale aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa ukarimu Wake? Bai tuliwapa (vilevile) watoto wa Ibrahimu Kitabu na hekima na tukawapa ufalme mkubwa"[3]

Kwa hakika mimi ninawanasihi wasomaji watukufu kupitia na kusoma kitabu kiitwacho Daairatul-Maarifil-Islaamiyyah ash-Shii'iyyah cha Sayyid Hassan al-Amiin, mada: al-Faatwimiyyuun, ili aweze kufahamu na kujionea kwa macho yake mwenyewe ukweli mkubwa na ulio wazi ambao inampasa kila msomaji mwenye kufanya utafiti wa kutafuta ukweli kuufahamu.

[1]-Na hiyo ni kutokana na watu wa Moroko kuwa Mashia katika wakati ule.

[2]- Dairatul-Maarifil-Islaamiyyah ash-Shii'iyyah juzuu 3 \ 257- ash-Shia wal-Haakimuun ukurasa 189.

[3]-Suratun-Nisaa'i aya 54.

SHEKH MTUKUFU ADBUL-AZIZ AL-JAALUDIY

MMOJA WA VIONGOZI WA MASHIA IMAMIYYAH KATIKA NCHI YA MOROKO

Ibnu Nadiim amesema katika kitabu al-Fehrest kwamba: al-Jaaludiy naye ni Ahmad Abdul-Aziiz bin Yahya al-Jaaludiy, kati ya watu wa Basra, ii Akhbariy, mwenye sira na riwaya. Alifariki dunia baada ya mwaka 330, na ana vitabu vifuatavyo:

Akhbaar Khaliid bin Swaf'waan, Akhbarul-Ajaaj na Ru'yat bin al-Ajaaj (Kitabu Majmuu Qiraa'at Amiril-Muuminiin Ali bin Abi Twalib).[1]

Na amesema mahala pengine: Abu Ahmad Abdul-Aziiz bin Yahya bin Ahmad bin Isa al-Jaaludiy, ni miongoni mwa viongozi wakubwa wa Shiah Imamiyyah, na ni mpokezi wa athari (za Mtume) na sira. Vimetajwa vitabu alivyo navyo vya sira katika sehemu yake katika makala ya Ikhbariyyiin na Nassabiin.[2] Na anavyo vitabu katika Fiqhi kama ifuatavyo:

al-Murshid wal-Mustarshid), al-Mut'atu wamaa Jaa'a fi Muhilliiha (Tahliiliha).[3]

Na mfano wa hivi vimetajwa na Shekh Tuusiy takriban katika kitabu chake kitwacho Fehrest.[4]

Na Shekh Abul-Abbas Ahmad bin Ali aliye mashuhuri kwa jina la an-Najaashiy (Mungu autukuze utajo wake - aliyefariki dunia mwaka 450 Hijiria) amesema: Abdul-Aziz bin Yahyaa bin Ahmad bin Isa al-Jaludiy al-Azdiy al-

[1]-al-Fehrest ukurasa 128.
[2]-Na hii ni ishara ya yale tuliyoyaelezea hapo kabla.
[3]-al-Fahras ukurasa 246.
[4]-Ukurasa 191-mlango:Abdul-Aziz.

Baswariy, Abu Ahmad Shekhe wa Basrah na Akhbariy wa huko Basrah, na Isa al-Jaludiy alikuwa miongoni mwa maswahaba wa Abi Jaafar (al-Jawaad (AS)), naye ananasibishwa kwa Jalud kijiji kilichoko bahrini... anavyo vitabu vilivyotajwa na watu kadhaa.

Na baada ya kutaja vitabu vyake akasema: Na hivi ni jumla ya vitabu vya Abi Ahmad al-Jaluudiy ambavyo niliviona katika Fehrestaat, na baadhi ya vitabu hivyo niliviona. Abu Abdillah al-Hussein ibn Ubaidullah akatwambia: Alitupa ijaza na ruhusa ya kuviandika vyote Abul-Hassan Ali bin Hammad bin Ubaidullah ibn Hammad al-Ad'wiy. Nilimuona Abal-Hassan bin Hammad ash-Shaair (Mungu amrehemu), na akatupa habari Abu Abdillah bin Hadyah amesema: Tumepewa habari na Jaafar bin Muhammad (Bin Qaulawaih) amesema: Tulipewa ijaza na Abdul-Aziz kuviandika vyote.[1]

Na imepokelewa kutoka kwa Thiqatul-Muhaddithiin Shekh Abbas al-Qumiy (Mungu amrehemu) amesema: Abu Ahmad Abdul-Aziz bin Yahyaa al-Baswariy, Shekhe Thiqah na mtukufu, ni miongoni mwa maulamaa wakubwa wa Shia imamiyyah, mwenye vitabu vingi mbali mbali..... alifariki dunia mwaka 332 Hijiria.[2]

Tunasema: Kutokana na yaliyotangulia tunafaidika ya kwamba shekh huyu mtukufu kituo cha safari yake kilikuwa ni Basrah japokuwa asili yake ni (Jalud) huko Afrika.

Bwana al-Jawhar amesimulia kutoka kwa al-Farraa'a ya kwamba Jalud ni kijiji kati ya vijiji vya Afrika, na katika kitabu al-Maraasid: Imeelezwa kuwa Jaalud kwa fat'ha kisha

[1]-Muujam Rijalul-hadiith juzuu 10 \ 39-42.
[2]-Hadiyyatul-Ahbaab ukurasa 167.

dhumma na sakna katika waw na daal isiyo na nukta wamesema ni kijiji kilichoko huko Afrika na imesemekana kuwa ni kijiji kilichoko huko Sham.[1]

Na kauli iliyo karibu na ukweli ni kuwa ni kitongoji kilichoko katika nchi ya Libya magharibi mwa Afrika. Kwa sababu hii baadhi ya familia katika Libya hunasibishwa siku hizi kwa kijiji cha Jaalud.

Ala kulli hal, shekh huyu mtukufu huzingatiwa kulingana na utaratibu wa matabaka kutokea kwenye zama za maswahaba wa Mtume Mtukufu (SAW) hadi zama za Shekh Tuusiy (Mungu autukuze utajo wake) (aliyefariki dunia mwaka 460 Hijiria) ni katika tabaka la tisa.[2]

Pamoja na haya, kwa hakika vitabu vilivyoandikwa na mtu huyu mtukufu na mkubwa vilizidi vitabu mia mbili (200), tutataja vingi vyake kwa ajili ya kubainisha na kuweka wazi akili ya hali ya juu ya mwanazuoni huyu navyo ni kama vifuatavyo:

1-Musnad Amiril-Muuminiin (AS). 2-Kitabu al-Jamal. 3-Kitabu Swiffin. 4-Kitabul-Hakamaini. 5-Kitabul-Gharaat. 6-Kitabul-Khawaarij. 7-Kitabu Bani Naajiyah. 8- Kitabu Huruub Ali (AS).

9-Manazala fil-Khamsah (AS). 10-Kitabul-Fadhaail. 11-Kitabu Nasabun-Nabii (SAW). 12-Kitab Tazwiij Fatwimah (AS).

13-Kitab Dhikri Ali (AS) fi Huruubin-Nabii (SAW). 14-Kitab Muhibbu Ali (AS) Waman Dhakarahu Bikhairi. 15-Kitab man Ahabba Aliyan wa Abghadhau. 16-Kitab Dhwaghaainu fii Suduuri Qawmin. 17-Kitab Man Sabbahu

[1]-Kutoka katika kitabu Tanqiihul-Maqaal juzuu 2 \ mlango: Abdul-Aziz-ukurasa 156-chapa ya Hajariyyah.

[2]-Angalia: Muujamuth-Thuqaat wa Tartiibit-Twabaqaat-ukurasa 70.

minal-Khulafaa. 18-Kitab al-Kinaayah an Sabbi Aliyyin (AS).19-Kitabut-Tfsiri Anhu.

20-Kitabul-Qirra'at. 21-Kitab maa Nazala Fiihi Minal-Qur'an.

22-Kitabu Khutwabihi (AS). 23-Kitab Shi'irihi (AS). 24-Kitab Khilafatihi (AS). 25-Kitab Ummalihi wa Wulaatihi (AS). 26-Kitab Kaulihi fish-Shuraa (AS). 27-Kitab Maakana Baina Aliyyin wa Uthman minal-Kalaam. 28-Kitab al-Mar'u maa Man Ahabba.

29-Kitab Maalush-Shia Baada Ali (AS). 30-Kitab Dhikrush-Shiah Waman Dhakarahum Huwa au Man Ahabba Minas-Swahaba. 31-Kitab Qadhwaau Aliyyi (AS). 32-Kitab Rasaailu Aliyyi (AS). 33-Kitab Man Rawaa Anhu Minas-Swahabati. 34-Kitab Mawaaidhuhu (AS). 35-Kitab Dhikru Kalaamihi (AS) fil-Malaahim. 36-kitab Maa Qiila Fiihi Minash-Shiiri wa Minal-Mad'hi. 37-Kitab Maqtalihi (AS). 38-Kitab Ilmihi (AS). 39-Kitab Qismihi (AS). 40-Kitab ad-Duaa'u Anhu (AS). 41-Kitab Allibas Anhu (AS). 42-Kitab ash-Sharabu Waswifatihi Wadhikri Sharaabihi. 43-Kitab al-Adabu Anhu (AS). 44-Kitab an-Nikaahu Anhu (AS). 45-kitab Atwalaq anhu (AS). 46-Kitab at-Tijaarati anhu (AS). 47-Kitab al-Janaaiz wad-Diyaat Anhu (AS). 48-Kitab Adhahayaa Wadhabaaihi was-Swaidi wal-Aiman wal-Kharaaj. 49-Kitab al-Faraaidh wal-Itqi wat-Tadbiir wal-Mukaatabati Anhu (AS). 50-Kitab at-Twaharatu Anhu (AS). 51-Kitab al-Huduud Anhu (AS). 52-Kitab as-Swalatu Anhu (AS). 53-Kitab as-Swiyamu Anhu (AS). 54-Kitab az-Zakatu Anhu (AS). 55-Kitab Dhikru Khadijah Wafadhlu Ahlil-Bait (AS). 56-Kitab Dhikru Faatwimah (AS) Aba Bakari. 57-Kitab Dhikrul-Hassan wal-Hussein (AS). 58-Kitab fii Amril-Hassan (AS) 59-Kitab Dhikrul-Hussein (AS) 60-Kitab

Maqtalul- (AS).

Vitabu vihusianavyo na Abdallah bin Abbas kutoka kwake vilivyotegemezwa kutoka kwake: 61-Kitab at-Tanziilu Anhu (AS)

62-Kitab at-Tafsiiru Anhu (AS). 63-Kitab al-Manaasiku Anhu (AS). 64-Kitab an-Nikaahu wat-Twalaaq Anhu. 65-Kitab al-Faraaidh Anhu. 66-Kitab Tafsiiruhu anis-Swahanati. 67-Kitab al-Qiraa'ati Anhu. 68-Kitab al-Buyuu'u wat-Tijaaraatu Anhu. 69-Kitab an-Naasikhu wal-Mansuukh Anhu. 70-Kitab Nasabuhu. 71-Kitab Maa Asnadahu anis-Swahabati. 72-Kitab Baqiyyatu Qawlihi fit-Twaharati. 73-Kitab at-Twaharati waz-Zakaati. 74-Kitab Maa Rawahu min Ra'ayis-Swahabati. 75-Kitab Adhabaaihu wal-At'imati wal-Llibaasi. 76-Kitab al-Ftyaa wash-Shahaadaati wal-Aqdhiyati wal-Jihadi wal-Uddati wa Sharaaiul-Islaami. 77- Kitab Qaulihi fid-Duaai wal-Awdhati Wadhikril-Khairi wa Fadhli Thawabil-Aamali wat-Twibbi wan-Nujuumi. 78-Kitab Qauluhu fii Qitaali Ahlil-Qiblati wa Inkaarir-Raj'ah wal-Amri bil-Maruufi. 79-Kitab Fil-Adabi Dadhikril-Anbiyaai wa Awwalikalaamihi fil-Arab. 80-Kitab Baqiyyatu Kalaamihi fil-Arab wa Quraishi was-Swahabati wat-taabi'iina waman dhammahum. 81-Kitab Qauluhu fi Shiati Ali (AS). 82-Kitab Baqiyyatu Risaalatihi wa Khutwabihi wa Awwal Munaadhwaratihi. 83-Kitab Baqiyyatu Munaadhwaratihi Wadhikri Nisaaihi wa Wuldihi. 84-Kitab Akhbarut-Tawwabiin wa Ainul-Wardati. 85-Kitab Akhbaru Mukhtaar bin Abi Ubaidu At-Thaqafiy. 86-Kitab Akhabaru Ali bin al-Hussein (AS). 87-Kitab Abi Jaafar Muhammad bin Ali (AS). 88-Kitab Akhabarul-Mahdiy (AF). 89-Kitab Akhbar Zaid bin Ali (AS). 90-Kitab Akhbar Omar bin Abdul-Aziz. 91-Kitab Akhbar Muhammad binil-Hanafiyyah. 92-Kitab Akhbarul-

Abbas. 93-Kitab Akhbar Jaafar bin Abi Twalib. 94-Kitab Akhbaru Ummi Haaniy. 95-Kitab Akhbaru Abdallah bin Jaafar. 96-Kitab Akhbarul-Hassan bin Abil-Hassan. 97-Kitab Akhbaru Abdallah bin Hassan bin Hassan. 98-Kitab Akhbaru Muhammad bin Abdallah. 99-Kitab Akhbaru Ibrahiim bin Abdallah bin Hassan. 100-Kitab Akhbaru man Ashiqa mina ash-Shuarai. 101-Kitab Akhbaru Luqmaan bin Aad. 102-Kitab Akhbaru Luqman al-Hakiim. 103-Kitab Marajul-Fuqahau. 104-Kitab Man Khatwaba alaa Mimbari bi Shiiri. 105-Kitab Akhbar Ta'abbatwa Sharra. 106-Kitab Akhabaru Akhbarul-Aaraab. 107-Kitab Akhbaru Quraish wal-Asnam. 108-Kitab fil-Hayawaanati (al-Jawaabaati). 109-Kitab Qabaailu Nizaar wa Harbi Thaqiif. 110-Kitab at-Twibbu. 111-Kitab Twabaqaatul-Arab wash-Shuaraau. 112-Kitabun-Nahwi. 113-Kitabus-sihri. 114-Kitabu at-Twiyaratu. 115-Kitab Zajrut-Twairi. 116-Kitab Maa Ruthiya bihin-Nabii (SAW). 117-Kitab ar-Ruu'yaa. 118-Kitab Akhbaru as-Suudan. 119-Kitab al-Awdhu. 120-Kitab ar-Ruqiyyi. 121-Kitab al-Matwar. 122-Kitab As-Sahaab war-Raad wal-Barq. 123-Kitab Akhbar Amru bin Maadiy Karb. 124-Kitab Umayaatu bin Abis-Swalt. 125-Kitab Akhbaru Abil-Aswad ad-Dualiy. 126-Kitab Akhabaru Aktham bin Swaifiy. 127-Kitab Akhbaru Abdur-Rahmaan bin Hassan. 128-Kitab Akhbaru Khaalid bin Swafwaan. 129-Kitab Akhbaru Abi Nuaas. 130-Kitab Akhbarul-Madaniyyiin. 131-Kitab al-At'imah. 132-Kitabul-Ashribati. 133-Kitabul-Llibas. 134-Kitab Akhbarulujjaj. 135-Kitab an-Nikaah. 136-Kitab Maa Jaa'a fil-Hamaam. 137-Kitab Akhbaru Ruuyah bin al-Ajjaj. 138-Kitab Maa Ruwiya fish-Shataranjiy. 139-Kitab Shiiru Ubbad bin Bash-Shaar. 140-Kitab Akhbaru Abi Bakri wa Omar. 141-Kitab Man

Awswaa bi Shiiri Jama'ahu. 142-Kitab man Qaala Shiiran fi Waswiyyatihi. 143-Kitab Khutwabin-Nabii (SAW). 144-Kitab Khutwabu Abi Bakri. 145-Kitab Khutwab Omar. 146-Kitab Khutwabu Uthman bin Affan. 147-Kitab Kutubun-Nabii (SAW). 148-Kitab Rasaailu Abi Bakri. 149-Kitab Rasaailu Omar. 150-Kitab Rasaailu Uthuman. 151-Kitab Hadiithu Yaaquub bin Jaafar bin Sulaiman. 152-Kitab at-Twayyib. 153-Kitab Rayaahiin. 154-Kitab at-Tamthiil bish-Shiiri. 155-Kitab Qatwaiun-Nabii (SAW). 156-Kitab Qatwaiu Abi Bakri wa Omar wa Uthmani. 157-Kitab al-Habaab. 158-Kitab ad-Danaaniir wad-Daraahim. 159-Kitab Akhbaarul-Ahnaf. 160-Kitab Akhbaru Ziyaad. 161-Kitab al-Wufuud alan-Nabii (SAW) wa Abi Bakri wa Omar wa Uthman. 162-Kitab Akhbarul-Fursi. 163-Kitab Akhbaru Abi Daud. 164-Kitab Maqtalu Muhammad bin Abi Bakri. 165-Kitab as-Sakhaau wal-Karam. 166-Kitab al-Iqtidhaau. 167-Kitab al-Bukhli wash-Shuhhu. 168-Kitab Akhbaru Qanbar. 169-Kitab al-Alwiyatu war-Rayaat. 170-Kitab Raayaatul-Azdi. 171-Kitab Akhbaru Shuraihi. 172-Kitab Akhbaru Hassan. 173-Kitab Akhbaru Daghfalun-Nassabah. 174-Kitab Akhbaru Suleiman. 175-Kitab Akhbaru Hamzah bin Abdil-Mutwalib. 176-Kitab Akhbarul-Jinni. 177-Kitab Akhbaru Swa'a swa'atu bin Swawhaan. 178-Kitab Akhbarul-Hajjaj. 179-Kitab Akhbarul-Farazdaq. 180-Kitabuz-Zuhdi. 181-Kitab ad-Duaau. 182-Kitab al-Qiswaas. 183-Kitabu adh-Dhikru. 184-Kitabu al-Mawaaidhu. 185-Kitab Akhbaru Jaafar bin Muhammad (AS). 186-Kitab Akhbaru Musa bin Jaafar (AS). 187-Kitab Munaadwaraatu Ali bin Musa ar-Ridhwaa (AS). 188-Kitab Akhbaru Aqiil bin Abi Twalib. 189-Kitab Assayyidu ibn Muhammad. 190-Kitab Akhbaru bin Marwaan bin Muhammad. 191-Kitab Akhabrul-Arab

wal-Fursi.192-Kitab Akhbarut-Taraajim. 193-Kitab Hadiyyatu bin Hashram. 194-Akhbarul-Muhaddithiin. 195-Kitab Akhbaru Sudaif. 196-Kitab Maqtal Uthman. 197-Kitab Akhbaru Iiyas bin Muawiyah. 198-Kitab Akhbaru Abi Tufaili. 199-Kitab al-Ghaaru 200-Kitabu al-Qiradu.[1]

Tunasema: Mwenye kusoma anwani za vitabu hivi vya mwanazuoni huyu mkubwa kwa hakika itamdhihirikia na kumbainikia mambo mengi yafuatayo:

Kwamba yeye alikuwa ni Daairatul-Maarifi (ensaiklopidia) kwa maana halisi ya neno hilo kwani alindika katika elimu nyingi sana kama vile ilmul-kalaam (itikadi), fiqhi, historia, siirah, tafsiir mashairi, visomo (qiraa'aati), akhlaq (maadili), nahau, twabia (maumbile-mazingira), tiba, uchawi nasaba, uchumi na elimu nyinginezo. Jambo hili hafanikiwi kulitekeleza isipokuwa mwenye hadhi kubwa na moyo salama na safi.

Alifahamu vyema Shakhsia ya Amiril-Muuminiin (AS) na pande zake zote za kimatendo na kikauli. Hii inabainisha kushikamana kwake na imani yake kumuhusu Imam huyu na mapenzi yake kwake, na kwamba yeye anapaswa hufahamika vyema na umma huu ili uweze kuona uzuri wa maneno na matendo yake, na kwamba yeye ndiye anayestahiki kuwa khalifa baada ya Mtume Mtukufu (SAW).

Miongoni mwa hayo ni kwamba: Ametaja hotuba za makhalifa watatu ambao walimtangulia Amiril-Muuminiin (AS) na barua za kila mmoja wao kivyake. Kutokana na ufahamu wetu, huenda kusiwe na mtu mwingine yeyote aliyemtangulia kufanya hivyo na wala hakuna yeyote

[1]-Muujam Rijaalil-Hadiith-juzuu 10 \ 39.

aliyemfuatia kwa mfano huo, hata miongoni mwa ndugu zetu Ahli Sunna. Hii inathibitisha insafu na uadilifu wake, na kwamba madhehebu yetu haifichi fadhila za mtu yeyote ikiwa atakuwa na fadhila hizo. Kama ambavyo huenda kwa kuyataja haya akawa na faida na malengo mengine yasiyofichika kwa mtu mwenye mazingatio.

Usia:

Ala kulli hal, hakika mimi ninawausia watu wa Afrika ya magharibi wachukue kigezo na kufuata nyendo za mwanazuoni huyu mtukufu ambaye hadhi na elimu yake iling'ara kati ya Waislamu wote, na walee maulamaa wenye mustawa kama huu. Asiyeweza kufanya hivyo, basi awahamasishe wengine watoke na kutafuta elimu kwenye Hawza ya mji mtakatifu wa Qum na Hawza zinginezo za kielimu ili wanufaike na matone machache tu kutoka kwenye bahari ya elimu ya Ahlul-Bait (AS). Hii ni kwa sababu wao ndio hazina ya elimu, mwisho wa upole (hilm), nguzo za ukarimu na viongozi wa umma mbalimbali. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, atuingize katika kundi la watu wenye kuifahamu haki yao na katika kundi la wenye kurehemewa kwa shafaa yao, hakika Yeye ni msikivu sana muitikiaji wa maombi.

RAIHAAN WA UHABESHI NI KIGEZO KATIKA ZUHDI NA ADABU

Shekh Abu Muhammad Raihaan bin Abdallah al-Habashiy huzingatiwa kuwa ni mmoja kati ya wanazuoni na maulamaa wa karne ya sita Hijiria aliyekuwa mwanairfan, faqihi na msimuliaji wa hadithi akipokea na kusimulia kutoka kwa mwanazuoni mwenye fadhila, muhakiki na faqihi Abdul-aziiz bin Abi Kaamil at-Twaraabilsiy -Lebanon[1] - na akisimulia kutoka kwa Allama al-Karaajikiy Abil-Futuuh Muhammad bin Ali bin Uthman mwanafunzi wa Shekh Mufiid (Mungu autukuze utajo wake), na muandishi wa kitabu kiitwacho Kanzul-Fawaaid na aliyefariki dunia mwaka 449 Hijiria. Kama ambavyo anapokea na kusimulia kutoka kwa Khalifatul-Murtadha katika miji ya Halabiyyah Taqiyyu bin An-Najmi al-Halabiy muandishi wa kitabu kiitwacho Taqriibul-Maarif na aliyefariki dunia mwaka 447 Hijiria na anasimulia kutoka kwake Shaadhaan bin Jibrailu al-Qumiy.[2]

Amesema Jalalud-Din as-Suyuutwiy katika kitabu-Azhaarul-Uruush fii Akhbaaril-Hubuush: Na miongoni mwao (yaani miongoni mwa maulamaa wa Uhabeshi) ni Raihaan al-Habashiy Abu Muhammad az-Zaahid ash-Shii'i (mcha mugnu na aliyekuwa Shia) alikuwa katika miji ya Misri na kati ya maulama wakubwa wa Shia Imamiyyah, akikariri na kusoma (mara kwa mara) kitabu an-Nihaayah na adh-Dhakhiirah, na amesema: Sikuhifadhi kitu chochote na kukisahau, akifunga siku zote ambazo ni

[1]-Aliyefariki usiku wa Ijumaa tarehe tisa ya mwezi wa Shaaban mwaka 481 Hijiria.
[2]-Angalia:Taasisush-Shiah ukurasa 319.

sunna kufunga, na Ibnu Raziik[1] alikuwa akimtukuza na kusema: wanasema: Hakuna aliyetawala kati ya watoto wa Haam isipokuwa Luqman na Bilal, na mimi ninasema: Raihan ni watatu wao alifariki mnamo mwaka 560[2] Hijiria.

Na ibnu Abi Tway amesema: Baba yangu aliniambia: Mwanazuoni wa Fiqhi Raihaan alikuwa ni miongoni mwa watu waliokuwa wamehifadhi sana (mwenye hifdhi ya hali ya juu), na inasemekana: Alikuwa akifunga sana na alikuwa hali chakula isipokuwa kile anachofahamu asili yake.[3]

Naam, amesema Mwenyezi Mungu mtukufu: "Basi na aangalie mwanadamu chakula chake akilacho." [4] Kwa hivyo basi haimpasi mwanadamu au mtu mwenye akili timamu kulifanya tumbo lake kama moto ulao kila kitupwacho kwenye moto huo, hata chakula chenye shubha ukiachilia (seuze) mbali kilicho cha haramu. Kwa hivyo inampasa mtu kujiepusha na chakula cha aina hiyo, kwa sababu: "Na mji mwema mimea yake hutokeza kwa idhini ya Mola wake na ule uliokuwa mbaya hautoi isipokuwa mibaya (Nakida)."[5] Sasa kwa ajili ya kulinda na kuwa makini na chakula na akida yake Raihaan al-Habashiy akautawala mji wake au nchi yake kama alivyoutawala Bilal al-Habashiy hapo kabla (kabla yake) na pia Luqman al-Hakiim, juu yao wote salamu na amani ya Mola wa viumbe wote.

[1]-Huyu ni mfalme mwema aliyekuwa akiitwa Twalaaiu bin Raziik waziri wa dola la Fatwimiyiin na aliyeuawa mwaka 556 Hijiria.
[2]-Mustadrakul-Wasaail juzuu 3 \ 480 chapa ya Hajariyyah.
[3]-Lisaanul-Miizan juzuu 2 \ 469.
[4]-Suurat Abasa 24.
[5]-Suuratul-Aaraf aya 58.

MSIMAMO WA KIPEKEE WA IMAM KHOMEINI KUHUSIANA NA WATU WA AFRIKA

Kila mwenye kupekua na kupitia kurasa za historia ya imam mtukufu al-Khumainil-Adhiim, amani ya Mwenyezi Mungu Mtukufu iwe juu yake, kabla na baada ya ushindi wa mapinduzi ya Kiislamu yaliyobarikiwa katika nchi ya Iran, ataona na kufahamu ni namna gani Imam alisimama kwa uwezo wake wote na watu wa Afrika kwa ajili ya kutetea haki zao zilizoporwa na kuliwa kwa fujo na wakoloni wa msalaba, Wazayuni na wabaguzi wa rangi.

Katika kukaribia ushindi wa mapinduzi, alijibu swali linahusiana na kubakia au kukatwa kwa uhusiano wa kidiplomasia kati ya Iran na Serikali ya Afrika ya Kusini, ambayo ilikuwa ikiongozwa na makaburu weupe waliojiingiza na kujifanya Waafrika katika zama zile[1] na kuishi maisha ya ubaguzi wa rangi na maonevu, pia ukandamizaji dhidi ya ndugu zetu Waafrika weusi na wazawa asilia wa ardhi hiyo. Aliulizwa pia iwapo Iran ingekata kuiuzia mafuta nchi hiyo pamoja na serikali haramu ya Israili.

Alijibu kwa kusema: Ama kuhusiana na Israili ni jambo lisilo na shaka ya kwamba sisi hatutausaidia kamwe utawala ghasibu na haramu, unaokanyaga haki za Waislamu na kudumisha uadui dhidi ya Uislamu. Hali ya Afrika Kusini

[1]-Yaani mwaka 1978 Milaadia. Lakini baada ya jihadi kubwa na ya muda mrefu na isiyokatika Waafrika waliweza kuiangusha na kuiteketeza serikali ile ya kibaguzi na hiyo ilikuwa ni mwaka 1991. Kufuatia tukio hilo Iran ilianzisha upya uhusiano wake wa kidiplomasia na nchi hiyo na kuwa kama nchi zingine za Kiafrika.

pia iko wazi, kwani huo ni utawala wa kibaguzi usiothamini hata chembe utu wa mtu na kimsingi ni utawala mbovu unaomwaga kidhulma damu ya watu.[1]

Na akasema pia: Maadamu serikali ya Afrika ya Kusini haitatizama upya na kurekebisha misimamo yake ya hivi sasa, kamwe sisi hatutakuwa nayo na uhusiano wa kawaida wa kidiplomasia wala kuiuzia mafuta.[2]

Ama kuhusiana na kuzisaidia nchi zingine za Afrika na watu wa Afrika Imamu wetu mtukufu alitangaza katika sehemu nyingi ya kwamba nchi za Afrika hivi leo zinataka msaada wetu na zinatutaka msaada kwa ajili ya kukabiliana na Amerika, wageni wengine na vibaraka wao. Na akasema pia:Hakika wito wetu wa kujitenga na kuepukana na maadui wa Allah (katika msimu wa hija) ni mwangwi wa sauti ya Waislamu huko Afrika, ni wito wa ndugu na dada zetu katika dini, miongoni mwa watu wanaoishi chini ya minyororo ya dhulma ya ubaguzi wa kijahili kutokana na rangi ya ngozi yao nyeusi.[3]

Na haikuwa misimamo hii ya Imam Khomeini isipokuwa ni kwa sababu yeye ni mtoto wa Madrasa ya Ahlul-Bait wa Mtume Mtukufu (SAW), ambao walitufunza tuwe mahasimu wa madhalimu na wasaidizi wa watu wenye kudhulumiwa,[4] bila ya kutofautisha kati ya Muarabu na asiye Muarabu au mweupe au mweusi. Kwa sababu hii utakuta pia ya kwamba, Imam wa wanyonge na ambaye alikuwa akihisi na kuumia kutokana na maumivu na

[1]-Manhajiyyatu ath-Thauratil-Islaamiyyah ukurasa 514.
[2]-Kalimaatul-Qiswaar cha Imam Khomaeiny ukurasa 200.
[3]-Chanzo kilichotangulia ukurasa 200.
[4]-Nahjul-Balagha, barua ya 47, na miongoni mwa usia wa Amiril-Muuminiin (AS) kwa Hassan na Hussein (AS) ukurasa 135.

maonevu ya wanyonge, Sayyid Musa Swadr[1] aliposafari kuelekea Abidjan mji mkuu wa Ivory Coast na kukutana na Walebanoni waishio huko na kumpatia msaada wa pesa kwa ajili ya watu walio jeruhiwa huko Lebanon, aliamua kuwapa pesa hizo watu masikini wa Ivory Coast kutokana na umasikini mkubwa aliouna huko na kusema: Mali na pesa ya Abijan ni kwa ajili ya watu wa Abijan. Yaan pesa zenu hizo mnazotupatia sisi kutokana na juhudi zenu na taabu zenu ni matokeo na faida ya kazi yenu katika nchi hii, na maadamu katika nchi hii kuna umaskini, ufukara na uhitaji pesa hizo zinapasa kutumika katika nchi hii na kwa manufaa ya watu wa nchi hii, kwa sababu hakuna tofauti yoyote kati ya fukara huyu na fukara wa nchi nyingine. Hii ni kwa sababu majukumu yetu na wadhifa wetu kwa mujibu wa mafundisho ya Maimamu wetu (AS) ni kupambana na umasikini popote utakapokuwa.

Yote haya yanamfanya kila Muafrika mwenye fikra huru, mara tu baada ya kufahamu na kuifanyia uhakiki madhehebu ya Ahlul-Bait (AS), kujiunga nayo moja kwa moja na bila ya kusita kwa sababu anaona katika madhehebu hii saada na wema wa nyumba mbili (dunia na akhera) asiouona katika madhehebu nyingine yoyote. Ni kwa sababu hii ndio maana katika miaka kadhaa hivi

[1]-Imam Swadr alikuwa ni wa pekee katika zama zake na katika jihadi na kujitolea muhanga katika njia ya Mwenyezi Mungu na kuwasaidia kwake wanyonge na watu walionyimwa haki zao ulimwenguni. Ni kwa sababu hii ndio maana akatekwa nyara na mtu ambaye ni mpotovu zaidi kuliko mnyama pindi alipoitika wito wa kufanya ziyara na matembezi huko Libya, na hiyo ilikuwa ni katika tarehe 27 ya mwezi mtukufu wa Ramadhani mwaka 1398 Hijiria Qamaria sawa na 31 Agosti mwaka 1978. Tokea hapo, habari zake zilikatika na hatima yake kutojulikana hadi hivi leo ninavyoandika maandishi haya nasi tukiwa katika mwaka 1423 Hijiria sawa na 2002 Milaadia.

mwishoni wakajiunga mamilioni kwa mamilioni ya watu wa Afrika wenye fadhila na madhehebu ya Shia kwa sababu walikuta ndani yake mji wa elimu na mlango wake na maisha ya utulivu na mazuri, hasa ikiwa wafuasi wake watapata tawfiiq ya kutekeleza hukumu zake zote. Hii ni kwa sababu tumesoma ni jinsi gani kulikuwa na maisha mazuri, ya utulivu na mema katika zama za uongozi wa kiongozi wa watu wampwekeshao Mwenyezi Mungu na bwana wa maurafaau Amiril-Muuminiin Ali bin Abi Twalib (AS).

Imepokelewa na kusimuliwa ya kwamba Imam Ali (AS) alimtuma msimamizi wake kwenda Afrika, na baada ya muda yule msimamizi akatuma barua kwa Imam akisema: Hakika mali huku ni nyingi, sasa tuifanyie nini? Imam (AS) akamtumia barua na kumwambia: Wapatie masikini ili wajitosheleze na kuepukana na umasikini. Kwa mara nyingine msimamizi yule akamtumia barua Imam akisema tayari alikuwa amewapa masikini kitu cha kuwatosheleza lakini bado mali na pesa zilizobaki zilikuwa ni nyingi na kuuliza azifanyie nini. Imam akamuamuru kuwaozesha watu wote ambao walikuwa hawajaoa kwa kutumia pesa hizo. Yule bwana akawaoza wasiooa kisha akamtumia Imam (AS) pesa zilikokuwa zimebaki.[1]

Naam, wakati fikra, vitendo na mafunzo ya Imam Ali (AS) vinapotawala, Umma utaishi maisha mema, mazuri na yenye saada. Hii ni kwa sababu matendo yake ni matendo ya Mwenyezi Mungu na elimu yake ni miongoni mwa elimu ya Mwenyezi Mungu, bali yeye ndiye njia iliyonyooka na hoja juu ya watu wote. Na mwisho tunamuomba Mwenyezi

[1]-Bulghatul-Waaidhiin fil-Qiswasi wal-Mawaaidh kilichoandikwa kwa mkono.

Mungu mtukufu atufahamishe na kututambulisha mafundisho ya Kitabu chake, Sunna ya Mtume wake na mawasii wake na asitutenganishe nao duniani na akhera, kwa haki ya Muhammad na kizazi chake kitwaharifu, na tunasema mwishoni mwa maombi yetu al-Hamdu Lillahi Rabbil-Alamiin. Mimi ni mja mwenye kuhitaji dua za waumini, Muhammad Murtadha aishiye katika mji mtakatifu wa Qum.

Nimemaliza kuandika kitabu hiki jioni ya siku ya Jumanne tarehe 16\ 2 \ 1422 Hijiria sawa na 4 \ 9 \ 2001 Milaadia.

VYANZO VILIVYOTEGEMEWA KATIKA UANDISHI WA KITABU HIKI

- Qur'an Tukufu.
- Ad-Durrul-Manthuur cha Suyuutwiy-Manshuurat maktabatu Aayatullahil-udhmaa Al-Mar'ashiy an-Najafiy (Mungu autukuze utajo wake)-Qumil-Muqaddasah.
- Ad-Durrun-Nadhwiim fi Manaqibil-Aimmatil-Mayaamiim cha Shekh Jamaluddini Yusuf bin Haatam al-Baqaaiy ash-Shamiy Muassasatun-Nashril-Islaamiy-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Asfaar au al-Hikmatul-Mutaaliyah cha Swadrul-Muta Allihiin- msambazaji Mustafawiy-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Burhaan fi Tafsiiril-Qur'an cha msimuliaji Sayyid al-Bahraniy- Muassasatu Ismailiyan-Qum.
- Al-Fawaaidul-Milliyyah cha Shahiduth-Thaniy (Mugu amrehemu)- Markazul-Abhaath wad-Dirasatil-Islaamiyyah-Qum.
- Al-Ghaibatu Linnuuamaaniy (Mungu autukuze utajo wake)- Maktabatus-Swaduuq-Tehran.
- Al-Hadaaiqun-Naadhwirah cha Shekh Yuusuf al-Bahraaniy chapa Jamiatul-Mudarrisiin-Qum.
- Al-Iiqaad cha sayyid Muhammad Ali Shaah Abdul-Adhiimiy- Msabazaji Fairuz Abaadiy-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Iqbaal cha Sayyid Ibn Twawuus- Markazin-Nashri at-Taabiu Limaktabil-Iilaamil-Islaamiy-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Iswaabatu fii Tamyiizis-Swahabah cha Ibni

Hajar al-Askalaniy-Daaru Ihyaait-Turathil-Arabiy-Beirut.
- Al-Kaamilu fit-Taarikh cha Ibnu Athiir-chapa ya Daru Swaadir Beirut mwaka 1965 Milaadia.
- Al-Kafiy cha Thiqatul-Islaami al-Kulainiy-Daarul-Kutubili-Islaamiyyah-Tehran.
- Al-Kashkuul cha Bahaiy- Muassasatul-Iilamiy-Beirut.
- Al-Kasshaf cha Zamakhshariy-Nashri Adabul-Hawzah-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Khiswaal cha Swaduuq Manshuurat Jaamiatul-Mudarrisiin-Qum.
- Al-Mahaasin cha Barqiy (aliyefariki mwaka 274)- al-Majmaul-Aalamiy liAhlil-Bait (AS) - Qum.
- Al-Malhuuf alaa Qatlaat-Tufuuf cha Sayyid Ibni Twawuus (Mungu amrehemu) - Daarul-Us'wah Litwibaa'ati wan-Nashri-Iran.
- Al-Muuminuun fil-Qur'an cha Hujja Shahiid Sayyid Qassim Shubbar-chapa Jaamiatul-Mudarrisiin-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Urwatul-Wuthqaa cha Sayyid Muhammad Kaadhim al-Yazdiy (Mungu amrehemu) –chapa ya Jaamiatul-Mudarrisiin-Qumil-Muqaddasah.
- Al-Wafiy cha Faidh al-Kashaniy (Mungu amrehemu) - Maktabatul-Imam Amiril-Muuminiin Ali (AS) al-Aamah-Isfahan.
- Asaasul-Balaagha cha Zamakhshariy-Maktabun-Nashril-Islaamiy-Qumil-Muqaddasah.
- Ash-Shiah wal-Haakimuun cha Shekh Muhammad Jawad Mughniyah chapa ya sita-1984 Milaadia- Daru Maktabil-Hilaal-Beirut.

- As-Siiratul-Halabiyyah-chapa ya Misri.
- At-Tashriifu bil-Minan-cha Sayyid Ibni Twawuus (Mungu autukuze utajo wake)-Muassasatu Swaahibil-Amr-Isfahan.
- Bahrul-Maarif cha Aarif Maulaa Abdus-Swamad al-Hamadaniy (Mungu amrehemu)- Intishaarati Hikmati-Tehran.
- Baitul-Ahzaan cha Shekh Abbas al-Qumiy-Darul-Hikmah-Qumil-Muqaddasah.
- Bulghatul-Waaidh fi Qisasi Walmawaaidhi mtunzi-Makhtuti.
- Daairatul-Maarifil-Islaamiyyah ash-Shii'iyyah cha Sayyid Hassan al-Amiin chapa ya Darut-Taaruf-Beirut-mwaka 1981 Milaadia.
- Dalailus-Swidqi cha Allamah al-Mudhwaffar-Allamah al-Mudhwaffar.
- Dawaafiush-Shahiid wash-Shahadah cha mtunzi-chapa ya Sayyidish-Shuhadaai (AS)-Qumil-Muqaddasah.
- Faatwimatuz-Zahraau Bahjatu Qalbil-Mustwafaa (SAW) cha Shekh Ahmad Rahmaaniy-Muassasatul-Badri Tehran.
- Futuuhul-Buldaan cha Balaadhiriy-Darul-Kutubil-Ilmiyyah-Beirut.
- Hayaatu Muhammad (SAW) cha Muhammad Haikal-chapa ya Misri mwaka 1354 Hijiria.
- Hayatul-Hayawaanilkubraa cha Damiiriy-Intishaaraat Nasir Khosro-Tehran.
- Ikhtiyaaru Maarifatir-Rijaal cha Shekh Tusiy-chapa ya Jaamiatu Mash'had Iran.
- Ithbaatul-Waswiyyah cha Masoud-Muassasatu

Answaariyaan-Qumil-Muqaddasah.
- Ithnaa Ashariyyah fil-Mawaaidhil-Adadiyyah cha muhaddith mkubwa Abil-Qassim AL-iy al-Aamuliy (Mugu autukuze utajo wake) mchapishaji al-Hikmah: Qum.
- Jaamiu Liahkaamil-Qur'an cha Qurtubiy-Darul-Kutubil-Ilmiyyah-Beirut.
- Jaamiul-Akhbar cha mmoja kati ya wanazuoni wa karne ya saba Hijiria, Chapa ya Nashri Kitab-Iran.
- Jawaahirul-Kalaam cha Shekh Muhammad Hassan an-Najafiy-al-Maktabatul-Islaamiyyah-Tehran.
- Kalimaatul-Qiswaar cha Imam Khomeiniy-Muassasatu Nashri Aathaaril-Imaamil-Khomeiniy-Tehran.
- Kashful-Ghitwaa-cha Allamah shekh Jafar Kaashiful-Ghitwaa (Mungu amtukuze) (aliyefariki dunia mwaka 1228 Hijiria) - Maktabul-Iilamil-Islaamiy-Qumil-Muqaddasah.
- Majallatul-Aalam, la kila wiki lihusulo nyanja zote-lichapishwalo Uingereza-.
- Makatiibur-Rasuul (SAW) cha Allamah Shekh Ali al-Ahmadiy al-Miyaanjiy-Darul-Hadiith-Qumil-Muqaddasah.
- Manhajiyyatut-Thauratil-Islaamiyyah cha Imam Khomeiniy –Muassasat Nashri Aathaaril-Imam Khomeiniy (Mungu amrehemu) Tehran.
- Masaawiul-Akhlaaq cha al-Kharaaitwiy - chapa ya kwanza 1993 Milaadia- Muassasatul-Kutubith-Thaqafiyyah-Beirut.

- Mashaariqu Anwaaril-Yaqiin cha Haafidh Rajab al-Barsiy- Maktabu Nashri Thaqaafati Ahlil-Bait (AS)-Tehran.
- Muntahal-Aamaal cha Shekh Abbas al-Qumiy (Mungu amrehemu) Muassasatun-Nashril-Islaamiy-Qumil-Muqaddasah.
- Muruujudh-Dhahab cha Masoudiy-Darul-Hijrati-Qumil-Muqaddasah.
- Mustadrakul-Wasaaili cha Muhaddith an-Nuriy-Muassasatu Aalul-Bait (AS) Beirut.
- Nafsul-Mahmuum cha Muhaddith Shekh Abbasil-Qumiy (Mungu amrehemu) Manshuurat Maktabati Baswiiratiy-Qumil-Muqaddasah.
- Nafsur-Rahmaan cha Muhaddith an-Nuriy (Mungu amrehemu) chapa ya Hajariyyah-Iran.
- Nawaadirul-Akhbaar cha Faidh al-Kashaniy (Mungu amrehemu)-Muassasatud-Diraasaat wal-BuhuuthiAth Thaqaafiyyah-Tehran.
- Qaamusur-Rijaal cha Allamah Shekh Muhammad Taqiy at-Tustariy-Muassasatun-Nashriil-Islaamiy.
- Qiswasul-Anbiyaai cha Rawandiy-Majmaul-Buhuuthil-Islaamiyyah-Iran-Mash'had.
- Qurbul-Isnaad cha Hamiiriy na al-Jaafariyyaat cha Muhammad bin Muhammad bin al-Ash-Athiy-chapa ya Salman Farisiy-Qumil-Muqaddasah.
- Raudhatul-Kafiy-cha Allamah al-Majlisiy-chapa ya Baghdad.
- Raudhatul-Waaidhiin cha Abi Ali al-Fattal an-Naisaburiy (Mungu amrehemu) chapa ya Hajariyyah.

- Rihlatu Ibnu Jubairi-Daru Swaadir Beirut mwaka 1964 Milaadia.
- Safiinatul-Buhaar cha Shekh Abbas al-Qumiy (Mungu amrehemu)- Nashri Kitabkhane Sanaaiy-Iran.
- Sharhu Fusuusul-Hikam cha Qaisariy-Manshuuraat Anwaaril-Hudaa-Qumil-Muqaddasah.
- Sharhu Fusuusul-Hikam ma'at-Tas'hiih wat-Taaliq cha Sayyid Jalaalud-Din al-Ashtiyaaniy-Shirkatul-Intishaaril-Ilmiyyah wath-Thaqafah-Tehraan.
- Sharhu Nahjul-Balagha cha Ibnu Abil-Hadiid-Muassasatu Ismailiyan-Qumil-Muqaddasah.
- Sharhul-Usuulil-Kaafiy cha Swadrul-Muta'allihiin (Mugu amrehemu (chapa ya Hajariyyah-Maktabatul-Mahmuudiy-Tehran.
- Siiratu Ibni Is'haaq-Muassasatu Ismailiyyan-Qumil-Muqaddasah.
- Taarikhu Peyambare Islaam (cha Kiajemi) cha Dr. Muhammad Ibrahim Aayaatiy-chapa ya Chuo Kikuu cha Tehran.
- Taasisush-Shia cha sayyid Hassan as-Swadr (Mungu amrehemu)-Manshuurati Iilaamiy-Tehran.
- Tafsiiru Bayaanis-Sadah cha Aarif al-Janaabidhiy twamuombea malazi mema-Muassasatul-Aalamiy-Beirut.
- Tafsiirul-Baidhawiy cha Abdallah bin Omar as-Shiraziy al-Baidhawiy-Darut-Turaathil-Arabiy-Beirut.
- Tafsiirul-Mawdhuiy cha Ustadhul-Muadham Shekh Jawdiy Aamuliy (Mungu amzidishie utukufu wake) Markaz Nashri Farhangi Rajaai-Qumil-

Muqaddasah.

- Tafsiirul-Muhiitwil-Aadham cha Aarif Sayyid Haidar al-Aamuliy- al-Ma'ahad-Thaqafiy:Nuru Ali Nuru-Iran.
- Tafsiirul-Qumiy cha Abil-Hassan Ali bin Ibrahim al-Qumiy-Darus-Suruur-Beirut.
- Tafsiirul-Qur'anil-Kariim cha Swadrul-Muta'allihiin- Intishaarat Biidar-Qumil-Muqaddasah.
- Tajriidul-Iitikad cha Allamah al-Qawshajiy (aliyefariki dunia mwaka 879 Hijiria) chapa ya Hajariyyah.
- Tanqiihul-Maqaal fi Ilmir-Rijaal cha Allamah al-Maamaqaniy-chapa ya Hajariyyah.
- Taqriibul-Maarif cha Abi Swaalih al-Halabiy (Aliye fariki dunia mwaka 447)- uhakiki wa Faaris al-Hasuun-Qum.
- Thawaabul-Aamal cha Swaduuq-Intishaarat Akhlaq-Qumil-Muqaddasah.
- Wafayaatul-Aayaan - Ibnu Khalaqaan-Daaruth-Thaqafah-Beirut.
- Wasaailush-Shiah cha Hurril-Aamuliy (Mungu autukuze utajo wake) Darut-Turaathil-Arabiy-Beirut.